Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 22 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tati Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati ya Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

**MHE. ALI SAID SALUM (K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni yake Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 314

**Wilaya**

**MHE. LUCAS L. SELELII (K.n.y. MHE. STEPHEN M. KAHUMBI)** aliuliza:-

(a) Je, ni nini maana halisi ya mahali fulani kuitwa Wilaya, ni kuwa na Mkuu wa Wilaya au Halmashauri ya Wilaya?

(b) Kwa kuwa, tunapogawa fedha za Serikali za Maendeleo huzipa Halmashauri za Miji na Wilaya na Wakuu wa Wilaya hutengewa *OC* tu. Je, ni kipi muhimu kwa wananchi kati ya kupewa *DC* au Halmashauri ya Wilaya/Mji au Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, Serikali yetu inao mfumo wa Uongozi wa Nguzo Kuu Tatu, yaani Utawala (*Executive*), Bunge (*Legislation*) na Mahakama (*Judiciary*). Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kama ilivyo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wizara mbalimbali ni vyombo vya utawala ambavyo vinafahamika. Chini ya Ibara ya pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rais amepewa Mamlaka ya kuigawa nchi kulingana na atakavyoona inafaa. Hii ni katika uwezeshaji wa kutekeleza shughuli za Serikali. Ibara husika inasema hivi. Naomba kunukuu

"Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais anaweza kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mikoa, Wilaya na maeneo mengine kwa kufuata utaratibu uliowekwa". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Wilaya anateuliwa na Rais chini ya Kifungu cha 2 cha Sheria Na. 19 ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997. Jukumu kubwa la ngazi ya utawala ni utungaji wa Sera na Usimamizi wa jumla wa utekelezaji wa Sera hizo. Hivyo basi, Mkuu wa Wilaya ni Kiongozi anayemsaidia Rais katika ngazi ya Wilaya kusimamia kwa ujumla pamoja na mambo mengine utekelezaji wa Sera hizo katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa zimeanzishwa kwa mujibu wa Ibara Na. 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 145 inaeleza uhalali wa kuwepo kwa Halmashauri za Wilaya na inasema: "Kutakuwepo na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila Mkoa, Wilaya, Mji na Kijiji katika Jamhuri ya Muungano". Ibara ya 146 inatoa madaraka kwa wananchi na inasema "Vyombo vya Serikali za Mitaa vitakuwa na haki na mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipago na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa jumla"

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine kutokana na maamuzi haya ya Kiserikali katika kuimarisha madaraka kwa umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ndiyo vyombo vya utekelezaji wa Sera zote zinazotungwa na Serikali. Mkuu wa Wilaya ndiye anayesimamia kwa ujumla vyombo hivyo ili viweze kutekeleza sera za nchi. Kwa hiyo, eneo linaloitwa Halmashauri liko chini ya usimamizi wa jumla wa Mkuu wa Wilaya na

Mkuu wa Wilaya ndiyo msimamizi wa shughuli zote za maendeleo katika eneo hilo zinazotekelezwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kutokana na maelezo haya ndiyo maana fedha nyingi za miradi ya maendeleo na Matumizi mengineyo kwa makusudi zinapelekwa katika mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuwa ndiyo watekelezaji wa mipango yote ya maendeleo. Kupitia Mabaraza yao ya Madiwani, fedha hizi zinapaswa kutumika kulingana na malengo yaliyowekwa na kupitishwa na Serikali. Hata hivyo, Serikali inatoa fedha ya Matumizi ya Kawaida (*OC*) kwa Mkuu wa Wilaya ili kumwezesha naye kuangalia kwa ujumla uendeshaji na usimamizi wa shughuli mbalimbali katika uendeshaji na usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwananchi, Mamlaka za Serikali za Mitaa ni muhimu sana kwa kuwa ni vyombo vya kutekeleza mipango yao ya maendeleo. Wananchi pia wanamhitaji Mkuu wa Wilaya kuongeza *checks and balances* katika utekelezaji wa shughuli za mamlaka hizo katika shughuli nyingine mbalimbali za utawala zikiwemo uhamasishaji, ulinzi na usalama na usimamizi wa sheria nyingine zilizo chini ya Serikali kama uandikishaji wa vizazi na vifo na kadhalika. Hivyo, suala si kwamba nani ni muhimu kati ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri bali kikubwa ni mgawanyo wa majukumu kwa kila upande. Suala la nani ni muhimu zaidi kati ya Mkuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa hilo halipo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri yenye ufafanuzi mrefu bado nina maswali miwili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, katika ufafanuzi wake imeonekana ni vigumu sana kupata Wilaya hasa katika Wilaya ya Nzega lakini upo uwezekano wa kupata Halmashauri.

Je, kwa maelezo yake hayo aliyoyatoa Serikali ipo tayari kuongeza Halmashauri nyingine katika Wilaya ya Nzega chini ya Mkuu wa Wilaya mmoja?

Kwa kuwa, katika swali la pili la Mheshimiwa Stephen Kahumbi alizungumzia suala la miji midogo na katika Wilaya ya Nzega ipo miji midogo ambayo inastahili kupewa hadhi ya miji midogo kwa mfano mji mdogo wa Ndala, Bukene na Mji Mdogo wa Nate.

Je, Serikali ipo tayari kuipa hadhi miji hiyo midogo ili iweze kupata *OC* za Halmashauri ndogo kuendesha hiyo miji midogo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI(K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali miwili ya Mheshimiwa Lucas Selelii, kama ifuatavyo:-

Kuongeza Halmashauri ya Nzega inategemea wananchi mtakavyojipanga katika Halmashauri yetu mkiweka hoja na kuleta katika Ofisi ya TAMISEMI nina hakika

mtafikiriwa kama kweli hoja hiyo ni ya msingi.Kwa hiyo, suala ni lini mnahitaji, mahitaji gani, watu kiasi gani, miundombinu mnayo kiasi gani, hilo ni suala la kujadili na kuiarifu Serikali kuweza hayo mnayoyahitaji. Hali kadhalika miji midogo ni ninyi wenyewe na Halmashauri zetu kukaa na wanavijiji wale wanaohusika kuzungumzia kama mmepata kiasi ambacho kinahitajika katika mji idadi ya watu basi nina hakika Serikali itawasikiliza na kuweza kutamka rasmi kwa vigezo mtakavyoviweka ili miji hiyo midogo iweze kupandishwa hadhi. (*Makofi*)

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi kwa niaba ya Wizara inayohusika amejibu vizuri sana kwa upande wa Halmashauri na mgao wa fedha. Sasa kuna swali moja dogo la nyongeza.

Hapo zamani za kale wakati nauliza swali kuhusu Mji wa Dar es Salaam kuwa Halmashauri moja ya Jiji lakini kuwa na Wakuu wa Wilaya watatu, halafu nikauliza Morogoro Vijijini kuwa na Mkuu wa Wilaya mmoja na kuwa Halmashauri zaidi ya moja, nilisema kuwa *Commanding Chain* kuwa kwa Utawala Bora kwa kweli inampa matatizo Mkuu wa Wilaya kuongoza Halmashauri nyingi kama vile.

Tatizo la fedha liwe palepale kwa gharama zake na kila kitu libaki hapo hapo tu lakini tukija katika *Command of Chain* kumpa Mkuu wa Wilaya mmoja na kuwa na Ma – *DED* wawili hivi inawezekana kweli kwa nini hizi Halmashauri zilizobakia hizi chache kama ziko sita tu Tanzania kama Singida na Morogoro Vijijini kwa nini Morogoro Vijijini ikawa na Mkuu wa Wilaya wake na *DED* wake ambaye Halmashauri tayari ambayo ndiyo kiwango kikubwa cha fedha?

Ahsante nashukuru sana kwa ajili ya *Command of Chain. (Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa jibu hayo mambo ya zamani za kale. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI(K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Semindu Pawa.

Katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Mkuu wa Wilaya ni Mtawala, kuhakikisha kwamba kazi za Halmashauri zinaendelea kwa hiyo si lazima sana kuwa na Wakuu wa Wilaya wawili lakini nimesema kwamba kama mnataka kwamba kuwa na Halmashauri mbili inakubalika kwa sababu kila Wilaya ina Mkurugenzi wake na wale ndiyo Watendaji huyu ni msimamizi.

Kwa hiyo hata huko Dar es Salaam Msimamizi hana kazi kubwa lakini lazima awepo kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama na *Checks and balance* nilizozingumza katika jibu langu la msingi. Kwa hiyo hili halina tatizo ni kazi ya kuandaa ninyi wenyewe na vigezo vinvyohusika muweze kuomba hiyo Halmashauri au Wilaya inayotakiwa.

Na. 315

**Mgogoro wa Mipaka – Wialaya ya Kwimba na Wilaya ya Kishapu**

**MHE. ROBERT K. MASHALA (K.n.y. MHE. PAUL N. MAKOLO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, upo mgogoro wa mipaka kati ya Wilaya ya Kwimba na Wilaya ya Kishapu katika Kijiji cha Nyasamba Kata ya Bukiki.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)**alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paulo Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ulikuwepo mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Kwimba na Kishapu katika Kijiji cha Nyasamba kata ya Bubiki. Wataalam wa Idara ya Ardhi yaani Upimaji wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa kuzishirikisha Halmashauri za Wilaya ya Kwimba na Shinyanga wameshachambua ramani ya mpaka wa Wilaya hizo mbili ambazo pia ndiyo mpaka wa Mikoa hii miwili kwa kusoma *General Notice* ya 41 ya mwaka 1954 ili kurudishia alama za mpaka huo. Alama hizo kutoonekana bayana kwa wananchi ndio kilikuwa chanzo kikubwa cha kuwepo mgogoro huo. Kazi hiyo ilianza rasmi tarehe 1 Septemba, 2002 kwa Wataalam wa pande zote mbili za Mikoa na Halmashauri za Wilaya husika kushiriki kwa pamoja. Zoezi hili liligharimu shilingi 9,500,000/= zilizotolewa na Halmashauri za Wilaya za Kwimba na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba kazi hii ilimalizika kwa kuweka alama za kudumu kwenye mpaka huu. Tangu kuwekwa kwa alama hizo hakuna vitendo au dalili za kuonyesha kwamba mgogoro huu bado upo.

Na. 316

**Kusimamia Hifadhi ya Mazingira**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mapango gani wa kuwashirikisha wananchi wanaoishi mlimani katika hifadhi ya mazingira badala ya kuwahamisha wananchi na kuleta *NGOs* kusimamia mazingira kama inavyofanywa kwenye maeneo mangine.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – (ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Serikali inasisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika maandalizi na utekelezaji wa mipango na miradi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na miradi ya mazingira. Ushirikishwaji huo huhusisha wananchi wenyewe, vikundi mbalimbali wanavyoviunda na mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni muhimu kuwashirikisha kikamilifu wananchi wanaoishi milimani katika suala zima la hifadhi ya mazingira. Ndiyo maana kwa kuzingatia hilo, miradi yote inayotekelezwa na serikali huwahusisha wananchi wenyewe katika maeneo yao. Kwa mfano, jitihada mbalimbali za kuhifadhi mazingira ya milima ya Uluguru, kushirikisha *NGOs* za *Wildlife Conservation Society of Tanzania* na *CARE – Tanzania*. Aidha, kwa kupitia mradi wa *UMADEP*, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, hushirikisha wananchi wa milima ya Uluguru katika shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira ya milima hiyo. Vilevile katika maeneo mengine nchini, ipo mifano kadhaa ikiwemo *Program* ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria ambayo imehusisha sana *NGOs* na vikundi mbalimbali vya wananchi katika kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria. Aidha, kwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, Serikali inatekeleza Mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Misitu ambao mojawapo ya shughuli muhimu zinalenga ushirikishwaji wa wananchi katika kuanzisha na kusimamia misitu ya hifadhi ya vijiji, ikiwa ni pamoja na vijiji vya milimani.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa pia kwamba Kampeni ya Upandaji Miti Kitaifa inawashirikisha wananchi wote kwa ujumla kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wake. Katika kuzindua kampeni, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo yahusuyo ushirikishwaji wa wananchi suala zima la hifadhi ya mazingira, ikiwa ni pamoja na mazingira ya milimani.

Vilevile, Serikali ilisambaza Waraka wa Waziri Mkuu wa mwaka 1991 juu ya Uhifadhi wa Mazingira kwa lengo la kushirikisha wananchi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala za mazingira linagusa maisha ya kila mwananchi, Serikali kwa kupitia taasisi mbalimbali za Serikal na zisizo za Serikali, itaendelea kushirikisha umma katika utoaji maamuzi juu ya masuala ya mazingira, ikiwemo uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango na miradi mbalimbali ya mazingira.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais yananikumbusha kwamba yeye kwa sababu alikuwa Rais wa Mazingira Duniani na alikuwa Nairobi na kwa kuwa nilikuwa naye Nairobi tarehe 20/2/2005 katika mkutano wa Mazingira duniani ndipo alipojiuzulu na tulizungumza suala hili.

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Je, kutokana na majibu yake kwamba tulikuwa na Kamati hii ya Usimamizi wa Mazingira Milimani jana tu walimkabidhi barua ya kuomba maombi fulani wananchi wa kule Vijiji vya Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe na Tandai. Je, utakubaliana na maombi hayo ili wapatiwe misaada? Hiyo A.

B. Makampuni aliyoyataja *UMADEP* na suala lingine *WTCC* hawa wanaomba wale wataalam tu wa kuwaelekeza jinsi ya upandaji wa mazingira siyo kwenda kukata migomba ya wananchi kama walivyofanya mwaka jana. Sasa wananchi wameshajiunga kwenye kikundi chao kinaitwa MMO, MAWEKO na MTUKINGE watashirikiana kama ni watendaji wazuri, ni wapandaji wa miti wa milima ya Uluguru. Je, lile swali la kuhama wananchi wa milimani linatangazwa na mtu ambaye hana madaraka kule je anaweza akawahakikishia wananchi waishi kwa matumanini badala ya kuishi kwa tahadhari kama hivi sasa. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – ARCADO D. NTAGAZWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Semindu Pawa kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu barua waliyotuletea wanavikundi wa Hifadhi ya Mazingira katika Milima ya Uluguru nikiri kwamba nimeipokea na nimeshaipeleka kwa wataalam ifanyiwe kazi ipasavyo ili tutakapokuwa tumepata fedha tuchangie katika juhudi zao.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba Shirika lile nililolitaja na wataalam, ni kweli lazima tukubali kwamba wataalam kazi yao ni kuelekeza ili kile wanachokijua wananchi waweze kuelewa na pale inapokuwa ni kwa manufaa yao unakuwa umejenga uwezo zaidi wa kuhifadhi mazingira.

Kuhusu maneno yanayosemwa ya kuhamisha watu milimani wakati mwingine si vizuri kutoa maamuzi ya ki imla ni vizuri kuwashirikisha wananchi mahali walipo na ukawajengea uwezo wa kuhifadhi mazingira katika maeneo wanamoishi.

Mheshimiwa Spika, hapa mfano hai ni kama katika Wilaya ya Same na Mwanga ambayo watu wengi wanaishi milimani na wanahifadhi mazingira yale kwa sababu wanajua ndiyo uhai wao wenyewe na ukiyaharibu mazingira kweli watachukia na wanaweza wakakuchukulia hatua kama wananchi wenye hasira kali. (*Makofi*)

Na. 317

**Elimu kwa Vijana**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kanisa Katoliki lililopo Tarafa ya Kipatimu Wilayani Kilwa pamoja na kueneza huduma ya kiroho limekuwa likitoa mafunzo ya Useremala, Uashi na Elimu ya Maarifa ya Nyumbani *(Domestic Science)* kwa wasichana walimaliza Elimu ya Msingi:-

(a) Kwa kuwa, hayo majengo hayatumiki na elimu hiyo inahitajika sana kwa vijana wetu ambao hawakubahatika kupata elimu ya Sekondari. Je, Serikali inaweza kutupatia vifaa vya ufundi ili tuweze kuondoa tatizo la ajira kwa vijana?

(b) Kwa kuwa, kuona ni kuamini. Je, Waziri yupo tayari kufanya ziara Kipatimu mwezi Mei, ili aweze kutoa uamuzi kabla ya mwaka mwingine wa fedha?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Omar Saidi Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Juhudi za kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana linategemea mchango na jitihada za wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za kidini. Napenda kutumia fursa hii kulipongeza Kanisa Katoliki lililopo katika Tarafa ya Kipatimu Wilayani Kilwa kwa jitihada wanazochukua katika kukabiliana na tatizo hilo. Pia natoa wito kwa wadau wengine kuiga mfano huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Saidi Chubi, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia *VETA* imekuwa ikisaidia vyuo vya Ufundi Stadi vya taasisi zisizo za kiserikali na vya watu binafsi kwa utaratibu maalum. Namshauri Mheshimiwa Mbunge amwambie mmiliki wa Chuo awasiliane na Mkurugenzi wa *VETA* kanda ya Kusini aliyepo Mtwara kwa maelekezo ili aweze kupata msaada huo.

(b) Napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kunialika kutembelea Kipatimu. Mwaliko huo ni ushahidi wa jitihada za Mheshimiwa Mbunge kupambana na tatizo la ajira kwa Vijana na kuinua maendeleo ya wananchi kwa ujumla jimboni kwake. Ijapokuwa sikuweza kufanikisha nia hiyo nzuri mwezi Mei kama tulivyotarajia, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu kupitia *VETA* itakuwa tayari kushirikiana naye kufuatilia upatikanaji wa vifaa muhimu vya ufundi vinavyotakiwa, pindi taratibu zote zinazotakiwa zitakapokamilishwa na wahusika.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri yenye matumaini ya Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya Chuo hiki cha Kipatimu. Je, atakuwa tayari kutuhakikishia kwamba vijana wetu wanaomaliza

*VETA* katika Kanda ya Kusini na maeneo mengine wanapata vifaa ili wakitoka pale kweli waweze kujiajiri?

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maria Watondoha kama ifuatavyo.

*VETA* wameshaanza utaratibu wa kutoa vifaa hawajaweza kutoa vifaa vyote kwa ukamilifu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba uwezo wa *VETA* utakapokuwa unaongezeka ndivyo jinsi ambavyo watakavyokuwa wanaongeza utoaji wa vifaa.

Na. 318

**Upimaji wa Viwanja Katika Miji**

**MHE. PAUL P. KIMITI (K.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Miji mingi nchini wananchi wamejenga kiholela kutokana na kutopimiwa viwanja na matokeo yake kunaharibu mandhari ya mji husika:-

(a) Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kupima viwanja katika miji na kuwauzia wananchi?

b) Je, sheria husika inasemaje pale ambapo Wizara ya Ardhi inapopima kiwanja na kutoa hatimiliki lakini Wizara ya Ujenzi inakuja kubomoa kwa madai kuwa ni eneo la barabara?

c) Je, kama Wilaya ya Nkasi ikitaka kukopa fedha za kupima viwanja kutoka *Revolving Fund* kama ilivyowahi kukoposhwa na kurejesha kwa faida itapewa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu umuhimu wa kupima viwanja katika miji yetu. Upimaji unaofanyika katika miji yetu ni kwa misingi ya kutoa huduma kwa wananchi wote. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya viwanja mijini, Serikali imeona kuna umuhimu wa kupima viwanja na wananchi wachangie sehemu ya gharama ya viwanja hivyo kwa kuwauzia. Nia ya kupunguza ruzuku kutoka kwa walipa kodi kulipia upatikanaji wa viwanja na kuondoa kabisa ulanguzi wa viwanja mijini. Mpango huu umetekelezwa kwa mafanikio katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2002 – 2005 na unaendelea kutekelezwa katika Jiji la Mwanza. Hivi sasa, Serikali inafanya tathmini ya

mahitaji ya viwanja mijini kwa nchi nzima ili kutengeneza ratiba ya kupima viwanja hatua kwa hatua mijini.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria za Ardhi na Mipangomiji ziko wazi katika kazi zote zinazofanyika kwenye ardhi na uendelezaji wa makazi nchini. Aidha, kutokana na utata uliozuka, kati ya milki za viwanja na hifadhi za barabara, Serikali imeunda Kamati ya Watalaam wa Wizara ya Ardhi na Wizara ya Ujenzi kuchunguza tatizo hili. Mara Kamati ya Watalaam itakapokamilisha kazi yake, Serikali itatoa uamuzi ili kuondoa utata uliopo.

(c) Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kwa kurudisha fedha zote za mkopo kutoka mfuko wa *lot Development Revolving Fund (PDRF.* Wizara iko tayari kuipatia mkopo mwingine kutoka mfuko wa *PDRF,* kulingana na andiko la mradi litakalo wasilishwa na Halmashauri husika. Aidha, natoa rai kwa Halmashauri za Miji na Wilaya zingine zinazopata fedha kutoka kwenye mfuko huu, kuzitumia vizuri na kurejesha mkopo kutokana na mauzo ya viwanja kwa wanaogawiwa viwanja hivyo. Pia, mkopo urejeshwe kwa wakati ili mfuko uweze kuzunguka na kuendelea kutoa huduma kwenye miji mingine.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kujua hivi kwa kuwa hivi sasa viwango vinavyotumika katika kutoa fidia ya nyumba zinazo bomolewa sehemu mbalimbali ni kidogo sana na kwa sababu wanaosimamia uthamini wa nyumba zenyewe ni Serikali yenyewe. Je, Mheshimiwa Waziri haoni ya kwamba wakati umefika ili kuwa na Utawala Bora wanaodhamini wawe ni watu binafsi pamoja na Serikali kwa pamoja isionekane ya kwamba upande mmoja unaonea upande mwingine? Mheshimiwa Spika, la pili, hivi ni kigezo gani kinachotumika katika kutoa gharama za kupima viwanja hasa ukilinganisha eneo hilo moja kiwanja kimoja kinakuwa shilingi laki mbili na kingine milioni moja na kingine kinafika mpaka milioni moja na nusu. Ni vigezo vipi vinatumika kwa sababu maeneo yenyewe tunafahamu na tofauti ya viwanja si kubwa sana mpaka ilete tofauti kubwa sana ya viwango vikubwa namna hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Paul Kimiti maswali yake miwili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Jinsi ya kuwashirikisha wataalam hakuna sehemu ambayo Serikali inakataa kuwashirikisha wataalam binafsi na Serikali ni kutokana na upatinaji wa watu hao ndipo tunafanya lakini mara nyingi tunachukua Serikali. Watu binafsi tunawatumia pale panapokuwa ni lazima, lakini na wao pia tumekuwa mara nyingi tunawaambia wajitokeze lakini wawe na viwango vinavyotakiwa katika kufanya kazi hiyo. Kigezo cha ulipiaji viwanja kutofautiana ni lazima vitofautiane kwa sababu inategemea eneo lenyewe linalopimwa, kwa mfano eneo la baharini hata kama ni ekari moja itatofautiana na eneo ambalo liko milimani au liko kwenye mbuga. Sababu ya soko ya kiwanja chenyewe lakini pia inategemea kiwanja hicho hicho kinaanza kuwa katika eneo la mjini katikati ya

mji kwa mfano Dar es Salaam litakuwa na soko kwa sababu ya watu hufikia eneo lile kwa urahisi kuliko sehemu nyingine.

Pia kunaweza kuwa na miundombinu mingi katika eneo lile kwa hiyo linaongeza gharama ya upimaji wa mradi huo.

Na. 319

**Wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu**

**MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza: Kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu nchini huchangia pato la Taifa; na kwa kuwa juhudi zao hukwamisha na ukosefu wa mtaji wa kununulia vifaa vya kisasa kama *pump* na *Generators*:-

Je, Serikali imewashirikisha vipi wachimbaji wakubwa kuwasaidia wachimbaji wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini , napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini huchangia katika pato ya Taifa na Serikali inathamini mchango wao huo. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* chini ya Wizara ya Kazi, Vijana na Maendeleo ya Michezo, idadi ya wachimbaji wadogo nchini ni takriban 1,000,000 na wengi kati ya hawa wanajishughulisha na uchimbaji wa dhahabu. Aidha, mchango wao katika pato la Taifa unakadiriwa kuwa ni asilimia 0.2. Kutokana na mchango wao, Wizara yangu imekuwa ikihakikisha kuwa wachimbaji hao wanaondokana na tatizo la ukosefu wa mtaji wa kununulia vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu na Taasisi zingine, imekuwa ikiwahamasisha na kuwataka wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo kuwa na ushirikiano mzuri wakati wa kuendesha shughuli zao za uchimbaji. Uhusiano na ushirikiano huo mzuri ndio utaowawezesha wachimbaji hao kufanikiwa katika (a) Utafutaji madini, (b) Kukopeshwa na kuazimwa vifaa na (c) Kuingia ubia na kuchimba madini.

Mheshimiwa Spika katika utafutaji wa madini, wachimbaji wadogo huwaruhusu wachimbaji wakubwa kuingia katika maeneo ya leseni zao kwa mikataba ya malipo. Kwa mfano, wachimbaji wadogo wa Sekenke Wilayani Iramba waliingia Mkataba na Kampuni ya *Barrick Gold* ambapo wachimbaji wenye leseni katika viwanja vinne

wanalipwa Tsh. 900,000/= kwa kila leseni kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mkataba utaisha 31/12/2005 na mwisho wa mkataba hao wachimbaji wadogo wana hiari ya kuuza leseni zao hizo kwa *Barrick* kwa jumla ya shilingi milioni 9 kwa kila leseni.

Kuhusu kukopeshwa au kuazimwa vifaa, mfano mzuri ni mchimbaji Enock Mwita wa Nyamongo, Tarime ambaye aliingia mkataba na Kampuni ya Afrika Mashariki *Gold Mine (AMGM)* wa kufanya utafiti katika eneo la viwanja vyake. Mchimbaji huyo aliweza kupata fedha pamoja na kukopeshwa vifaa vya uchimbaji kama vile mashine za kuvuta maji (*water pumps*) na mashine ya kuingiza hewa kwenye migodi (*compressors*)

Mheshimiwa Spika, upo pia ushirikiano katika kuchimba madini ambapo wachimbaji wakubwa huchimba kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo kwa makubaliano. Kwa mfano, Kampuni za *AAPS* na *Amazon Trading* za Tanga zimeingia mikataba na wachimbaji wadogo wa madini ya vito kule maeneo ya Umba ambapo wachimbaji wadogo hulipwa asilimia 20 ya mapato yanayotokana na machimbo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ushirikiano mzuri kati ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo ili wachimbaji wakubwa waweze kuwasaidia wachimbaji wadogo vifaa vya kisasa na ujuzi. Aidha, Wizara yangu inaangalia upya shughuli za *STAMICO* ili Shirika hili la umma lihudumie pia wachimbaji wadogo wadogo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na utaratibu wa wachimbaji wakubwa wakubwa wanapoingia hapa nchini huwaondoa wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo yao na kusababisha vurugu katika maeneo hayo. Je, Serikali inaonaje kuwatengea sehemu maalum wachimbaji wadogo wadogo ili wasiingiliwe na wachimbaji wakubwa wakubwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwanza si sahihi sana kusema kwamba upo utaratibu wa wachimbaji wakubwa kuwaondoa tu kienyeji wachimbaji wadogo. Mchimbaji mkubwa akifika katika eneo ambalo wachimbaji wadogo tayari wana leseni akitaka kuingia katika eneo hilo lazima akubaliane na hao wenye leseni na wanakubaliana kwa malipo. Kwa hiyo, isitokee dhana kana kwamba wachimbaji wakubwa wakifika mahali kazi yao ni kuwatimua kienyeji wachimbaji wadogo si kweli hata kidogo. Serikali ipo inawalinda kwa sababu huyo mwenye leseni ndiyo mwenye mali ya kile kiwanja. Lazima ukitaka kuingia ukubaliane naye kwa mkataba maalum kwa malipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rai kwamba wachimbaji wadogo watengewe maeneo maalum ya kuchimba, hilo limeanza kufanyika. Kwa mfano, kule katika Mkoa wetu wa Singida kuna eneo linaitwa London sasa kulikuwa na mgogoro kati ya waliokutwa pale

na mchimbaji mkubwa. Hivi majuzi Wizara ya Nishati na Madini imekuja imeweka mpaka kwamba wachimbaji wadogo wenye eneo hilo wapata leseni na huyo mchimbaji mkubwa kapata eneo lake. Kwa hiyo, utaratibu huu umeanza kutekelezwa.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Kanda ya Ziwa na Magharibi ya nchi yetu ni maeneo yaliyo madini mengi na ya aina mbalimbali. Lakini wakati huo huo ni kwamba wananchi wengi hasa vijana wanaomaliza shule na wengineo wamejitumbukiza katika kazi ya uchimbaji wa madini na mara nyingi wamepoteza maisha yao katika kuwatumikia wachimbaji wakubwa wakubwa. Lakini nchi nzima ina Chuo kimoja tu cha kufundisha elimu na maarifa kuhusu uchimbaji wa madini. Je, ni lini Serikali itakubali kuongeza Chuo kingine kwa kile cha hapa Dodoma kwa kuweka Chuo cha Madini katika Kanda ya Ziwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, hii Sekta ya Madini ni moja ya Sekta ambayo ni miaka ya hivi karibuni tu imeanza kuibuka. Ni Sekta mpya ambayo sasa hivi ndiyo inaanza kushika kasi na kwa kiwango cha uchimbaji kilichopo sasa Chuo kimoja kilikuwa kinatosheleza ambacho kiko hapa Dodoma, Chuo cha Madini. Lakini jinsi Sekta hii inavyopanuka kwa haraka kwa sababu sasa wachimbaji wakubwa wanakuja kwa wingi ndani ya nchi. Wachimbaji wadogo vilevile wenyewe wanaongezeka sasa hivi wako karibu milioni moja na wote hao wanataka wapate ujuzi ili Sekta hii iweze ikatekelezwa kwa ujuzi. Kwa hiyo, suala la kuanzisha Chuo kingine ni suala muafaka na muda muafaka ukifika litatekelezwa na Kanda ya Ziwa itafikiriwa.

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea tu kidogo kwenye majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hili linalotoa madini kwa wingi na linaelekea kuwa na uwezekano wa kuendelea kutoa madini mengine zaidi. Serikali imeshakamilisha mazungumzo na Kampuni ya *Golden Pride* kuanzisha Tawi la Chuo Kikuu *Faculty* ya Madini pale Nzega. Kwa hiyo, taaluma hizi zitaendelea kutolewa kuwakaribia wananchi wenyewe ambao wanahusika na utoaji wa madini.

Na. 320

**Sera ya Sekta ya Ujenzi**

**MHE. HAMISI J. NGULI (K.n.y. MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Baraza la Ujenzi wa Taifa (*National Construction Council*) kama mwendelezaji wa sekta ya ujenzi nchini, ndicho chombo kinachotegemewa sana katika utekelezaji wa sera ya sekta ya ujenzi hasa katika kuieneza, kuratibu na kutoa ushauri

na kwa kuwa katika kitabu cha sera Serikali imeona kuwa baraza lina upungufu wa fedha na uwezo wa kisheria katika kutimiza majukumu yake:-

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kuliwezesha baraza kupata fedha linazohitaji kwa kutengewa kwenye Bajeti au kwa kuliwezesha kupata vyanzo vingine vya mapato yatakayokidhi mahitaji yake?

(b) Je, Serikali iko tayari kuleta Muswada wa Sheria Bungeni inayotoa uwezo wa kuliwezesha Baraza kutimiza wajibu wake kikamilifu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo: Baraza la Taifa (*National Construction Council*) lilianzishwa chini ya Sheria Na.20 ya mwaka 1979. Kulingana na Sheria inayounda Baraza la Taifa la Ujenzi, majukumu makuu ya Baraza ni kama yafuatavyo:-

(a) Kusimamia na kuratibu maendeleo ya Sekta ya Ujenzi Nchini na kushauri kuhusu sera, mipango na mikakati ya kukuza sekta;
(b) Kutoa ushauri wa kiufundi (*Technical Audit*);
(c) Kutoa mafunzo kwa Washauri wazalendo;
(d) Ukusanyaji wa takwimu za ujenzi na kufanya utafiti;
(e) Kuchapisha na kusambaza habari kuhusu shughuli za sekta; na
(f) Utoaji wa miongozo ya kiufundi ikiwa ni pamoja na kanuni za zabuni.

Baada ya maelezo hayo mafupi kuhusu majukumu ya Baraza la Taifa la Ujenzi, sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Ismail Iwvatta kwamba Baraza la Taifa la Ujenzi lina wajibu mkubwa katika kuratibu na kuongoza utekelezaji wa Sera ya Ujenzi ambayo imepitishwa na Serikali mwezi Februari, 2003. Aidha, ili utekelezaji wa Sera ya Ujenzi na majukumu mengine ya Baraza yaweze kuwa na ufanisi, ni dhahiri Baraza linahitaji kuimarishwa kisheria na kifedha kwa maana ya mapato ya Baraza. Serikali inayatambua masuala hayo ya msingi na hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa kama vile:-

(i) Kulitengea Baraza Bajeti yake ya mwaka kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake muhimu kama vile fedha za mishahara ya wafanyakazi na fedha nyingine kwa ajili ya matumizi mengineyo.

(ii) Kuifanyia marekebisho Sheria Na.20 ya mwaka 1979 iliyounda Baraza. Sheria ya sasa hailiwezeshi Baraza kuwa na vyanzo endelevu vya fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

(iii) Kubuni mbinu za kupanua wigo wa mapato ili kukidhi mipango ya Baraza na ambayo itapanuka sana kutokana na kutekeleza Sera ya Ujenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshaanza maandalizi ya marekebisho ya Sheria Na. 20 ya mwaka 1979 inayounda Baraza la Taifa la Ujenzi. Muswada wa Mapendekezo kuhusu marekebisho ya Sheria hii umeshajadiliwa na kikao cha Makatibu Makuu (*Inter – Ministerial Technical Committee* (*IMTC)* na sasa rasimu itawasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri wakati wowote kuanzia sasa.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri kwamba Baraza hili lina shughuli muhimu ya kuishauri Serikali kwa majukumu yake ambayo limeundwa; na kwa kuwa yaelekea bado Serikali inaendelea kufanya taratibu hizo za kuliongezea Baraza fedha na vyanzo vya fedha na kufanya taratibu za kisheria ili liweze kuwa na uwezo wa kukamilisha majukumu yake. Lakini yaelekea bado Serikali haijakamilisha. Sasa, je, ni kwa nini sasa Serikali ilitanguliza kulipa Baraza hili majukumu ya kufanya wakati fedha pamoja na uwezo wa kisheria ulikuwa bado haujatekelezwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba kwa kawaida unaandaa na kukamilisha sera halafu unatunga sheria kutekeleza sera na sera inakupa misingi ya yale unayotaka kuyatekeleza na sheria inakupa utaratibu wa kutekeleza yale yaliyomo katika sera. Sasa katika jibu letu la msingi nimesema Sheria ya Baraza ni ya mwaka 1979, sera baada ya kuifanyia rejea, sera mpya imetolewa mwaka 2003. Kwa hiyo, tunaposema ndani ya Serikali kwamba tunaendelea kufanya utaratibu na tumesema tutakapokamilisha rejea ya sheria hiyo ya mwaka 1979 ili itekeleze majukumu yaliyotamkwa katika sera bila shaka haya aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge katika msingi wa kuuliza swali kwamba hatua zichukuliwe, tuko katika mchakato wa kuchukua hatua hizo.

Na. 321

**Maeneo Korofi katika Barabara Kuu Nchini**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa sehemu korofi katika barabara kuu nyingi hapa nchini zikiwemo zile za Mikoa na Wilaya zinaendelea kuhatarisha maisha na mali za wananchi pamoja na sehemu ya barabara ya Singida – Mwanza kwenye milima ya Sekenke Wilayani Iramba:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa tatizo hili ni la Kitaifa na linafaa kushughulikiwa na Taifa *(TANROAD)* na sio kuziachia matatizo hayo Halmashauri za Wilaya, hali ikijua kuwa hazina uwezo wa kifedha na kiufundi?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu sehemu korofi kwenye milima ya Sekenke ambapo mara kwa mara wananchi wanaendelea kupoteza maisha na mali zao?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kurudishia ile lami nyepesi iliyowekwa zamani ili kunusuru upotevu wa maisha na mali za wananchi wakati barabara ya Dodoma – Singida - Mwanza inayojengwa sasa ikikamilishwa kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Mlumba Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* imeweka mikakati madhubuti katika Mpango Mkakati *(Strategic Plans)* na Mpango wa Utekelezaji (*Business Plans*) kudhibiti maeneo yote korofi kwenye barabara Kuu na za Mikoa kwa jinsi Bajeti itakavyoruhusu. Barabara zingine ambazo ziko chini ya Halmashauri zitashughulikiwa na mamlaka husika kwani uwezo mdogo wa Serikali wa kuzifanyia matengenezo barabara hizi unajulikana hata zikihamishiwa *TANROADS.* Aidha, pale ambapo utahitaji utaalam zaidi na ambao unapatikana *TANROADS,* tutashirikiana kutatua matatizo kwa kadri yanavyojitokeza.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu sya swali la Mheshimiwa Leonard Shango kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mkopo kutoka Benki ya Dunia *(IDA)* kugharamia ujenzi wa barabara kati ya Singida hadi Shelui kwa kiwango cha lami na kusaini mikataba ya ujenzi kwa sehemu ya Sekenke – Shelui, tarehe 24 Januari, 2005 na sehemu ya Singida – Sekenke tarehe 29 Aprili, 2005. Mkandarasi tayari upo kwenye eneo la kazi akijiandaa kuanza kazi yenyewe. Naamini kazi zitakapokamilika tatizo la wananchi kupoteza maisha na mali zao litaisha japo mara nyingine barabara inapokuwa nzuri ndio ajali zinakuwa nyingi kutokana na madereva kuendesha magari kwa mwendo wa kasi kupita viwango vinavyoruhusiwa pamoja na matumizi mabaya ya barabara za lami.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Iramba, namwomba Mheshimiwa Waziri apokee shukrani za

wananchi wa Wilaya ya Iramba kwa Serikali kutimiza ahadi yake kwa kuanza kujenga ile sehemu ya barabara kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge *Hansard* wanasema hawakusikia maneno yako, *Microphone* iko mbali hebu anza upya.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninaomba radhi. Kwanza kabisa naomba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Iramba Mheshimiwa Waziri apokee shukrani kwa Serikali kuanza sasa kujenga sehemu ile ya barabara kwa kiwango cha lami.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa lami inajengwa kwa sehemu ile ya barabara, lakini wananchi wataendelea kuumia, kupoteza maisha na kupata uharibifu wa mali zao. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu tatizo hilo ambalo limekuwepo kwa miaka mingi sana?

(b) Mheshimiwa Waziri pia amekiri kuwa Halmashauri hazina uwezo katika kushughulikia barabara ambazo ziko chini ya huduma zake. Je, Serikali itakubali ombi la wananchi wa Kata za Kidalu na Kisiriri kusaidiwa kiufundi na *TANROADS* kujenga ile sehemu ya milimani kutoka Kisiriri mpaka Kidalu pale mlimani kusaidiwa kujenga kwa sababu Halmashauri haina uwezo kabisa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu Serikali kupokea shukrani, naomba niseme sisi Serikali ni watumishi wa watu, wananchi ndiyo waliotuajiri kazi na wanaposema tunatimiza wajibu wetu wanatutia moyo na tunawashukuru wao na kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya pili tumesema kwamba barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa anasema Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na yote hayo bado kutakuwa na matukio ya wananchi kupoteza maisha nadhani hakusema moja kwa moja kutokana na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, hili nadhani ni tatizo katika jamii ya binadamu unapotatua tatizo moja. Sasa hivi katika hiyo tunataka kutatua tatizo la kutokuwa na barabara ya lami, lakini tutakapokuwa na barabara ya lami tutapata tatizo jipya la watu kuendesha magari kuzidi kiwango kinachotakiwa na kusababisha ajali na kupoteza maisha ya watu. Tunachoweza kusema na siku zote tunashauri wale wanaoendesha magari na hata waenda kwa miguu na wapanda baiskeli wawe waangalifu katika matumizi ya barabara iwe ni ya lami au barabara ya changarawe ambazo ni nyingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezo wa Halmashauri na kutoweza kujenga maeneo ya Kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge na kusema ni vipi *TANROADS* itasaidia Halmashauri kiufundi.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba Halmashauri haizuiwi kuwasiliana na *TANROADS* ili kupewa ushauri wa kiufundi na pale inapowezekana Halmashauri iweze kupata huduma kutoka *TANROADS* ikiwa ni pamoja na Halmashauri kulipia huduma ya *TANROADS* ikiwa ni sehemu au kazi ya kujenga sehemu ambayo wao hawawezi kufanya hivyo.

Na. 322

**Tanzania Kuridhia Makubaliano ya Ununuzi Serikalini**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni Mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organization*); na kwa kuwa Shirika hilo linawataka wanachama wake waridhie kwa hiari makubaliano ya ununuzi Serikalini *Government Procurement Agreement (GPA):-*

Je, ni sababu gani zinazoizuia nchi yetu kuridhia makubaliano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, makubaliano ya ununuzi Serikalini au *Government Procurement Agreement (GPA)* ambayo hadi sasa ina nchi wanachama 13 tu ilisainiwa tarehe 15 Aprili, 2004. Nchi tisa ziko kwenye majadiliano ya kujiunga na nchi kumi na moja bado ni watazamaji *(observers)* ikiwemo Cameroon kama nchi pekee ya Kiafrika. Lengo la *GPA* ni kuweka zabuni za Serikali wazi kwa ushindani wa Kimataifa kwa makampuni ya nchi zilizoridhia makubaliano hayo. Kwa mantiki hiyo *GPA* inaondoa vikwazo vyote vya ushiriki wa kampuni za nje kushiriki katika zabuni ndani ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo: Tanzania kama nchi nyingine nyingi haijaridhia makubaliano ya *GPA* kwa sababu kwa kufanya hivyo itakuwa imefungua mipaka yake kwa kampuni za nje zenye uwezo zaidi na hivyo kuzidi kuendeleza kudumaza kampuni za ndani ya nchi ambazo bado ni changa na hivyo zinahitaji kulindwa.

Mheshimiwa Spika, kama itakavyokumbukwa katika Mkutano wa kumi na saba wa Bunge lako Tukufu Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 ambayo ina

vipengele vya kulinda kampuni za Kitanzania ilipitishwa. Kwa mfano kifungu 49 kinatoa upendeleo kwa kampuni za Kitanzania zinazoshindana na kampuni za nje kwa kuzitengea zabuni zisizozidi kiasi fulani cha thamani.

Mheshimiwa Spika, endapo Tanzania itaridhia *GPA,* tutalazimika kuondoa vipengele husika na hivyo kuruhusu kampuni za ndani na nje kushindana bila upendeleo wowote.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba niulize kwamba sasa kama misingi yenyewe ndiyo hiyo ambayo amezungumza Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa kwa nini tuliingia katika mkataba huo *in the first place*. Kwa nini ilibidi sisi tujiingize katika makubaliano hayo?

(b) Ni kwamba mimi nina wasiwasi kwamba wakati mwingine tusipoingia katika makubaliano au mikataba hii ya Kimataifa tunakuja kupata matatizo baadaye kama tulivyoyapata ya mkataba wa ununuzi wa vifaa mbalimbali katika *IPTL* ambapo mpaka hivi sasa unatuweka katika hali mbaya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini juu ya uhusiano wa hayo manunuzi pamoja na suala nzima la ununuzi wa Kimataifa kama lilivyoulizwa swali?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, kwanza sisi hatujaridhia yale makubaliano kama nilivyojibu katika jibu la msingi. Kilichoelezwa hapa ni kwamba katika taratibu za Shirika la Biashara Ulimwenguni *World Trade Organization* kuna kipengele ambacho kinahitaji nchi wanachama waridhie hayo makubaliano.

Lakini mpaka sasa hivi kama nilivyosema ni nchi 13 tu ndiyo zimeridhia na nchi nyingi bado hazijaridhia na sababu nilizozitoa kwa upande wetu Tanzania ni kwamba tukifanya hivyo tunafungua milango kwa makampuni ya nje ambayo yana nguvu zaidi kuliko makampuni yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nia yetu sisi hapa ni kulinda makampuni yetu yakae yanashindana yenyewe kwa ndani kwa sababu bado ni machanga. Kwa hiyo, hata wasiwasi wake huo aliouliza katika swali la (b) kusema kweli haupo kwa sababu nia ni kulinda makampuni yetu ya ndani. *(Makofi)*

Na. 323

**Simu za Mkononi – Sikonge**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Sikonge ndio pekee iliyobaki bila kuwa na mtandao wa simu za mkononi wala *TTCL;* na kwa kuwa wananchi wamekuwa wakiahidiwa mara kwa mara juu ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Hayati Dr. Omari Ali Juma, aliyoitoa wakati wa uhai wake kwenye kampeni za mwaka 2000:-

(a) Je, Serikali inaweza kutuambia sasa kwamba, mawasiliano hayo yatapatikana lini kutokana na ahadi zake za kila linapoulizwa swali hapa Bungeni?

(b) Je, mtambo uliopo Sikonge uliochakaa na kutengenezwa kila wakati bila mafanikio una faida kwa *TTCL* au una hasara na kama una hasara, kwa nini *TTCL* isilete mtambo wa kisasa Wilayani Sikonge ambapo kwa sasa kuna wateja zaidi ya 200 wanaohitaji huduma hiyo ya simu na wameweka *line* moja chakavu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sikonge siyo pekee iliyobaki bila kuwa na mtandao wa simu za *TTCL.* Mji wa Skikonge unahudumiwa na mtambo wa *TTCL* wa kukoroga wenye jumla ya njia 70 na wateja wanaofaidika na huduma hiyo hadi sasa ni 41 tu. Pia Mji huo umeunganishwa na Tabora kupitia Mtambo wa redio wa *analogue* wenye njia mbili *(2 channel Motorola Radio System).* Njia moja ina matatizo ya maingiliano ya masafa (*radio interference*) na redio za Idara ya Wanyamapori na juhudi zinaendelea kurekebisha dosari hiyo.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara imejitahidi kuwahamasisha Makampuni ya simu za mikononi waone umuhimu wa kufikisha mawasiliano ya kisasa katika Mji wa Sikonge. Pia waone uwezekano wa kubadilisha mitambo ya *analogue* katika eneo hilo. Takriban makampuni yote yameonyesha nia thabiti ya kufanya hivyo pale hali ya fedha ya makampuni zao itakapotengemaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali duni ya kifedha inayoikabili Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL),* ni vigumu kueleza kwa uhakika kwamba mawasiliano ya simu za kisasa yatapatikana lini kule Sikonge.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nafurahi kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Sikonge kuwa Kampuni ya Simu ya *Celtel* inategemea kufikisha mawasiliano ya simu za mkononi katika Mji wa Sikonge mwaka huu kabla ya mwezi Desemba.

Mheshimiwa Spika, mtambo uliopo Sikonge huingiza wastani wa Shs.150,000/= kwa mwezi, hiki ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na gharama za kuendesha hicho kituo yaani kwa maana mishahara na gharama zingine za matengenezo. Kwa hiyo, kituo cha Sikonge kwa kweli kinatoa tu huduma kwa sababu hakiingizi faida kwa Shirika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni matumaini ya Wizara yangu kwamba sehemu za vijijini kule Sikonge na kwingineko hapa nchini zitapata huduma za simu mara baada ya kuanzishwa kwa mfuko wa *Rural Access Fund* ambapo maandalizi yake karibu yamekamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Said Juma Nkumba ameridhika. Tunashukuru na muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Kwa hiyo, sasa tunaendelea Waheshimiwa Wabunge.

Kuna tangazo moja la Kikao cha Kamati nayo ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba anaomba niwatangazie Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 22 saa tano asubuhi katika ukumbi Na. 227. Hiyo ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Waziri Maokola-Majogo, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho asubuhi katika viwanja vya Bunge, pale viwanja vyetu vya burudani kutafanyika shughuli za uzinduzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusu MKUKUTA. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria uzinduzi huo ambao utaanza, mwenyewe anasema utaanza saa 2.30 asubuhi. Lakini tufanye saa 3.00 ndiyo saa zetu za kawaida. Uzinduzi wa MKUKUTA katika viwanja vya Bunge kesho.

Mheshimiwa Waziri anasema shughuli hiyo itaendeshwa kwa mfumo wa semina zetu za kawaida. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Kamanda wa Kikosi cha Wabunge watakao kwenda kupiga shabaha kesho Mheshimira Parmukh Singh Hoogan, anasema idhini ya Waziri wa Ulinzi imepatikana kwa Wabunge wanaopenda kwenda Makutupora kwa ajili ya zoezi la kupiga shabaha hapo kesho waweze kufanya hivyo na usafiri utakuwepo hapa kuanzia saa 2.00 asubuhi. *(Makofi)*

Mwisho wa matangazo Katibu tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006
### Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali kupitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursha hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rorya kutoa rambi rambi zangu kwa wananchi, familia na ndugu ambao wameondokewa na Wabunge wao wapendwa; Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria – Mbunge wa Raha Leo; Marehemu Frank Michael Mussati – Mbunge wa Kasulu Mashariki; Marehemu Abu Towegale Kiwanga – Mbunge wa Kilombero Mashariki na Marehemu Margareth Bwana – Mbunge wa Viti Maalum. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.*(Amin)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela na Wajumbe wote wa Kamati yake kwa kuyapitia kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na hatimaye kuwasilisha Taarifa kwenye Bunge lako Tukufu. Wajumbe wa Kamati hii wamekuwa wepesi katika kuyaelewa majukumu ya Wizara, matatizo yetu, kushauri, kutuasa, kuelekeza, kukosoa na kutetea hoja za Wizara pale ilipobidi; nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningelipenda pia kumpongeza sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Frederick T. Sumaye kwa Hotuba yake ya kina na ambayo imeelezea mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kipindi cha 1995 hadi 2005. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu ambao Hotuba zao zimekwisha kujadiliwa na kupitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu ni mkutano wa mwisho wa Bunge lako hili kabla ya Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba mwaka huu, nami naomba nichukue fursa hii ili niweze kuungana na wenzangu walionitangulia kumpongeza kwa dhati kabisa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa mafanikio yaliyopatikana chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu aliyoiongoza bila kuyumba kuanzia Novemba mwaka 1995. Kwa kuongozwa na Sera sahihi za CCM, Serikali ya Awamu ya Tatu imepata mafanikio makubwa katika kufufua na kukuza uchumi, miundo mbinu na huduma za msingi za jamii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza mwenzetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa CCM, Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kwake na CCM kwa kura nyingi, kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM. Naomba vile vile nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa kuteuliwa na Kamati Kuu ya CCM kuwa Mgombea Mwenza wa Rais kwa tiketi ya CCM. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kuteuliwa kwake

kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1995 hadi 2005, Serikali ya Awamu ya Tatu imepata mafaniko makubwa katika kutekeleza majukumu ya Ulinzi wa Taifa. Kwa kuzingatia mfumo mzuri wa Bajeti endelevu, Serikali ya Awamu ya Tatu imeendelea kutoa umuhimu wa kipekee katika suala zima la kuimarisha ulinzi wa Taifa. Ni kutokana na ukweli huo Bajeti ya Ulinzi imeongezeka kwa asilimia 382.33 kati ya mwaka 1995/1996 na 2004/2005. Kutokana na ongezeko hilo la Bajeti, uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za msingi kwa askari kama vile maji, umeme, chakula, tiba, makazi na usafiri umeimarika kwa kiwango cha kuridhisha.

Vile vile kero za ucheleweshо wa mishahara, marupurupu mbalimbali, nyongeza za kila mwaka, ukosefu wa fedha za likizo, ukosefu wa sare, vitendea kazi kwa ajili ya michezo, mazoezi na utendaji kivita ndani ya vyombo vyetu vya ulinzi zimepungua kwa kiasi kikubwa. Hivi sasa ari ya utendaji kazi, uzalendo, uadilifu na nidhamu miongoni mwa wanajeshi na vijana wa JKT imepanda mara dufu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mafanikio muhimu ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuhusu ulinzi wa Taifa letu yanaweza kuanishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu katika hili imekuwa ni kundeleza juhudi za dhati za kuimarisha mtiririko wa utoaji wa huduma muhimu kwa ajili ya utendaji wenye ufanisi ndani ya Jeshi. Katika kipindi hiki utoaji wa huduma kama vile lishe, mabwalo, sare na tiba kwa wanajeshi na vijana wa JKT ulizidi kuimarika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki mfumo mpya unaoruhusu wanajeshi kujinunulia wenyewe chakula kutoka kwa Wazabuni ndani ya Makambi ulianzishwa. Kwa kupitia utaratibu huu kasoro iliyokuwepo na ambayo ilichangia kuwepo na utoaji wa huduma hewa ya vyakula kwa Jeshi iliondolewa na hivyo kuondoa matumizi mabaya ya fedha. Wakati huo huo huduma katika mabwalo vikosini ziliimarishwa.

Mheshimiwa Spika, hatua kwa hatua tatizo la ukosefu wa sare sasa limemalizika. Changamoto iliyopo sasa ni kuhakikisha kuwa tatizo hili halijirudii tena.

Mheshimiwa Spika, huduma ya tiba ni muhimu sana ndani ya Jeshi. Jeshi pasipo huduma ya tiba ni sawa na mvuvi bila mtumbwi. Hivyo katika kipindi cha miaka kumi, eneo la tiba limepewa uzito wa hali ya juu kwa maana ya kuimarishwa kwa utaratibu wa Hospitali za Kanda. Baadhi ya Hospitali hizo ziliweza kukarabatiwa au kujengwa upya na nyingine zinasubiri upatikanaji wa fedha. Kwa sasa tunazo jumla ya Hospitali Tisa (9) za Kanda.

Mheshimniwa Spika, katika eneo la UKIMWI, sote ni mashahidi kuwa hili ni janga lisilochagua. Tatizo hili limelikumba Jeshi pia na katika kipindi hiki cha miaka 10 mikakati mbalimbali iliandaliwa kwa kushirikiana na Tasisi nyingine. Kwa ujumla,

kiwango cha ufahamu wa tatizo hili ndani ya Jeshi kiliimarishwa na katika vita hivi kwa sasa sote tunazungumzia lugha moja ya ulazima wa sote kujikinga na njia bora za kuwahudumia walioathirika.

Mheshimiwa Spika**,** katika kipindi cha miaka kumi ya Awamu ya Tatu, eneo la Utendaji Kivita na Mafunzo limeimarishwa kwa kiwango kikubwa. Hii sio kwamba tumeweza kufanya kila kitu. Muhimu ni kuwa tumeweza kufanya mengi ya msingi ili kuliweka Jeshi kwenye utayari wakati wote. Mheshimiwa Spika, ni katika kipindi hiki pia tuliweza kurejesha tena mafunzo chini ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, juhudi kubwa zimefanyika ili kulipatia Jeshi la Ulinzi zana na vifaa bora ili kulijengea uwezo kizana, usafiri na usafirishaji na hivyo kuliwezesha kutekeleza majukumu yake muhimu kama vile doria mipakani, baharini na kwenye maziwa, uwezo na kutoa misaada kwa mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga au maafa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nyumba za makazi kwa wapiganaji katika Makambi ni kati ya mambo ya msingi yaliyopewa kipaumbele katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu lengo kuu likiwa ni kutanzua tatizo sugu la uhaba mkubwa wa nyumba linalolikabili Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika kipindi hiki miradi mbali mbali ya ujenzi wa nyumba za makazi na mabweni kwa ajili ya askari kapera ama imekamilishwa au inaendelea kukamilishwa katika mikoa mbalimbali nchini. Kipaumbele pia kilitolewa kwenye ujenzi wa maghala na mabwalo, mitandao ya maji safi na maji taka pamoja na umeme.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kazi kubwa nyingine iliyofanyika ni kurejesha ari na uwezo wa kuendesha miradi ya ujenzi kwa kutumia uwezo uliopo ndani ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kufanya hivyo, tumeweza kuokoa gharama kwa karibu zaidi ya asilimia 30 kwa baadhi ya miradi inayohusika. Tumejenga pia uwezo ambapo sasa wataalam wa Wizara ndio wanaosimamia kazi zinazofanywa na Makandarasi wa nje na hivyo kupunguza sana gharama za ushauri, kazi ambayo imekuwa inafanywa na watu binafsi waliokuwa wanatoza asilimia 14 ya gharama ya mradi. Michoro pia inachorwa na wataalam wa Wizara yenyewe na hivyo kuokoa sehemu kubwa ya gharama zinazoendana na kazi ya uchoraji. Haya ni mafanikio makubwa, endelevu na mageuzi katika mfumo mzima wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia miradi ya ujenzi ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa maeneo ya Jeshi ni zoezi lililopewa umuhimu wa juu katika mpango wa Serikali wa kuliimarisha Jeshi. Maeneo kadhaa ya Jeshi yakiwa ni pamoja na yale ya Makazi, Makambi, maeneo ya Mazoezi, Mafunzo na Uzalishaji mali kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa yamepimwa na yanaendelea kupatiwa Hatimiliki ili Wizara iweze kuyamiliki kisheria na hivyo kuepusha migogoro ya uvamizi.

Katika kipindi cha miaka kumi cha Serikali ya Awamu ya Tatu uzito maalum umetolewa katika kuimarisha uwezo wa Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kutekelelza wajibu wao wa kisheria wa kutoa msaada kwa Mamlaka za Kiraia katika

kukabiliana na maafa, majanga na dharura mbalimbali zinazohatarisha usalama wa nchi, wananchi na mali zao. Hii ni pamoja na kuyapatia Majeshi utaalam, zana na vifaa vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, Majeshi ya Ulinzi yamewezeshwa kuimarisha doria za kudumu katika mipaka ya nchi yetu na hasa katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Rukwa na mwambao mzima wa Ziwa Tanganyika ambako kumekuwepo na matukio ya mara kwa mara ya ujambazi na uharamia dhidi ya wavuvi na wafanyabiashara. Majeshi ya Ulinzi kwa kushirikiana kikamilifu na Polisi lilipambana na kulitokomeza kabisa tatizo la matukio ya ujambazi wa kutumia silaha ulioendeshwa na watu waliosadikiwa kuwa ni Majangili wa Kisomali katika Wilaya za Monduli na Ngorongoro Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Spika, matukio mengine ambayo Majeshi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameshirikiana na Mamlaka nyingine kwa ufanisi mkubwa katika kuokoa ni katika matukio ya ajali za majini, katika migodi, reli, mioto inayohatarisha mazingira kama vile moto wa Mlima Kilimanjaro, shughuli za uokoaji na urejeshaji wa huduma za barabara baada ya mvua za El-Nino, kujenga kivuko cha Ilagala Mkoani Kigoma kilichokuwa kero kwa wananchi kwa muda mrefu, na operesheni maalum ya kupambana na uvuvi haramu na hatari wa kutumia baruti katika mwambao wa Bahari ya Hindi (Tanga hadi Mtwara).

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tatu imeendelea kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi wa umma ili kuongeza nguvu ya Jeshi la Ulinzi na Vyombo vingine vya Dola. Mafunzo yameboreshwa na zimeundwa Kombania za Ulinzi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Zoezi la kutoa vitambulisho vya Wana mgambo lilianza katika mwaka 2003/2004 kwa kuanza na Mkoa wa Dar es Salaam na limetekelezwa sambamba na utoaji wa vyeti kwa wahitimu wa mafunzo ya mgambo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1995 hadi 2005, Serikali imeweza kupanua na kuimarisha ushirikiano wake na nchi mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Tumeshiriki pia kwa njia moja au nyingine katika mazoezi ya kulinda amani nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 Serikali ya Awamu ya Tatu iliyarejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yaliyositishwa mwaka 1994. Tangu mafunzo haya yarejeshwe jumla ya vijana 11,263 wameshakupatiwa mafunzo kama ifuatavyo:- Operesheni Mkapa vijana 2491, Operesheni Miaka 40 ya JKT vijana 2613, Operesheni Utandawazi vijana 2785 na Operesheni Jiajiri vijana 3374. Idadi hii ni kwa kipindi kinachoishia 2005 na wengi ya waliomaliza waliweza kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMA JKT) nazo zimeimarika sana katika kipindi hiki cha miaka kumi (10). Mbali na miradi iliyokuwepo, SUMA JKT imeweza kuanzisha miradi mipya na hasa ushonaji wa mavazi na utengenezaji wa madawa ya binadamu. Vile vile ili kulipa Shirika ufanisi zaidi, Bodi ya SUMA JKT nayo iliimarishwa kwa kuirekebisha

Kanuni zinazohusika ili kutoa nafasi ya kuwa na Bodi yenye uwezo wa kutenda kazi kibiashara.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kujenga zaidi uwezo wa Utafiti na uendelezaji wa Teknolojia ya Kijeshi kupitia Shirika la Nyumbu na Shirika la Mzinga ziliendelea. Kwa mfano, mojawapo ya mafanikio ni uzalishaji wa magari saba (7) ya Nyumbu uliofanyika mwaka 2004 na Waheshimiwa Wabunge kupewa nafasi ya kuyashuhudia magari hayo. Eneo hili linaendelea kupewa uzito unaostahili ikiwa ni pamoja na utafutaji wa teknolojia mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2004/2005 wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mwaka jana wakati wa kufunga mjadala kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2004/2005, Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia, walitoa maelekezo kuhusu jinsi ya kuboresha zaidi utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa heshima na taadhima naomba kutoa taarifa kuwa kwa kiwango kilichowezekana tumezingatia ushauri na maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge kulingana na uwezo wa bajeti ulivyoruhusu. Taarifa rasmi ya utekelezaji imeandaliwa na Waheshimiwa Wabunge wamepewa nakala kama sehemu ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuandaliwa rasmi kwa Taarifa ya utekelezaji, naomba nitumie fursa hii pia kuelezea kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2004/2005:-

Mheshimiwa Spika**,** katika mwaka 2004/2005, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania liliendelea kutekeleza moja ya jukumu lake la kulinda mipaka ya nchi yetu, watu wetu na mali zao. Hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, matukio kadhaa ya kuhatarisha usalama wa wananchi na mali zao yaliyosababishwa na wakimbizi kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya *Congo* katika mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa yalidhibitiwa ipasavyo na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Dola pamoja na wananchi, chini ya operesheni maalum. Baadhi ya wahalifu walipotea na wengine walikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Katika mpaka wetu na nchi ya Rwanda yamekuwepo matukio ya wakimbizi kuingia Tanzania na mifugo yao kwa kuhofia mahakama ya wananchi ya Gachacha.

Mheshimiwa Spika**,** hali ya ulinzi na usalama katika mipaka yetu ya Kaskazini, Mashariki na Kusini imeendelea kuwa shwari.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa mgambo ni sehemu ya ulinzi wa nchi yetu. Katika mwaka 2004/2005 mafunzo ya ulinzi wa mgambo yameendelea kuimarishwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Hii ni pamoja na kuboresha mafunzo kwa kusambaza rejea za masomo nchi nzima. Zoezi la kutoa vitambulisho vya wanamgambo limeendelea katika Mkoa wa Dar es Salaam. Maandalizi kwa ajili ya kufufua na kuanzisha tena

mafunzo ya uongozi wa mgambo yamekamilishwa kwa kanda tano. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuanza kutolewa katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni Jeshi linalotokana na Watanzania wenyewe kwa manufaa ya watanzania wote. Katika kipindi cha miaka kumi, Jeshi letu limeendelea kutekeleza majukumu yake mengine ya kisheria kwa uaminifu, utii, uhodari na ushupavu. Wanajeshi wetu wameshiriki kwa uwezo wao wote katika operesheni mbali mbali za kusaidia Mamlaka za kiraia wakati wa amani. Wameshiriki katika uokoaji wakati wa maafa, operesheni ya kudhibiti majangiri, wahalifu na majambazi hatari wanaotumia silaha. Wanajeshi pia wameshirikiana na Vyombo vingine vya Dola, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya ili kuwahakikishia wananchi usalama na hivyo kuwawezesha kuendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo. Hii ni pamoja na kuendesha na kuimarisha doria za kudumu katika maeneo ya mipaka ya nchi yetu na hasa katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na mwambao mzima wa Ziwa Tanganyika ambapo yamekuwepo matukio ya mara kwa mara ya uvamizi, uharamia na utekaji nyara wa wananchi wetu. Nawapongeza Wakuu wa Mikoa kwa kusimamia ulinzi wa mipaka yetu Kagera, Kigoma, Rukwa pamoja na wananchi katika maeneo hayo kwa ushirikiano wao walioutoa.

Mheshimiwa Spika, vile vile wananchi wapatao 6,000 walipatiwa huduma katika hospitali ya muda ya Jeshi iliyowekwa Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam. Katika hospitali na vituo vya Afya za Jeshi asilimia 80 ya wagonjwa wanaohudumiwa ni wananchi.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi ya kijeshi yamefanyika kama ilivyopangwa katika vikosi mbalimbali ili kuwapa wanajeshi uwezo wa kupambana na adui wakati wote ule. Mafunzo na mazoezi hayo yameendelea kuviwezesha vikundi vya fani mbalimbali jeshini kujifunza mbinu mbalimbali za kimapigano na kuwawezesha wanajeshi kuzoea kutumia zana za kivita zilizoko na zana mpya, jambo ambalo ni muhimu kwa Jeshi lolote duniani.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika Mweleko wa Sera ya CCM (mwaka 2000 hadi 2010) Sura ya 9 kifungu 111 ukurasa wa 65, Kifungu kidogo (a) ninanukuu: *"Tutajenga Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lililo dogo na la kisasa, jeshi imara katika utayari na utendaji wa kivita. Maafisa na Wapiganaji wazalendo na waadilifu; na Jeshi linaloshirikisha wananchi wenyewe katika kutekeleza majukumu ya kulinda Taifa kwa kupitia Ulinzi wa Mgambo."*

Mheshimiwa Spika, ukweli huu ulidhihirika wakati wa zoezi la kusherehekea miaka 40 ya JWTZ lililofanyika Msata – Pwani na kushuhudiwa na Amiri Jeshi Mkuu, Viongozi wa kitaifa na wageni kutoka nchi mbalimbali. Ukakamavu, umahiri, nidhamu na ujuzi wa kivita wa wanajeshi wetu ulitia fora na wageni waalikwa kutoka nje ya nchi yetu walipigwa na butwaa. Hili ndilo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, litokanalo na Watanzania wenyewe na kwa manufaa ya Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa zana na vifaa umeendelea kupewa umuhimu kwa lengo la kuliimarisha Jeshi kiutendaji. Kama alivyotuasa Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa wakati wa kilele cha sherehe za Miaka 40 ya JWTZ, na nanukuu: *"Naomba wananchi ambao wanaonea fahari, Jeshi lao watambue kuwa Jeshi la kisasa lina gharama na kimsingi mbebaji wa gharama hizo ni wananchi kupitia Serikali yao. Amani na utulivu tunaohakikishiwa na majeshi yetu ikiwemo JWTZ na Polisi ndiyo huweka mazingira mazuri ya kukua kwa uchumi wa nchi na uchumi wa watu binafsi. Hivyo inapobidi kuongeza matumizi ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama wananchi wawe wa kwanza kuelewa na kutetea."*

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Serikali imefanya juhudi za kulipatia Jeshi zana na vifaa bora kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu kulingana na uwezo wa nchi kiuchumi. Katika mwaka 2004/2005 Serikali imeweza kununua magari aina mbalimbali pamoja na maboti ya doria, ndege za usafiri na usafirishaji na kulipia malipo ya awali ya helikopta kwa ajili ya shughuli za uokoaji kwa lengo la kuimarisha Jeshi lake. Hayo yote yamewezekana kutokana na msimamo usioyumba wa Amiri Jeshi Mkuu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Ulinzi wa Taifa inasisitiza juu ya kujenga ushirikiano katika nyanja za kijeshi na ulinzi kati ya nchi yetu na nchi nyingine duniani na hasa nchi jirani ili kudumisha amani na mshikamano na hivyo kuepusha migogoro baina ya nchi na nchi. Ni kwa misingi hiyo tumeendelea na juhudi za kuimarisha ushirikiano wetu na nchi mbali mbali duniani zikiwemo nchi za Canada, China, Finland, Ghana, India, Indonesia, Italia, Ireland, Marekani, Misri, *Netherlands,* Nigeria, Norway, Sweden, Switzerland, Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, *U.A.E.* na Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano wake wa kihistoria na Jamhuri ya Watu wa China, ushirikiano uliojengwa na waasisi wa mataifa yetu Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere na Mwenyekiti Marehemu Mao Tsetung kwa viongozi wa Majeshi na Serikali kufanya ziara kati ya nchi hizo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kijeshi. Mwezi Aprili 2005 Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Watu wa China Jenerali Cao Ganchuan na ujumbe wake alifanya ziara nchini Tanzania kwa mwaliko wa Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kufuatia ziara hiyo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilitoa misaada mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili 2005 Serikali ya Tanzania na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani zilitiliana saini Mkataba wa ukamilishaji wa awamu ya Pili ya ukarabati wa Hospitali ya Jeshi Lugalo, ukarabati wa karakana kuu ya kijeshi Lugalo na upanuzi na ujenzi upya wa Hospitali ya Jeshi Bububu, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE)* kupitia Wizara ya Ulinzi imeipatia Serikali ya Tanzania vifaa mbalimbali yakiwemo magari, vifaa vya ujenzi wa barabara, maboti ya doria, vifaa vya kunyanyulia mizigo na ndege kwa ajili ya kuimarisha Jeshi letu la Ulinzi. Pia Serikali ya Tanzania na

Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu zilitiliana saini Mkataba wa Maelewano (Memorandum of Understanding) ambapo Serikali ya *UAE* itajengea Serikali ya Tanzania Chuo Kikuu cha Kijeshi cha kisasa (*Command and Staff College*) kwa ajili ya mafunzo ya Maafisa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeshiriki kikamilifu katika vikao vyote vinavyohusu Jumuiya ya Afrika mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Tanzania kama muasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kutoa mchango wake kuimarisha Jumuiya hii katika vikao vyote vinavyohusu ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi. Katika kuimarisha ushirikiano huo, Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Ulinzi kilifanyika Arusha kuanzia tarehe 22 – 23 Juni 2005 chini ya Uenyekiti wa Waziri wa Ulinzi wa Tanzania. Mambo muhimu yaliyojadiliwa na kikao hicho ni kuhusu Ubadilishanaji wa Wakufunzi, Wiki ya Michezo na Utamaduni baina ya Majeshi ya Afrika Mashariki, Ushirikiano katika masuala ya Ufundi, Ushirikiano katika Utafiti, Mawasiliano na Upashanaji wa taarifa za tahadhari dhidi ya matukio ya kigaidi. Mambo mengine yalikuwa ni tathmini ya zoezi la Kijeshi "ONGOZA NJIA" lililofanyika Tanzania Februari 2005 na uchambuzi wa kina kuhusu namana ya kukabili tatizo la wizi wa Mifugo kwa kutumia silaha baina ya wafugaji wa Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa makubaliano ya ki – ulinzi ya Jumuiya ya *SADC* na kushiriki katika vikao kwenye ngazi ya Mawaziri na Wakuu wa Majeshi na Wataalam. Aidha, Majeshi ya nchi za Jumuiya ya *SADC* yameendelea kushirikiana kwa karibu katika kutoa nafasi za mafunzo katika vyuo vya kijeshi ili kubadilishana ujuzi na kuimarisha utendaji wa majeshi hayo. Kwa mfano Majeshi ya Anga ya Nchi za *SADC* yalifanya Zoezi la Medani la Maafisa (*Tactical Exercise Without Troops*) lililojulikana kama Exercise Blue Zambezi lililofanyika Zimbabwe mwezi Aprili 2005.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2004/2005 idadi ya vijana waliochukuliwa katika Makambi kwa ajili ya mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ilipanda hadi vijana 3374 wa Operesheni Jiajiri kutoka idadi ya vijana 2491 wa Operesheni Utandawazi katika mwaka 2003/2004. Mafanikio mengine ni kuendeleza ujenzi na ukarabati wa majengo mbalimbali na miundo mbinu ya maji safi, maji taka na umeme katika Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kuimarisha mafunzo.

Mheshimiwa Spika, jukumu hilo lilifanikishwa kwa kukamilisha miradi mbalimbali ya ujenzi kama ifuatavyo: - Kambi ya Bulombora -ukarabati wa mabweni kumi (10), ujenzi wa vyoo vitatu (3), ujenzi wa bafu mbili (2), ujenzi wa bwalo la chakula 1 na ukarabati wa madarasa mawili (2).Kambi ya Mgambo - ukarabati wa mabweni matano (5), ujenzi wa vyoo vitatu (3), ujenzi wa bafu mbili (2) na ujenzi wa bwalo la chakula na jiko moja. Kambi ya Mbweni - ujenzi wa mabweni mawili (2). Nane Nane – Morogoro - ujenzi wa bwalo la vijana na viongozi. Kambi ya Maramba - ujenzi

wa madarasa mawili (2) na ukarabati wa madarasa sita (6). Kambi ya Mgulani – ujenzi wa madarasa manne (4) na karakana moja (1) na ukarabati wa madarasa mawili (2), mabweni manane (8) na jengo la ushonaj. Kambi ya Mlale - ujenzi wa karakana mbili (2) na ukarabati wa madarasa mawili. Kambi ya Itende – ukarabati wa madarasa manne (4) na ofisi moja. Kambi ya Ruvu – ukarabati wa mfumo wa maji safi na umeme. Kambi ya Oljoro – umeme *(HT* na *LT)* umefikishwa, usambazaji wa umeme umeanza, usambazaji wa maji safi Kikosini. Makao Makuu ya JKT – ujenzi wa mabweni mawili (2) pamoja na ofisi mpya na marekebisho ya mtandao wa usamabazaji umeme.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba yake ya tarehe 1 Septemba, 2004 katika kilele cha sherehe za Miaka 40 ya JWTZ, Mheshimiwa Rais aliagiza kuanzishwa kwa makambi ya JKT ya kila Wilaya hapa nchi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeanza kufanyia kazi utekelezaji wa agizo hilo kwa kuandaa rasimu ya awali. Rasimu hiyo itawasilishwa kwa Wadau wengine ikiwemo Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais. Hata hivyo, Wizara itaanza kutekeleza mradi wa awali wa majaribio kwa kuanzisha makambi ya JKT katika baadhi ya Wilaya, baada ya kukamilika kwa uchambuzi yakinifu. Katika hili ningelipenda kumpongeza Mheshimiwa Masilingi, Mheshimiwa Shah na Mheshimiwa Mwamoto kwa ushirikiano wao.

Ili kuongeza tija, kuboresha teknolojia na kuimarisha shughuli za uzalishaji SUMA JKT limeandaa mipango ya kuingia ubia na makampuni yafuatayo: Kampuni ya *Maoming Sino Tanzania Great Wall Industrial Trading Development* kwa ajili ya kufufua kiwanda cha ushonaji Ruvu JKT. Kwa Kiwanda cha Samani Chang'ombe utaratibu wa ubia kati ya SUMA JKT na kampuni ya *Moaming Foreign Trade Corporation* kutoka China unaandaliwa. Maandalizi ya kuingia ubia kati ya SUMA JKT na *CAMI Textiles Tanzania Ltd* kwa ajili ya kiwanda kipya cha nguo Mgulani JKT yamekamilika kwa kuleta mashine za kisasa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kuboresha miradi ya kilimo na ufugaji kama ifuatavyo:- kilimo cha zabibu na bustani katika Kambi ya Makutupora, kilimo cha machungwa na mahindi katika Kambi ya Mgambo, kilimo cha kakao katika Kambi ya Maramba, kilimo cha kahawa katika Kambi ya Itende na Itaka, mradi wa ufugaji ng'ombe katika Kambi ya Mafinga na mradi wa ufugaji kuku katika Kambi ya *Ruvu JKT.* Kuhusu sekta ya Viwanda SUMA JKT imeendela kuzalisha bidhaa bora katika viwanda vyake vya samani Chang'ombe, mahema Mgulani, ushonaji nguo Ruvu na madawa katika Kiwanda cha *TANZANSINO* – DSM. Katika sekta ya biashara *SUMA JKT* imechukua hatua za kupanua biashara ya bidhaa na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na kazi nzuri zinazofanywa na Idara ya Ujenzi ya SUMA JKT, Idara hiyo imepandishwa madaraja kama ifuatavyo: Ukandarasi wa Ujenzi wa majengo kutoka Daraja la Nne hadi Daraja la Kwanza; Ukandarasi wa umeme Daraja la Nne na Ukandarasi wa barabara Daraja la Nne.Kutokana na sifa na uaminifu wa SUMA JKT, Serikali imeendelea kutoa kandarasi za ujenzi kwa Shirika hili. Miradi mikubwa ambayo imetolewa kwa SUMA JKT ni pamoja na ujenzi wa nyumba 250 za watumishi wa Serikali – Dodoma, nyumba 91 za Viongozi wa Serikali – Dar es Salaam,

maghorofa 25 ya kuishi watumishi wa Serikali – Dar es Salaam na miradi mingine ya kati inayoendelea sehemu mbalimbali nchini. Thamani ya miradi hiyo inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 33.6 pindi itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT imeweza kuchangia gharama za uendeshaji Jeshi la Kujenga Taifa ili kuipunguzia mzigo Serikali wa kuendesha chombo hiki kwa kununu vifaa mbalimbali vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi milioni 406.6 ambavyo vinatumika katika kuiendeleza JKT. SUMA JKT pia imegharamia upimaji wa maeneo ya JKT kwa gharama ya shilingi 13,900,000/=. Imeweza kugharamia ushonaji wa sare za maafisa, askari na vijana wa JKT kwa gharama ya shilingi 8,000,000/=. SUMA JKT kuanzia Januari 2003 hadi Machi 2005 imeweza kuwalisha vijana wa JKT waliopo kambini kwa gharama ya shilingi 131,000,000/=. Hongera JKT, Hongera SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *TANZANSINO* kinachotengeneza dawa za binadamu kwa njia ya ushirikiano baina ya Jimbo la Shanxi la Jamhuri ya Watu wa China na JKT kimeendelea kutengeneza dawa za aina mbalimbali. Hatua zinachukuliwa za kuongeza aina na kiasi cha dawa zinazotengenezwa kwa kuzingatia mahitajio ya soko sambamba na kuboresha mitambo na mazingira ya kiwanda ili kukidhi masharti ya kimataifa kuhusiana na utengenezaji wa dawa za binadamu *(GMP).* Aidha, marekebisho yanafanyika katika mejimenti ya kiwanda hicho. Madhumuni ya hatua hiyo ni kuondoa mapungufu yaliyojitokeza na kuongeza tija na kiwango cha faida.Kama nilivyotaarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara imefanya juhudi za kuendeleza shughuli za viwanda na utafiti wa teknolojia ya kijeshi kupitia Shirika la Nyumbu na Shirika la Mzinga. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 viwanda havikuweza kuzalisha bidhaa za kijeshi kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya Jeshi kutokana na ufinyu wa bajeti, na teknolojia ya zamani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 utafiti wa gari la Nyumbu umeendelea kupewa uzito wa pekee kwa lengo la kuboresha na kuongeza ubora wake. Magari 14 ya Nyumbu yalianza kutengenezwa mwezi Novemba 2004 na yanatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2005. Matengenezo ya magari haya yamezingatia matokeo ya matumizi ya magari 7 yaliyotengenezwa mwaka 2003/2004 ambayo sasa yanaendelea kufanyiwa majaribio vikosini kwa lengo la kurekebisha kasoro zilizojitokeza na kuzifanyia masahihisho.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo Serikali imeendeleza jitihada zake za kumpata mbia ambae tutaweza kushirikiana naye katika kuendeleza kiwanda cha Shirika la Nyumbu kwa pamoja na kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Ulinzi imekamilisha mpango wa ununuzi wa mitambo ya kisasa ili kuboresha ufanisi na kuwa mitambo hiyo ilitarajiwa kufungwa kiwandani mwisho wa mwaka 2004. Baada ya kukamilisha taratibu zote Serikali ya Ubelgiji ilitoa kibali cha kusafirisha mitambo inayohusika, lakini baadae kutokana na upinzani wa ndani kwa ndani baina ya makundi

yanayopingana kisiasa ndani ya majimbo yanayounda Serikali Kuu huko Ubelgiji kibali kilifutwa kwa visingizio mbalimbali.

Tanzania kama Taifa huru na lenye heshima na wajibu wa kuwalinda wananchi wake kwa kila hali hatungelipenda Taifa lingine au mtu mwingine atuamulie ni vipi tulihudumie Jeshi letu na kututaka tuwe tegemezi kwao kwa kila kitu hata pale ambapo hatukiuki wajibu wetu wa kimataifa. Tunalo Jeshi letu la ulinzi la Wananchi wa Tanzania na halilindi nchi kwa mabua na mapanga. Kutuambia tusikarabati kiwanda chetu cha Mzinga ni sawa na kutuambia tusiwe na Jeshi au tuagize risasi kutoka kwao. Hili halikubaliki na ni haki yetu kama nchi huru. Hivyo pamoja na kucheleweshwa kwa ufungaji wa mitambo kutokana na malumbano yao ya kisiasa, katika mwaka 2005/2006 tutaendelea na jitihada zetu za kukarabati kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Buhemba Gold Mine* inayoendesha shughuli zake chini ya kivuli cha Meremeta iliendelea kufanya kazi yake kwa mafanikio. Tangu shughuli za uzalishaji zianze Februari 2003 hadi Juni 2005, jumla ya kilogram 7,185.88 zenye thamani ya Dola za Marekani 77.725 milioni zimezalishwa na kuuzwa. Wakati huo majadiliano yanaendelea kati ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Nishati na Madini kuhusu uendeshaji wa migodi ya Meremeta Geita.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mtandao wa Mawasiliano ya Pekee (*Independent Telecommunications Network*) unaohusu uboreshaji na upanuzi wa mtandao kwa lengo la kuupa uwezo wa kutoa huduma za mawasiliano ya simu na *internet* kwa ajili ya matumizi Jeshini na wateja wengine unaendelea. Mradi huu ni sehemu ya Serikali – Elektroni *(E-Government*). Fedha za kuendeleza Mradi huu zimetengwa katika Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma mwaka 2005/2006 ikiwa ndiyo Wizara itakayosimamia mtandao wa Serikali - Elektroni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa huduma muhimu kwa wanajeshi na vijana wa JKT lengo katika mwaka 2004/2005 ni kuendeleza mafanikio yaliyoanza kupatikana katika miaka ya hivi karibuni. Ni kutokana na ukweli huo katika mwaka 2004/2005 utoaji wa huduma kama vile chakula, mabwalo, sare na tiba kwa wanajeshi na vijana wa JKT ulizidi kuimarika. Uimarishaji huo pia ulihusu urekebishaji wa kasoro zilizojitokeza katika mifumo ya usimamizi wa utowaji wa huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za chakula mfumo unaoruhusu wanajeshi kujinunulia wenyewe chakula kutoka kwa wazabuni ndani ya makambi (utaratibu wa *canteen*) umeendelea kuboreshwa. Kupitia utaratibu huu wanajeshi sasa wanapata chakula chenye virutubisho na cha kiwango kinachotakiwa. Wakati huo huo huduma katika mabwalo vikosini imeendelea kuimarishwa. Maafisa na askari vikosini wameendelea kuhakikishiwa uwepo wa mahali pa uhakika pa kupumzika au malazi kwa wasiooa na vile vile kujipatia vinywaji kwa bei iliyo nafuu kila siku.

Mheshimiwa Spika, sare kwa ajili ya wanajeshi na vijana wa JKT zimeendelea kutolewa kwa vikosi vyote na kwa wakati. Kuanzia kipindi cha 2004/2005 utaratibu wa kuwa na akiba ya sare katika maghala umerejeshwa ili kuhakikisha kuwa wakati wote

hapatokei mwanajeshi kukosa sare. Jeshi la Ulinzi na JKT wameagizwa kununua mahitaji yao ya sare kutoka hapa nchini ili kukuza uchumi wetu. Uagizaji kutoka nje hufanyika tu inapobidi.

Mheshimiwa Spika, huduma za Tiba Jeshini zimeendelea kuboreshwa. Baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani, majengo ya Hospitali za Jeshi za Kanda za Mwanza na Mbeya zimekabidhiwa kwa Serikali kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanajeshi, familia zao na wananchi. Hospitali hizo zinaendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vifaa kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani. Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, zimefanya ukarabati wa Hospitali ya *TMA – Monduli.* Baadhi ya vifaa vya kisasa vya tiba na uchunguzi wa maradhi kwa ajili ya Hospitali hiyo vimefungwa. Hospitali ya Mazao – Mzinga imefanyiwa ukarabati mkubwa kwa kutumia fedha zetu wenyewe na Serikali ya Ujerumani imekubali kukamilisha ujenzi upya wa Hospitali hii ambayo baada kukamilika itakuwa na hadhi ya hospitali ya Kikanda, Morogoro.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Ujerumani kupitia Wizara yake ya Ulinzi imeonyesha nia ya kutoa msaada kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kujenga upya na kukarabati Hospitali saba za Jeshi ambazo kwa sasa zipo katika hali mbaya. Hospitali hizo ni Mirambo - Tabora, *TMA - Monduli,* Bububu - Zanzibar, Songea, *Navy – Dar es Salaam,* Mazao - Mzinga na Nyumbu – Kibaha. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali ya Ujerumani imetenga fedha kwa ajili ya kujenga upya Hospitali ya Bububu, Zanzibar na kazi hiyo imeanza. Kwa niaba ya Makamanda, wapiganaji na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda kuishukuru sana Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa kutoa msaada huo muhimu kwa ajili ya kuimarisha Afya ya wanajeshi na wananchi wetu. Ukarabati/ujenzi wa Hospitali zingine zilizotajwa utafuata baada ya kukamilika ujenzi wa hospitali ya Bububu. Kukamilika kwa hospitali hizi kutaiwezesha Tanzania kuwa na Hospitali kumi za Jeshi katika kanda zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukarabati/ujenzi wa Hospitali za Kanda, Serikali imeendelea na mpango wake wa kuhakikisha kuwa dawa za kutosha na vifaa vya kisasa kwa ajili ya Tiba na uchunguzi wa maradhi, zinapatikana. Aidha, Serikali imeandaa mpango wa kuendeleza wataalamu/mabingwa wa kada zote za fani ya Afya kwa lengo la kutoa huduma bora katika hospitali zote za Kanda, vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria imeendelea kuimarishwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, *TACAIDS,* Mashirika ya Kimataifa na Mashirika yasiyo ya kiserikali hapa nchini. Katika kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo utafiti uliofanywa unaonyesha kuwa wanajeshi walio wengi wamelielewa vema janga la UKIMWI na kinga dhidi yake. Dawa kwa ajili ya kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI (*Anti Retrovirus*) zimeanza kutolewa kwa wanajeshi walioathirika na familia zao kuanzia mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, huduma za nyumba za makazi kwa ajili ya wapiganaji wetu katika Makambi ni kati ya mambo yaliyopewa uzito maalum katika mwaka 2004/2005.

Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba za kuishi na mabweni kwa ajili ya wanajeshi unaendelea katika Mikoa ya Arusha, Mara, Iringa, Morogoro, Tanga na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya ujenzi wa majengo muhimu ambayo katika mwaka 2004/2005 utekelezaji wake kwa kiwango kikubwa ulikamilika na bado unaendelea. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa uzio kuzunguka baadhi ya Makambi na vikosi, kuweka lami barabara ndani ya Makambi, ujenzi wa Hanga la kuegesha ndege, ujenzi/uimarishaji wa maghala na ukarabati wa mabwalo. Miradi mingine inayopewa kipaumbele ni mtandao wa maji safi na maji taka pamoja na umeme. Kwa kiwango kikubwa kero ya maji imeondolewa katika vikosi vingi. Kuhusu miradi ya mitandao ya maji na umeme lengo ni kumaliza kabisa tatizo sugu la huduma hizi katika vikosi vyetu.

Mheshimiwa Spika, tofauti na miaka iliyopita, kuanzia mwaka 2004/2005 mkazo umewekwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi Jeshini kwa njia ya kujitegemea kwa kuzingatia Mwongozo wa Serikali. Kwa kutumia utaratibu huu Brigedi za Ujenzi za JWTZ na JKT zimekamilisha miradi ya ujenzi kwa gharama nafuu. Miradi iliyokamilishwa iligharimu shilingi 1,599,884,200/= ikilinganishwa na shilingi 3,638,811,200/= iliyokadiriwa na wakandarasi binafsi. Wakati huo huo Brigedi za Ujenzi za JWTZ na JKT zimeweza kufanya ukarabati mkubwa na mdogo wa majengo na nyumba katika Vikosi mbalimbali kwa kutumia fedha za bajeti zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Spika, programu iliyoanza mwaka 2003/2004 ya kupima maeneo yote ya Jeshi kwa ajili ya makazi, makambi, maeneo ya mafunzo na mazoezi ya kijeshi na yale ya uzalishaji mali kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa iliendelea kutekelezwa katika mwaka 2004/2005. Maeneo yaliyopimwa katika kipindi hiki ni katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kigoma, Lindi, Morogoro, Mtwara, Shinyanga, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya karibu yanaendelea kufanyika na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kuharakisha kusajiliwa kwa ramani za maeneo yote yaliyokwishapimwa ili kupata umiliki wa kisheria na kuepukana na migogoro ya mara kwa mara ya uvamizi wa maeneo ya Jeshi. Jeshi ni la kudumu na ni lazima liwe na maeneo ya kudumu. Upimaji wa maeneo ya Jeshi utaendelea katika kipindi cha 2005/2006 kwa kuhusisha maeneo yaliyopo katika Mikoa ya Arusha, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Tanga, Pemba na Unguja.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba zoezi la kupima maeneo yote hayo limefanywa na wataalam wetu wa Wizara kwa gharama ya shilingi 100,686,220/= ambapo gharama ingelikuwa shilingi 716,880,000/= kama kazi hii ingefanywa na Makampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika**,** ili kumaliza migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Jeshi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imefuatilia kwa karibu maswala ya fidia za

wananchi kwa mali zao zilizoko kwenye maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi kama ifuatavyo:-

(a) Zoezi la kulipa fidia za wananchi wa Tondoroni – Pwani limeendelea kutekelezwa kwa awamu;

(b) Ulipaji wa fidia za wananchi kwa eneo la JWTZ, Welezo – Zanzibar umekamilika;

(c) Tathmini ya stahili za wananchi wa eneo la Oldonyo Sambu – Arusha imekalika. Ulipaji umeanza kwa awamu ya kwanza na utakamilika kabla ya mwisho wa Julai, 2005. Hazina imetenga fedha zote zinazohusika na zimeshawasilishwa kwa Uongozi wa Mkoa wa Arusha;

(d) Tathmini ya stahili ya wananchi eneo la Msangani – Kibaha nayo imekamilika na fedha zinazohusika zimeshakabidhiwa Uongozi wa Mkoa wa Pwani kwa malipo.

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la Jeshi la Kujenga Taifa ni kutoa elimu kwa vijana wa Taifa letu. Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kuendesha, kusimamia na kuratibu elimu ya Msingi katika shule zake za msingi zilizoko katika Makambi ya Bulombora (Kigoma), Oljoro (Arusha), Makutupora (Dodoma), Mgambo, Maramba (Tanga), Chita (Morogoro), na Mlale (Ruvuma) kwa kushirikiana na Mamlaka za Wilaya. Jumla ya wanafunzi 2445 wanaendelea na masomo katika shule hizi wakiwemo watoto wa familia za maafisa, askari na watoto wa familia za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Mamlaka za Elimu katika ngazi za Wizara, Mikoa na Wilaya, JWTZ na JKT yameendelea kutoa huduma ya elimu ya Sekondari katika shule tisa (9) za Sekondari zinazomilikiwa na Jeshi. Shule za Sekondari za Jeshi zikiwemo Makongo High School, Sekondari ya Airwing, Kigamboni, Nyuki, Unyanyembe, Ruhuwiko, Kizuka, Kawawa na Jitegemee zinaendelea kuwapatia vijana wa Tanzania elimu ya Sekondari bila ubaguzi. Kwa niaba ya maafisa, wapiganaji na wananchi napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa Wizara yake kukubali kuchangia asilimia 40 ya gharama ya uendeshaji wa shule hizi.

Mheshimiwa Spika**,** tangu Serikali irejeshe mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 2001 vijana wapatao 2,843 waliojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa wamepata mafunzo ya ufundi stadi, kilimo na mifugo kwa kufuata mitaala na mitihani inayotolewa na Mamlaka ya Ufundi Stadi nchini *(VETA)* katika vyuo vya ufundi vya JKT.

Mheshimiwa Spika**,** michezo Jeshini ni sehemu ya kazi na mafunzo. Kila mwanajeshi anatakiwa ashiriki katika michezo mbalimbali kwa kuwa michezo hujenga afya, akili, nidhamu na ukakamavu. Kwa kila Fomesheni, Brigedi, Kikosi, Chuo na Kombania utaratibu umeandaliwa kwa kila mwanajeshi kushiriki katika michezo. Kutokana na utaratibu uliowekwa, timu za Jeshi zimeendelea kupata ushindi katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Kuhusu mafanikio ya timu za mpira wa

miguu za Jeshi timu ya Kipanga iliweza kushiriki katika mashindano *CAF***,** timu ya *Ruvu Stars na Transit Camp* zimeendelea kushiriki katika Ligi Kuu ya Vodacom Tanzania Bara na kuweza kuzinyanyasa timu kubwa kama timu ya Yanga katika Ligu Kuu ya Vodacom Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, michezo ya Majeshi ya Ulinzi na Usalama ilifanyika Novemba 2004 Zanzibar na kufunguliwa na Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Aman Karume. JKT na JWTZ zilipata ushindi wa Kwanza wa Jumla na wa Pili. Timu ya Ngome pia ilishiriki katika michezo ya Majeshi ya Ulinzi ya nchi za Afrika Mashariki na kuibuka mshindi wa Kwanza wa Jumla.

Mheshimiwa Spika, misingi/nguzo muhimu kwa kila mwanajeshi kutekeleza majukumu na wajibu wake kazini imewekwa bayana katika Kanuni za Majeshi ya Ulinzi. Nguzo hizo muhimu ni pamoja na uaminifu kwa nchi ambao hauna dosari, utii usio na wasiwasi wala kinyongo na uhodari na ushujaa. Utawala Bora pia unazingatia nguzo hizo muhimu pamoja na uwajibikaji. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inahimiza na kusimamia katika ngazi zote utendaji unaozingatia uaminifu, utiifu sheria na kanuni. Vitendo vya rushwa, wizi, ubadhirifu wa mali ya Umma, matumizi mabaya ya fedha za Umma, matumizi mabaya ya madaraka hayana nafasi.

Katika misingi hiyo hiyo ya kuimarisha Utawala Bora, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilianza kutekeleza mpango maalum wa Serikali wa kuimarisha huduma zake ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na Wizara na Taasisi zake zinalingana na matarajio ya wananchi na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, historia ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni historia yenye sifa, uaminifu, uhodari, ushujaa na uzalendo iliowadhirishia Watanzania na dunia tangu kuasisiwa kwa JWTZ miaka 40 iliyopita. Baada ya Muungano wetu, Amiri Jeshi Mkuu wa Kwanza Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Nyerere kwa kushirikiana na Makamu wake wa Kwanza na Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Marehemu Aman Abeid Karume, aliunda Jeshi Jipya baada ya Majeshi yaliyoundwa na wakoloni *KAR* na baadaye ikiwa Tanganyika Rifle ikiongozwa na Waingereza kuasi. Jeshi hilo Jipya liliundwa na vijana toka Jeshi la Kujenga Taifa, Vijana wa *TANU Youth League,* na Vijana wa Afro-Shirazi, tarehe 1 Septemba 1964 na kupewa jina la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Idadi yao ilikuwa 1,000.

Mheshimiwa Spika, akiwaasa wanajeshi wapya tarehe 1 Septemba 1964 Mwalimu aliwasisitizia mambo matatu ya msingi waliyopaswa kuyazingatia kama Jeshi jipya la wananchi. Mambo hayo ni Uaminifu usio na dosari wala shaka, Utii usio na wasiwasi wala kinyongo na Uhodari na ushujaa ambao ni sifa za lazima kwa mwanajeshi. Akifafanua majukumu matatu makuu baada ya kupokea kiapo cha wanajeshi 1,000 wa Jeshi jipya, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania Mwalimu alisisitiza kuwa; Jeshi Jipya la wananchi wa Tanzania ni la Watanzania Wenyewe, litatokana na Watanzania Wenyewe kwa manufaa ya Watanzania Wenyewe, Jeshi la Ulinzi siyo Jeshi la Uvamizi bali ni chombo cha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu na uhuru wetu, Jeshi la Ulinzi

litaendelea kuwa nguzo muhimu katika harakati za kupigania haki na uhuru wa Afrika na watu wake. Mwalimu aliliita Jeshi la Ukombozi. Hii ndiyo "*doctrine*" ya Jeshi la Ulinzi. Hii ndiyo siri ya mafanikio ya Jeshi la Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 Septemba 2004 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilikuwa na sababu ya kusherehekea mafanikio makubwa yaliyopatikana tangu kuasisiwa kwake. Akihutubia umati mkubwa wa wanajeshi na wananchi katika uwanja wa Taifa wakati wa kilele cha Sherehe za Miaka 40 ya JWTZ Amiri Jeshi Mkuu Rais wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliagiza yafuatayo yazingatiwe na kutekelezwa na Jeshi la Ulinzi, Rais alisema: "Jeshi letu Jipya liliundwa kwa Sura yetu, kwa malengo yetu, kwa kuzingatia Sera yetu wenyewe ya Ulinzi na Usalama na sheria yetu wenyewe ya ulinzi. Jeshi la Ulinzi ni kielelezo na mhimili wa uhuru wetu na amani yetu, mshikamano wetu na uslama wetu; ni fahari ya kila raia mwema. Hivyo basi ni lazima JWTZ ibakie daima kioo cha mambo hayo, na maadili ya Utanzania wetu. Ni lazima ibakie tegemeo kubwa la Uhuru, umoja na Muungano wa Taifa letu. Hayo ndiyo maagizo yangu kwenu leo".

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilikuwa nguzo muhimu katika harakati za kupigania utu na uhuru wa ndugu zetu wa kusini mwa Afrika dhidi ya wakoloni wakongwe na wabaguzi wa rangi. Baada ya uhuru wa Msumbiji 1975, walowezi wa *Rhodesia* kwa kushirikiana na wasaliti wa wananchi wa Msumbiji *RENAMO* walianzisha harakati za kuvuruga uhuru wa Msumbiji ili wapigania uhuru wa Zimbabwe waliokuwa Msumbiji wasiweze kuingia *Rhodesia* ambayo sasa ni Zimbabwe. Wapiganaji wetu wakiongozwa na Kamanda wao Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, walishiriki katika Operesheni Tegemea na ya mwisho Safisha ambapo mashujaa wetu 109 walipoteza maisha yao, miili ya mashujaa wanane ilirejeshwa nchini kwa mazishi na miili ya mashujaa 101 ilizikwa katika maeneo mbali mbali nchini Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 12 mabaki ya miili ya mashujaa wetu 101 yalirejeshwa nchini katika ndege yetu ya Jeshi na Kamanda wao Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi na kuzikwa upya kwa Heshima zote za kitaifa katika eneo la Naliendele Mkoani Mtwara na kuhudhuriwa na Amiri Jeshi Mkuu aliyekuwa mgeni wa heshima Agosti, 2004. Napenda kumshukuru Amiri Jeshi Mkuu aliyeagiza mabaki ya miili ya mashujaa wetu yarejeshwe na kuzikwa upya Tanzania kwa heshima za kitaifa. Namshukuru Mheshimiwa Makwetta ambaye alifuatilia kwa karibu zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, mipango ya utekelezaji ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2005/2006 ni mwendelezo wa mkakati wa kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaaa bora, kufufua vilivyopo, kuimarisha mafunzo na pia kujenga mazingira mazuri ya kazi ikiwa ni pamoja na kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika upatikanaji wa huduma za msingi kwa wanajeshi. Hivyo, kwa kutumia fedha za Bajeti ya 2005/2006, mambo muhimu yafuatakayofuatiliwa ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na ukamilishaji wa miradi inayojengwa na Wakandarasi binafsi, Jeshi la Kujenga Taifa na Idara ya Maji. Hii inajumuisha:-

- Ujenzi wa Hanga la kuegesha ndege Dar es Salaam;

- Ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa maghala kwa ajili ya shughuli mbali mbali;

- Ujenzi wa mabweni ya askari Rukwa, Kigoma, Kaboya, Tanga na Mtwara;

- Ukamilishaji wa Hospitali ya Jeshi Mtwara;

- Ukarabati wa mifumo ya Maji taka Keko, *Navy – Kigamboni,* Lugalo, Kambi ya Mirambo - Tabora na Ihumwa – Dodoma;

- Ukamilishaji wa ujenzi wa mahanga ya zana huko Shinyanga, Dodoma na Pwani;
- Ukamilishaji wa majengo ya Ofisi 36 KJ – Pwani;
- Kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Jeshi Bububu – Zanzibar;

- Kukamilisha ujenzi wa *VIP Ward* na bwalo ndani ya Kambi ya Kiabakari – Musoma;

- Ukamilishaji wa miradi ya maji Mwanza (Hospitali), Kyera na Kisarawe;

- Ukamilishaji wa nyumba za kuishi maafisa huko Mkalama – Dodoma;

- Kukamilisha miradi mbali mbali ya umeme ndani ya maeneo ya Makambi kama vile Msalato – Dodoma, Makambako – Iringa n.k.

(ii) Kuendelea kukamilisha miradi ya viporo pamoja na kujenga nyumba mpya kwa njia ya kujitegemea na hasa:-

  - Ujenzi wa nyumba za kuishi askari na mabweni Tanga;

  - Ujenzi wa nyumba za kuishi askari Makambako – Iringa;

  - Ujenzi wa nyumba za kuishi askari Lugalo – Dar es Salaam;

  - Ukamilishaji wa mtandao wa Majitaka Nguvumali- Tanga;

  - Kukamilisha ujenzi wa Bwalo la askari Monduli – Arusha;

- Ujenzi wa nyumba za kuishi askari Tanzania Zanzibar.

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi wa Mtandao wa Mawasiliano ya Kipekee;

(iv) Kuendelea na juhudi za kuimarisha shughuli za uzalishaji na utafiti wa Mzinga na Nyumbu;

(v) Kuendeleza miradi mbali mbali inayosimamiwa na Jeshi la Kujenga Taifa na kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais kuanzishwa kwa mafunzo ya JKT kiwilaya kwa kukamilisha upembuzi yakinifu;

(vi) Kuendelea na upimaji na umilikishwaji rasmi wa maeneo ya Jeshi;

(vii) Kulipia zana na vitendea kazi kwa ajili ya Jeshi na hasa vinavyohusu usafirishaji, uokoaji na doria;

(viii) Kuendelea na juhudi za kumaliza kabisa tatizo sugu na kero za miaka mingi kuhusu malipo ya mafao ya wanajeshi wastaafu na warithi kuanzia mwaka 2000 na kurudi nyuma; na

(ix) Kuendelea na jitihada za kukarabati Hospitali za Kanda za Jeshi.

Mheshimiwa Spika**,** baada ya wiki moja kuanzia leo Bunge lako Tukufu litamaliza Awamu ya Tatu. Kabla ya kumaliza Hotuba yangu napenda kuchukua nafasi hii ya mwisho kwa niaba ya Makamanda, Maafisa na Wapiganaji wote kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote waliotuwezesha kufanikisha na kutekeleza mipango ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika**,** napenda kutoa shukrani za moyoni kwa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kufufua ari mpya, uzalendo, uhodari, ushujaa, uwezo mpya, nguvu mpya, uongozi mpya wenye nidhamu, JKT mpya na mazingira mapya ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Amiri Jeshi Mkuu ataliaga Jeshi lake likiwa na uhakika wa kutimiza majukumu yake na kuhakikisha kuwa linalinda umoja wetu, mshikamano wetu, kujenga na kutetea nchi yetu, litabakia daima kioo cha Watanzania, maadili ya Kitanzania, tegemeo kubwa la uhuru, umoja na Muungano wetu. Hii ndiyo ahadi yao kwa Amiri Jeshi Mkuu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wasaidizi wakuu wa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri yetu ambao kwa mshikamano wao, umoja na uzalendo wao wamemsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu ya kikatiba kwa asilimia 95 kwa kipindi cha miaka kumi 1995 – 2005. Napenda kumshukuru Makamu wa Rais

Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri wetu Mkuu Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye na Mawaziri wenzangu. Napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa ushupavu, hekima busara na uzalendo.

Napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Mzee wangu Dr. John Samwel Malecela na Wajumbe wa Kamati yake kwa msaada wao mkubwa waliotoa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda kuwashukuru Wabunge wenzangu kwa kunitia moyo, kunishauri na kunikosoa pale nilipotetereka. Nawatakia Waheshimiwa Wabunge mafanikio mema katika Uchaguzi Mkuu 2005. Nina hakika wananchi watawarejesha tena. Napenda kuwashukuru madereva wetu ambao tuliwakabidhi maisha yetu na za familia zetu. Madereva hawa wamefanya kazi nzuri na ya kizalendo kuhusu usalama wetu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa nchi zifuatazo na Serikali zao kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika kipindi cha miaka kumi ya Awamu ya Tatu. Kwa kipekee natoa shukrani kwa nchi ya Jamhuri ya Watu wa China, kwa misaada yao isiyo na masharti na yenye heshima kwa uhuru wetu. Nchi za Falme za Kiarabu *(UAE),* Canada, India, Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Ufaransa, Ireland, Uingereza, Ubelgiji, Ghana, Misri, Italia, Sweden, Norway na Marekani. Napenda kuzishukuru nchi za Jumuiya zetu za Afrika Mashariki na Maaendeleo Kusini mwa Afrika kwa ushirikiano wao wa kiundugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nahodha bila wasaidizi wake meli itazama, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wasaidizi wangu walionisaidia kuongoza meli hii hadi kutia nanga bandarini. Napenda kumshukuru nahodha aliyenitangulia Mheshimiwa Edgar Maokola – Majogo na Katibu Mkuu wangu wa zamani Ndugu Vincent Mrisho. Natoa shukrani za pekee kwa Katibu Mkuu Ndugu Bernard S. Mchomvu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali George M Waitara, Mnadhimu Mkuu Luteni Jenerali Iddi S Gahhu, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Davis Mwamunyange, Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunitia moyo kwa kunisaidia kwa kazi hii ngumu. Wote nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa walionipa. Nawashukuru na kuwapongeza wanamichezo wote wa timu mbali mbali za Jeshi kwa heshima waliyotuletea kwa kushinda michezo mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa. Napenda kumshukuru Mpiga Chapa wa Serikali na Wafanyakazi walio chini yake kwa kuichapisha Hotuba hii na kuikamilisha kwa wakati. Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza waandishi wetu wa habari wa vyombo vyote vya habari kwa moyo wao wa uzalendo wa kutoshabikia habari potofu zinazoandikwa na waandishi wa kimataifa kuhusu Ulinzi na vyombo vyetu vya ulinzi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Rorya baada ya kunichagua kuwa Mbunge wao, na Mheshimiwa Rais kuniteua kuongoza Wizara hii, wao na Mheshimiwa Rais ndiyo wanastahili shukrani zote. Nataka niwahakikishie kwamba nitarudi niwakuwa

nao na tumetekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa asilimia 75 na tutaendelea kutekeleza kwa asilimia 100. Napenda kuwashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Rorya na Madiwani kwa ushirikian o walionipatia. Napenda kuwakumbusha kuwa tumetekeleza Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM kwa asilimia 75. Hivyo basi katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2005 – 2010) wasiwe na wasiwasi nitakuwa nao tena, na tutatekeleza Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005 – 2010 kwa asilimia 80 hadi 90 kwa kuwa tumepata uzoefu, tuna ari, tumeona mafanikio, tumeona matunda yake katika huduma za jamii na miundo mbinu. Rorya na maendeleo Daima mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania wanajiandaa kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2005, kama alivyosisitiza Amiri Jeshi Mkuu kuwa atahakikisha Uchaguzi Mkuu unafanyika kwa amani na utulivu bila vurugu. Mojawapo ya majukumu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni kuhakikisha kuwa umoja wetu, mshikamano wetu, amani na utulivu pamoja na mipaka ya nchi yetu yanalindwa kwa nguvu zote hasa wakati huu wa Uchaguzi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake iweze kutekeleza majukumu yaliyoelezwa katika Hotuba hii kwa mwaka 2005/2006, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi244,144,262,600/= fedha za hapa nchini ambazo kati yake shilingi198,428,262,600/= zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya kulipia mishahara, chakula cha wanajeshi na vijana wa JKT na matumizi mengineyo; na shilingi45,716,000,000/= kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mgawanyo ufuatao:-

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

(a) Fungu 38: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania shilingi 156,127,395,200/=.

(b) Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 36,421,689,800/=.

(c) Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 5,879,177,600/=.

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

(a) Fungu 38: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania shilingi 506,000,000/=.

(b) Fungu 39 Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 200,000,000/=.

(c) Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 45,010,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeuungwa mkono. Naomba nitambue kuwepo katika *Gallery* za Bunge, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Generali George Waitara pamoja na Makamanda Wenzake ambao nao wamehudhuria Hotuba ya Waziri. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa John S. Malecela, ningependa kwanza kabisa kutumia nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliyosomwa hivi punde na Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Mbunge wa Jimbo la Rorya na Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kutoa salaam za rambi rambi kwa wenzetu waliotutoka; Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na Mheshimiwa Margareth J. Bwana. Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi. Amen.

Vile vile ningependa kutumia nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa wao kugombea nafasi za uongozi wa ngazi za juu katika Serikali zetu mbili kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. Wote hao tunawatakia mafanikio katika Uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama yanatokana na taarifa iliyowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati tarehe 3 Juni, 2005 Jijini Dar es salaam. Kwa kuzingatia Kanuni 81 Kifungu kigodo Na. 1 na Na.4 ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004, Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa Ahadi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005 pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge uliotolewa kwa Wizara husika ndani ya Bunge hili. Aidha Kamati ilipitia mafungu ya makadirio ya Wizara ya mwaka 2005/2006:- Fungu 38 la Jeshi la Wananchi, Fungu 39 la Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti hii, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa juhudi zake ambazo zimeiwezesha Tanzania kuendelea kuwa nchi ya amani na utulivu licha ya kuzungukwa na nchi zenye migogoro ya kisiasa na vita. Hali hii ya Usalama imewezesha nchi yetu kuwavutia wawekezaji wengi na kusababisha mafanikio ya kiuchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Katibu Mkuu Ndugu Bernard Mchomvu na Wataalam wengine wa Wizara hii kwa kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Kamati taarifa iliyoonyesha jinsi Wizara ilivyotekeleza majukumu yake kwa ufasaha. Kwa kuwa taarifa hii ni ya mwisho kutolewa kwa uhai wa Kamati hii, napenda kutumia nafasi hii pia kuwapongeza Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi rafiki yangu Generali George Waitara, Makamanda na Wapiganaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda nchi yetu pamoja na kutoa huduma mbali mbali kwa wananchi wa Tanzania. Jeshi letu kweli ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Linalinda na kuwahudumia Watanzania kama jina lake linavyoonyesha, JW (Jeshi la Wananchi).(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru Wajumbe wa Kamati kwa jinsi walivyotoa ushirikiano katika kipindi chote cha uhai wa Kamati hii. Utendaji wa Kamati hii ulilingana sana na utendaji wa Sekta hii kwa kutunza muda na kufanya kazi kwa muda mrefu na kwa uvumilivu wa hali ya juu. Kwa kifupi, Wajumbe wa Kamati hii wanastahili pongezi zetu sote. Wajumbe hawa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa John S. Malecela – Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella – Mjumbe, Mheshimiwa Anne K. Malecela – Mjumbe, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta – Mjumbe, Mheshimiwa Thomas S. Nyimbo – Mjumbe, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah – Mjumbe, Mheshimiwa Ereneus N. Ngwatura – Mjumbe, Mheshimiwa *Cornel* Feteh Saad Mgeni – Mjumbe, Mheshimiwa *Major* Jesse J. Makundi – Mjumbe, Mheshimiwa Frank G. Maghoba – Mjumbe, Mheshimiwa Benito W. Malangalila – Mjumbe, Mheshimiwa Haji J. Shereweji – Mjumbe na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali – Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Kamati inamshukuru sana kwa jinsi alivyosaidia kufanikisha malengo yake. Shukrani pia ziwaendee Katibu wa Bunge Ndugu Damian S. L. Foka na Watumishi wa Sekretarieti ya Kamati Ndugu Matthew Kitundu na Elise Mbise kwa kazi yao nzuri ya kuihudumia Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa 2004/2005; Waziri wa Ulinzi aliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa ahadi

zilizotolewa hapa Bungeni kwa mwaka 2004/2005. Kamati ilizipokea taarifa hizo na kuzichambua kwa makini. *(Makofi)*

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imetekeleza kwa ufanisi mkubwa ahadi zilizotolewa hapa Bungeni pamoja na kuzingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbele ya Bunge lako Tukufu. Katika kujiridhisha na taarifa za utekelezaji wa Wizara, Kamati ilitembelea maeneo mbali mbali ya nchi kujionea kazi zinazotekelezwa na Wizara hii. Kamati imeridhika sana na utekelezaji wa mipango mbali mbali iliyoahidiwa na Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006. Katika Mwaka wa Fedha 2005/2006, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inakusudia kutekeleza mambo yafuatayo ili kutimiza majukumu yake. Moja, kuajiri Watumishi wenye ujuzi kwa kulingana na mahitaji ya Wizara. Pili, kuimarisha uwezo wa kupambana na adui wakati wote kwa kutoa mafunzo ya kijeshi katika taaluma mbali mbali ili Jeshi lisitoe damu nyingi wakati wa vita, lazima litoe jasho jingi wakati wa amani kama huu. Kutengeneza na kukarabati vifaa na miundombinu iliyopo, kununua vifaa vipya na vya kisasa, kutunza vizuri zana na vifaa vilivyopo. Tatu, kuboresha tekinolojia ya kijeshi kwa kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji mali katika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu. Nne, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwajengea wanajeshi nyumba za kuishi ili waishi makambini, kuboresha utoaji wa huduma za matibabu, shule na kumbi za burudani.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imepitia na kuridhika na michanganuo mbali mbali iliyowasilishwa na Wizara ikionyesha jinsi malengo hayo yatakavyotekelezwa na vipaumbele vilivyotolewa kwa kila eneo kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati: Kamati pia ilitembelea mipaka yote ya nchi yetu. Hivi karibuni ilipata fursa ya kutembelea mpaka wa nchi yetu na Msumbiji. Kimsingi hakuna tatizo la mpaka kati ya nchio hizi mbili. Hata hivyo Kamati inashauri kwamba ziwekwe alama za kudumu *beacons* kwenye mpaka huo kwa sababu Mto Ruvuma ambao unachukuliwa kama mpaka wa nchi hizi mbili, hivi sasa una uwezo wa kuhama hama kama inavyotokea kwa Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi.

Pia alama za mipaka zilizowekwa upande wa Msumbiji ni za miti ambayo inaweza kukatwa au kukauka. Kwa hiyo Kamati inashuri ziwekwe alama za kudumu.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti vitendo vya ujambazi na uvamizi vinavyofanywa katika mwambao wa ndani ya Ziwa Tanganyika, Kamati inashauri kwamba Serikali inunue *boat* ziendazo kasi na zenye vifaa vya mawasiliano na zana za kisasa ili kudhibiti uvamizi unaoweza kufanywa na maharamia toka nchi jirani. Aidha *boat* nyingine

zinazotumiwa na vyombo vya Dola, zinunuliwe *engine* kulingana na mahitaji. Kumbuka malipo ya Uhuru wetu ni kujitahadhari daima.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipotembelea maeneo mbali mbali hasa maeneo ya mipakani, ilibaini kwamba matatizo mengi ya kiusalama hasa katika Mikoa ya mipakani yanasababishwa na Wakimbizi na Wahamiaji haramu. Kamati inashauri kuwa Serikali iwe inafanya *operation* za mara kwa mara kwa lengo la kuwaondoa Wahamiaji haramu waliozagaa maeneo mbali mbali ya mipakani. Ni vizuri ieleweke kuwa nchi ya Tanzania ni nchi ya Watanzania. Watanzania hawana Ubia na raia wa nchi nyingine yoyote kuhusu miliki ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati inashauri kwamba Vituo vyote vya Ulinzi vilivyoko mipakani, vipatiwe vyombo vya mawasiliano vya kisasa ili kukabiliana na uhalifu unaoendeshwa na watu binafsi kwa kutumia vyombo vya mawasiliano vilivyo bora zaidi kuliko vya Wanajeshi wetu. Aidha wananchi waelimishwe na kushirikishwa kwa ukamilifu katika kuwatambua wageni na watu wahalifu ili vitendo vyao viweze kudhibitiwa kabla hawajafanya maafa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la uhasama miongoni mwa Wakimbizi linaendelea kushamiri ndani ya Makambi na Makazi ya Wakimbizi yaliyoko nchini. Hali hii ya kuendeleza chuki na kulipa kisasi itaendelea kuleta mifarakano ndani ya nchi zao hata pale juhudi za kuleta amani zitakapofanywa. Kamati inashauri kuwa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi, ipeleke wataalam wa Elimu ya Siasa *(Political Commissars)* katika Makambi na Makazi ya Wakimbizi ili kuwaelimisha Wakimbizi umuhimu wa amani na kuvumiliana.

Njia hii itasaidia kurekebisha tabia za chuki na uhasama wa kikabila na kuleta maelewano wakati watakaporejea nchini kwao.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilitembelea baadhi ya miradi inayoendeshwa na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Shirika lake la Uzalishaji mali SUMA – JKT. Kwa mfano Kamati ilitembelea mradi wa nyumba 91 za Watumishi wa Serikali zinazojengwa na SUMA – JKT kama Mkandarasi. Kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Kikosi hiki, Bodi ya Wakandarasi Nchini ilipandisha Daraja la Kikosi hiki cha SUMA – JKT kutoka Daraja la Tatu hadi Daraja la Kwanza. Kamati inalipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafanikio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na mradi wa ujenzi wa nyumba, Kamati pia ilitembelea Kiwanda cha kutengeneza Samani, Ujenzi wa Kiwanda Kipya cha Nguo na Kiwanda cha Kutengeneza Dawa. Kamati ilielezwa kwamba Viwanda vya nguo na Dawa vinao uwezo wa kuzalisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu.

Kutokana na uwezo wa Viwanda hivi, Kamati inashauri kwamba vyombo vyote vya Dola kwa maana ya Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Kujenga Taifa, Polisi na Magereza, wawe wananunua Sare zao kutoka Kiwanda cha SUMA – JKT. Hali kadhalika vyombo hivi viwe vinanunua Dawa moja kwa moja kutoka kwenye kiwanda cha SUMA – JKT, badala ya kununua Dawa hizo kupitia Taasisi nyingine na kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kurudisha utaratibu wa kuchukua vijana wa kujitolea ili kujiunga na Mafunzo ya JKT. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali itoe mwongozo utakaoelekeza vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama viwe vinaajiri Watumishi yaani Askari kutokana na JKT - Watumishi wenye nidhamu na Wazalendo.

Katika kutekeleza hili, vyombo vyote vya ulinzi na usalama viwe vinawasiliana na JKT ili kuelezea mahitaji yao mapema kwa maana ya sifa ya watu wanaohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana wanaomaliza mafunzo ya JKT kwa njia ya kujitolea, Kamati inashauri kwamba Serikali iweke utaratibu wa kuwapatia nyenzo kwa kulingana na mafunzo waliyopata ili warudipo makwao wawe na uwezo wa kujitegemea. Hatua hii itasaidia sana kupunguza tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo agizo la Mheshimiwa Rais la kulitaka Jeshi la Kujenga Taifa lipeleke shughuli zake wilayani. Kamati ilielezwa kwamba agizo hili bado linafanyiwa kazi na mamlaka husika. Kamati inashauri kwamba, mpango huu uharakishwe ili kupunguza idadi ya vijana wanaokimbilia mijini baada ya kumaliza shule. Katika kutekeleza agizo hili, Kamati inashauri kwamba Serikali iandae maeneo mapema katika kila Wilaya kwa shughuli mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kurudisha nyumbani mabaki ya miili ya Askari wetu waliofia Msumbiji wakati wa vita vya ukombozi na kuwazika tena kwa heshima za Kitaifa katika eneo la Naliendele mkoani Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia ya nchi yetu haiwezi kukamilika bila kuwakumbuka mashujaa mbalimbali waliopigania uhuru wa nchi hii na nchi nyingine za Afrika. Kamati inapongeza Wizara kwa kupokea ushauri wa Kamati wa kujenga mnara wa mashujaa wote waliopigania uhuru wa nchi hii na nchi nyingine za Bara la Afrika hapa Dodoma. Zaidi ya ekari 1,000 zimetengwa katika eneo la Chimwaga kwa madhumuni hayo na tayari Wizara imelipia gharama za kupima viwanja katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kuipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya katika kuboresha maisha ya Wanajeshi wetu na vyombo vingine vya dola kwa muda wa miaka mitano ya uhai wa Kamati hii. Pamoja na kwamba matatizo yote hayawezi kumalizwa au kumalizika kwa mara moja, lakini maeneo mengi yaliyokuwa kero yamepatiwa ufumbuzi na Kamati imeridhika sana na kazi inayofanywa na Wizara hii. Kamati inashauri kwamba, mafanikio yaliyopatikana yaendelezwe kwa lengo la kuondoa kabisa matatizo ya Askari hasa kuhusu nyumba za kuishi na usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote, kwa niaba ya Kamati na mimi mwenyewe, napenda kusema wazi kuwa kazi ambayo mlitutuma sisi wenzenu tumejitahidi kuifanya kwa nguvu zetu zote na tunadhani tumefanya vizuri. Kwa heshima, naunga mkono hoja ya Waziri. *God willing, we shall meet again, Inshallah. (Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa wanne watakaochangia mwanzoni, ili waweze kujiandaa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud. Hilo moja.

La pili, tumekwishagawa nakala za Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani, ameniletea masahihisho muhimu ambayo atayafanya wakati anaisoma. Kwa wale walio na nakala hizi ni kwamba, kifungu cha saba anakifuta, kiko ukurasa wa tatu na kifungu cha nane ukurasa wa nne anakifuta. Halafu kuna kifungu cha tatu kidogo, ukurasa wa sita vile vile anakifuta. Sababu ya kufuta vifungu hivyo ni nzuri sana, anasema kwamba huu si muda wa hotuba za malumbano au maneno ya kukashfiana, ndiyo maana anavifuta vifungu hivyo. *(Makofi)*

Sasa namualika Mheshimiwa Ali Said Salim awasilishe Maoni ya Kambi ya Upinzani kama yalivyorekebishwa. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM – (K.n.y. MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli si msemaji wa Wizara hii, lakini kwa bahati mbaya mwenye Wizara hii amesafiri leo, kesho ana mkutano wa kura za maoni. Kwa hiyo, nawasilisha kwa niaba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni na kwa niaba ya Mheshimiwa Makundi, nachukua fursa hii kwa ruhusa yako nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(c).

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba yangu na Wananchi wapendwa wa Jimbo la Vunjo, napenda niungane na Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa wafiwa wote waliofiwa na Waheshimiwa Wabunge wao wapatao (10) kumi waliotutangulia mbele ya haki tangu tuanze Bunge hili Tukufu, Novemba 2000 hadi leo hii 2005. Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu hawa. Amin.

Mheshimiwa Spika, pia kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, natoa salaam za rambirambi kwa waliofiwa na Afisa au Askari JWTZ na JKT katika kipindi hiki 2000 hadi 2005. Hawa ni mashujaa wa Taifa letu, wamekufa kishujaa na Mwenyezi Mungu azilaze roho za mashujaa hawa mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, kipekee Kambi ya Upinzani inawakumbuka Majenerali wa JWTZ na JKT waliotutangulia mbele ya haki tangu mwaka 2000 hadi 2005. Wanakumbukwa hawa kipekee kwa mchango wao mkubwa kwa kuongoza majeshi yetu kishujaa na kwa ufanisi mkubwa. Ni vigumu sana kwa Taifa kupata Jenerali mbadala na mwenye sifa na uzoefu kama yule aliyetutoka.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote, Mashujaa hawa waenziwe na kwa gharama yoyote ile. Ili kuwaenzi vilivyo makambi

yote ya JWTZ yaitwe kwa majina yao. Hii ni pamoja na Majenerali waliostaafu na wako hai. Kwa mfano, 34 KJ - *General Musuguri Camp,* 511 KJ - *General Kiaro Camp*, 675 KJ - General *Twalipo Camp* (Hii tayari iko Mgulani), 491 KJ - *General Marwa Camp,* 701 KJ - *Major General Walden Camp,* 705 KJ - *Lt. General Kombe Camp.*

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na kujenga minara mbalimbali yenye sanamu ya Jenerali huyo akivalia kijeshi. Mnara wa sanamu wa ukumbusho ujengwe pale mahali alipouliwa kwa ajali Luteni Jenerali Amrani Kombe. Huyu ndiye Jenerali wa kwanza wa cheo cha juu kabisa aliyetutangulia mbele ya haki na baada ya ukombozi wa Bara lote la Afrika na uvamizi wa Nduli Iddi Amini wa Uganda.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inampongeza sana Amiri Jeshi Mkuu; Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuongoza majeshi yake vyema kwa kipindi chote cha miaka kumi 1995-2005 bila majeshi haya kumnyooshea kidole Amiri Jeshi Mkuu wao na anajua maana ya Jeshi kumnyoshea kidole. Majeshi yetu yana nidhamu na uvumilivu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Profesa Philemon Sarungi (Mbunge), kwa umahiri wake mkubwa na kwa jinsi alivyoongoza Wizara hii na kwa mafanikio makubwa sana tangu 2000 hadi 2005 kama hotuba yake inavyojieleza. Pongezi pia zimwendee *CDF* na Wataalamu wake. Bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara na Wafanyakazi wote. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa nadhiri kwa Taifa hili la Tanzania kuwa; kama itaingia madarakani kwa ridhaa ya Watanzania ambao sasa wameshaelimika ya kutosha kuhusu Rais anayefaa, Taifa litaneemeka kama ifuatavyo: -

Amiri Jeshi Mkuu huyo ambaye atachaguliwa kwa tiketi ya itikadi yake toka Upinzani atakuwa ni Amiri Jeshi Mkuu wa itikadi zote, Madhehebu yote, viumbe vyote vilivyo hai na visivyo hai. Wote atawatendea haki. Wenye itikadi zao wataongoza itikadi zao na wenye madhehebu yao wataongoza madhehebu yao kwa mujibu wa sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Amiri Jeshi Mkuu huyo toka Upinzani hatajineemesha mwenyewe kwa dhahabu, *Tanzanite* au madini ya aina yoyote ya nchi hii. Madini hayo ni Mwenyezi Mungu aliwapa Watanzania kama alivyowapa Waarabu mafuta. Neema hii ya madini itanufaisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Mtanzania yeyote mwenye macho safi anafurahia sana mwanga wa mchana. Ndiyo maana usiku ukiingia anakata tamaa ya kufanya kazi, hivyo anaamua kulala. Jeshi letu linafanya kazi masaa 24, hakuna kulala!

Mheshimiwa Spika, wakati wa amani Amiri Jeshi Mkuu ataendeleza kwa kasi kubwa sana ujenzi wa nyumba za waliooa na pia makapera walioko makambini. Wote watapata nyumba zenye hadhi stahili. Hali kadhalika maghala, mahanga, mavazi ya

kijeshi na mambo yote ya kiutawala na ya kiutendaji kivita yataboreshwa kwa kiwango cha hali ya juu sana. Madini yote tunayo, gesi tunayo, makaa ya mawe tunayo, watalii wanamiminika nchini, kilimo tunacho uvuvi tunao, kodi wanalipa kwa wale wote wanastahili kulipa kodi. Udhibiti utakuwa wa hali ya juu na kila Mtanzania atajitahidi awe mzalendo na kuzoea uzalendo kiasi kwamba chochote kinachopatikana kinatosha kuinua maisha ya Watanzania na majeshi yake yote. Uchumi bora majeshi bora.

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi wa JWTZ wanafanya kazi masaa 24 bila kupata nafasi hata ya kutengeneza tuta moja la mchicha. Amiri Jeshi Mkuu ajae, toka Kambi ya Upinzani atahakikisha mishahara na marupurupu yao hayakatwi kodi hata kidogo. Kodi yao iko ndani ya masaa 24 ya utumishi wao. Mishahara na marupuru yataboreshwa yaendane na wakati tulionao.

Mheshimiwa Spika, vyeo vya Maafisa vitapandishwa kwa utaratibu uliowekwa. Kozi, mitihani ya nadharia, mitihani ya vitendo na muda aliokaa na cheo alicho nacho. Kama yuko kwenye kikosi ambacho muundo hauruhusu kupandishwa cheo zaidi, ni lazima apewe uhamisho, cheo na madaraka. Mshauri wa Mgambo wa Wilaya anapaswa kuwa Meja au Luteni Kanali.

Mheshimiwa Spika, ukiona Jeshi la nchi yoyote limetulia ni dhahiri kwamba mianya yote ya utovu wa nidhamu imezibwa. Kila Afisa na Askari anajua ni nani *senior*, kwa nini na ampigie saluti nani. Maana ya saluti ni kwamba, anayepiga saluti ana cheo kidogo kuliko yule anayepigiwa saluti na yuko tayari kufuata/kupokea amri zake. (Nashangaa, nawaona Askari Polisi wakilinda hapa Bungeni tangu 2000 hadi 2005; sijaona hata mmoja amepandishwa cheo chochote na je, ni miaka mingapi kabla sijafika ametumikia Jeshi la Polisi na cheo alicho nacho?)

Mheshimiwa Spika, majeshi ya *Infantry, Air Force, Air Defense* na *Navy* chini ya Serikali mpya ya Upinzani yatapata stahili yao kulingana na mahitaji yao na malengo yao. Wakati wa amani ni mazoezi ya kivita kwa JWTZ na ufundi, kilimo na ukandarasi (uzalishaji mali) kwa JKT. Idara za shughuli hizo zitaimarishwa kwa kasi kubwa kwa kuwapeleka makamanda katika mafunzo zaidi ndani na nje ya nchi.

Vijana wanaochukuliwa na kuhitimu mafunzo ya JKT watapatiwa mkopo na nyenzo na kuratibiwa shughuli zao badala ya kuachwa solemba mitaani na matokeo yake kugeuka kuwa majambazi na kutumia silaha kwa kutumia mafunzo waliyopewa wakiwa jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inasema kuwa; si kwamba Rais Amiri Jeshi Mkuu toka Upinzani ataanza vitu vipya kabisa;, la hasha! Ataendeleza vilivyoanzishwa kwa kasi zaidi na kwa ufanisi zaidi na kuwa mbunifu kwa yale ambayo hayakuwepo. Ataondoa na kurekebisha maazimio yaliyopitwa na wakati kama vile lilivyoondoka Azimio la Arusha. Pia, vitabu vya Sheria: *Volume One, Volume Two* na *Volume Three* vitafanyiwa marekebisho ili viendane na wakati tulionao.

Mheshimiwa Spika, waliostaafu miaka ya nyuma na bado wako hai watapata pensheni sawa baada ya *standardization* sawa na waliostaafu mwaka jana au miaka ijayo. Hakuna mwenye tumbo dogo aliyestaafu miaka ya nyuma na mwenye tumbo kubwa aliyestaafu mwaka jana au miaka ijayo. Wote wamestaafu kwa cheo kilichotukuka na miaka iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote waliostaafu kwa heshima watatungiwa utaratibu, kanuni na sheria wapandishwe vyeo kulingana na stahili ya vyeo vyao walivyostaafu navyo. Utaratibu huu upo India na mataifa mengine. Ndiyo maana wakati wa vita au maafa wanaitwa kazini. Meja Jenerali Mirisho Sarakikya alipopandishwa cheo na kuwa Jenerali na sasa amepumzika uraiani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa wito kwa wote waliostaafu wagombee nafasi za uongozi katika ngazi zote hasa Ubunge; wafuate mfano ulio hai, kama alivyofanya Mheshimiwa Meja Jesse Jeremia Makundi ambaye sasa ni Mbunge mahiri wa Jimbo la Vunjo kwa tiketi ya *TLP*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini fika kuwa sasa majeshi yetu na Wizara ya Ulinzi na JKT kwa ujumla wameshajua kuwa alama ya vema (“) wataweka kwa mgombea Urais yupi tarehe 30 Oktoba, 2005.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu hongera na pongezi sana kwako kwa kuongoza vyema Bunge lako Tukufu tangu 2000 hadi 2005. Tunakutakia afya njema na maisha marefu. Pongezi za dhati zimwendee pia Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kuliongoza vyema.Bunge hili.

Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Wilfred Lwakatare Kiongozi wetu Mkuu ndani ya Kambi kwa kutuongoza vyema na kwa umahiri licha ya sisi wazungumzaji wakuu wa Upinzani kwa kila Wizara kutoka katika vyama tofauti vya siasa. Kwa mfano huu, kumbe Serikali ya Umoja wa Kitaifa inawezekana. *(Makofi)*

Napenda niwapongeze kwa dhati kabisa Wana wa Vunjo kwa ushirikiano tuliopeana kwa kipindi chote cha miaka mitano. Ninaamini kabisa kuwa mchango wangu Bungeni na kwa Wananchi wa Vunjo mmejua fika kuwa mimi ni kimbilio lenu usiku na mchana. Wale waliogombea Ubunge na mimi mwaka 2000 walipotelea wapi na ahadi zao hewa? Mbona wamenisusia Jimbo zima kama vile siyo Jimbo lao? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, angalizo letu ni kwamba, bajeti itumiwe vizuri kwa malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Bajeti ya Wizara yetu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mwanzo

kabisa niwapongeze wote waliohusika katika kuandaa hotuba hiyo. Waziri, Katibu na Makuu wa Majeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi vitu vingi husikika kila mara. Hivi sasa wengi tumepokea sifa za uchumi wa nchi hii kukua vizuri pamoja na sifa mbalimbali. Leo nilipenda kupitia *Hansard* ni-rejiste kwa kiwango gani Watanzania waelewe kazi kubwa ya kujenga uchumi inayotekelezwa na Jeshi letu la Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni kwamba, mahali popote ambapo ulinzi na usalama umedhibitiwa vizuri, mara nyingi hatutambui na mara nyingine huwa tunasahau tukadhani usalama huo, ulinzi huo, umoja wetu huo, maendeleo hayo ni jambo linalotokana na Mungu mwenyewe. Lakini ni vizuri Watanzania tukatambua kwamba, nchi ambazo majeshi ya nchi hizo yameshindwa kutekeleza majukumu waliyopewa sawa sawa na mara nyingine yakasaidia kuongeza vurugu na uvunjaji wa amani katika nchi zao, hakuna barabara inayojengwa, hakuna hospitali inayojengwa, hakuna shughuli nyingine ya kumuendeleza Mwananchi wa nchi hiyo bila kuhangaika na ulinzi na usalama wao Wananchi, jamii na mali zao.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nilipenda nafasi ya kwanza kabisa nimpongeze sana Amiri Jeshi Mkuu; Rais Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Jeshi lake la Ulinzi na Usalama ameweza kuimarisha na kusimika uchumi wa nchi hii ambao tutaendelea kuuenzi na kuufanyia kazi kwa miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la nchi ndiyo chombo kikuu cha utekelezaji wa kazi kubwa ya Serikali. Serikali yoyote kazi namba moja ni ulinzi na usalama wa maisha na mali za Wananchi wake. Serikali ikiishashindwa hilo, haina sababu ya kuwepo kwa kazi nyinginezo, maana kazi nyingine zote huwa haziwezekani. Serikali ya Tanzania katika miaka 10 ya uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa, imetuhakikishia uwezo wake na upeo wake mkubwa katika kuiendeleza jamii ya Watanzania. Tumeshuhudia Jeshi la Ulinzi likitumika kuwaendeleza Watanzania katika shughuli mbalimbali na pekee, ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina uhakika, si tu wanajenga hizo nyumba, lakini pia kwa wao kujenga nyumba hizo kiuhandisi zinakamilika vizuri zaidi. Kwa vyovyote vile, angejenga kwa mkataba mtu mwingine yeyote angezingatia faida iliyomfanya aanzishe kampuni yake la ujenzi kuliko umadhubuti wa nyumba zenyewe.

Lakini Jeshi letu licha ya kutumia gharama ndogo na kuponya fedha nyingi ziweze kuzalisha nyumba nyingi, pia limezingatia umadhubuti wa kiuhandisi kwa majengo wanayojenga. Ni lazima niwapongeze na kuwaenzi sana tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mheshimiwa Philemon Sarungi; Mbunge wa Rolya. Nina uhakika Wanarolya wanafuatilia shughuli za ulinzi na usalama wa nchi hii na nina uhakika wanafahamu Mbunge wao anashughulika na jamii ya Watanzania kwa ulinzi wao. Wao

kule sehemu za Musoma ni watu wa kupigana pigana ngumi na nini, lakini nina uhakika wamemuona bwana huyu akishughulikia ulinzi na akihakiki mwenendo wa nchi yetu kwa ajili ya mshikamano wetu. Najua watamrudisha tena. Si kwa faida yao, ila kwa faida ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli wako watu ambao wana tamaa tamaa ya vyeo, huamini kila analofanya mwenzako na wewe ungefanya maana unatamani cheo. Zamani nilikuwa na mashaka na Profesa Sarungi, huyu *newly Surgeon* itakuwaje! Nilisahau kuwa anatoka Musoma. Lakini alipoanza kazi nikakuta yeye ni Askari wa mstari wa mbele anafanya kazi ya kuheshimika. Pongezi nyingi sana. Mheshimiwa Sarungi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa pekee nimpongeza Katibu Mkuu, lakini pia nimpongeze Mkuu wa Majeshi; Jenerali George Waitara. Nimekutana naye mara nyingi kwa mazungumzo mbalimbali, ni kijana, ana nguvu, ana ari, ana upeo na uwezo. Ninampongeza sana na kupitia yeye nimewapongeza Viongozi wote wa Jeshi katika kada zao mbalimbali. Naomba niende haraka mahali pamoja ambapo nadhani ni vizuri nirudie kwa faida ya *Hansard*. Sasa hivi kuna mtu sijui kwa makusudi au kwa bahati mbaya anajaribu kuifanya Serikali ione siyo lazima kuajiri vijana katika majeshi yetu kutoka *National Service.* Jambo hili nasema ni jambo la ajabu na kwa nini wengine hawaoni, nashindwa kuelewa! Jeshi lolote bora huanza siku mtu anapoajiriwa. Kwa kiasi gani amefanyiwa *vetting,* amefanyiwa uchambuzi wa kumfahamu vizuri ni nani huyu na ndiyo hatimaye unapata Mwanajeshi na kada wa Jeshi endelevu na Mzalendo ambaye anaweza kupigana hata kufa kwa ajili ya nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wengine sana wanajaribu kuipotosha Serikali ichukue vijana kutoka sijui kwa *DC!* Kuna mtu anadanganya kwamba eti vijana wa Jeshi wanaomba vijijini, halafu wanakwenda sijui ofisi ya *DC*, sijui wanachambuliwa na kadhalika. Sasa, mimi ninayeishi kijijini na kwa *DC* na wapi wanawadanganya! Mahali bayana nchi, Serikali au Jeshi lolote lile linaweza kupata au kufanya *recruitment* na likawa na uhakika huyu ninayemuajiri ni nani, anatoka wapi, kwa ajili ya nini, ana uwezo gani na kadhalika ni katika Jeshi la Kujenga Taifa. Ndiyo mahali pekee pa Kiserikali. Kuendelea kuchukua vijana kutoka kwa ma-*DC* na wapi, ni sawa sawa na kupita humo pembeni pembeni kusikojulikana na kuokoteza watu ambao mara nyingine huwa wala siyo Watanzania. Wote ni mashahidi, tumekwishakuwa na Wanajeshi ambao walikwenda mpaka ngazi za juu kabisa za Jeshi letu, lakini baadaye ilidhihirika kwamba siyo Watanzania, ni *minority immigrants.* Ni lazima tuhakikishe hili linatekelezeka. Pamoja na kuishauri Serikali, najua kwamba Serikali yetu ni sikivu, ni Serikali ya chama kilichokomaa, endelevu, chama chenye uwezo mkubwa wa kuwaongoza Watanzania. Jambo dogo kama hili nina uhakika linaeleweka na litazingatiwa kuanzia sasa na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu tumeomba kama Kamati, vijana wa JKT wapewe zana za kujiendeleza wanaporudi majumbani kwao. Nataka niongeze sehemu ndogo tu. Nilidhani kwa kuanzia ili iwezekane mapema, waanze kupewa wale waliofanikiwa na kuonyesha umadhubuti na umashuhuri katika mafunzo yao hatua kwa

hatua baadaye kuweza kuwapatia karibu wote wanaofaulu na kuondoka kurudi vijijini. Hatari yake ni kwamba, tukikaa na watu wengi ambao hawana ajira vijijini na ambao wana mafunzo mazuri ya kijeshi, hakuna jambo ambalo ni zuri tu, kila jambo lina upande mweupe na mweusi. Hawa vijana wakikosa kazi, wakianza kuingia kwenye matendo batili na maovu, namna ya kuwadhibiti huwa ni tabu sana kuliko wale ambao hawakupitia mafunzo ya kijeshi. Kwa hiyo, ni vizuri tukachagua nani waingie *National Service,* baadaye tukachagua nani wenye elimu, sifa na mahitaji kama majeshi yanavyohitaji na waliobaki, nani wana sifa za juu tuanze kuwapa zana. Wanaweza kupewa zana wawili/watatu, lakini watakapotengeneza vikundi vya uzalishaji watakuwa zaidi ya watatu au wanne. Haya yote yatatusaidia kufikisha malengo, kulinda amani na utulivu wa Tanzania ambaye ndiyo mama wa maendeleo yote ya kijamii na kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninaiunga mkono kwa sababu ninafahamu vizuri kazi wanazofanya, ninafahamu vizuri umahiri wao na ninafahamu vizuri jinsi walivyopania kuiendeleza na kuiweka Tanzania mahali panapoheshimika na penye sifa za kutukuka katika jamii ya Walimwengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga tena hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, nami kwanza sina budi kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, nadhani ningeanza pia kukupongeza wewe, hasa kwa umahiri wako, uwezo wako na uhodari wako wa kuliongoza Bunge hili Tukufu bila kuwa na zogo, bila kutokuwa na kutokuelewana. Ndani ya Bunge hili kuna Wazee waliokuzidi wewe kwa umri, kuna Wasomi, kuna Wataalam, kuna Maprofesa, lakini hao wote ukaweza kuwamudu na ukaweza kuliongoza Bunge hili ipasavyo. Ninakupongeza sana na ninakutakia kila la kheri wewe binafsi na familia yako yote.

Mheshimiwa Spika, nami pia nianze kutoa pole kwa ndugu zetu, Wabunge wenzetu waliotutoka katika kipindi hiki cha karibuni, Mheshimiwa Abu Kiwanga na ndugu yetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za ndugu zetu hao. *Amin*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze pia kumpongeza ndugu yetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa Chama Kitukufu cha CCM kumweka mgombea wake wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa na chama vile vile kuwa Mgombea Mwenza. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais Zanzibar, Mwenyezi Mungu, awajalie wote hawa walete mafanikio na wapate ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kumpongeza Waziri na Wizara yake, kwa kazi kubwa ambayo waliifanya. Nami ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, uliyoniteua wewe mwenyewe. Tumeona na tumeridhishwa na kazi kubwa ambayo Waziri Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, akishirikiana na Katibu wake Mkuu na watendaji wote wa Wizara, wameweza kutekeleza agizo kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Lakini vile vile napeleka pongezi zangu kwa Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maana msaada wake na kukubali kwake, ndiko kulikolisaidia Jeshi kukamilisha kazi zao, kuweza kupata mahitaji yao yote na kuweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mkuu wa Majeshi, Jenerali George Waitara, Majenerali wake, pamoja na Makamanda na wapigaji wote, tumetembelea mipaka yetu yote ya Kaskazini, Magharibi, Kusini na mpaka Mashariki, tumeona namna vijana wetu walivyokuwa wameweka amani na utulivu. *(Makofi)*

Sisi Watanzania tunainunua amani na utulivu katika nchi yetu kwa bei yoyote. Amani iliyopo Tanzania ni mfano mkubwa, wakubwa hawa kutoka duniani wasingependa kuja Tanzania wakati Tanzania ina vurugu. Juzi tu tumepokea wageni wazito kutoka nchi kubwa za ulimwengu, lakini wamekuja kwa sababu ya amani na utulivu uliopo. Kwa hiyo, Tanzania ni kioo kwa Bara la Afrika. Tanzania wakati wa Mwalimu walisema hatujakuwa huru wala hapajakuwa na amani ikiwa Tanzania peke yake ndiyo iko huru, wakati nchi jirani bado zinatawaliwa na wakoloni. Kweli alisimama kidete na Mungu ametusaidia, leo Tanzania imekuwa huru kweli baada ya kuwa nchi jirani zote ziko huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa sababu niliwahi kumwomba katika Bajeti zilizopita katika kambi yangu ya Bumbwini, moja kati ya kambi zilizokuwa mpya, lakini ilikuwa na shida kubwa sana ya usafiri na maji. Nashukuru na kumpongeza kwamba, sasa nimeona tayari mitaro inaendelea na maji yatapatikana hivi karibuni. Aidha, nimeona pia usafiri unaandaliwa kupelekwa na uzio niliokuwa naulalamikia pia naona unaandaliwa ili kuweka amani na utulivu wa maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona Hospitali ya Bububu, maendeleo makubwa yanapatikana. Ujenzi unaboreshwa, inajengwa kisasa. Kwa sisi wastaafu wa Jeshi na hata raia, ile ndiyo hospitali yetu kuu tunayoitumia. Siku moja nilikuwa nazungumzia katika Kamati yetu ya Ulinzi kwamba, nilipata mgonjwa katika jimbo langu, nililetewa mtoto mmoja ameziba mkojo. Nikashauri tumpeleke haraka haraka katika Hospitali ya Bububu. Tulipofika Bububu tukamweleza daktari kwamba, huyu mtoto hawezi kupata mkojo na hivi sasa anapiga kelele kwamba, hawezi kukojoa. Basi madaktari walitumia utalaamu wao, walifungua bomba la maji wakamwambia kojoa, yule mtoto akakojoa pale pale. Nikashangaa utalaamu huu pia Bububu upo. Kwa hiyo, wengi walikataa kuniamini, lakini waliniamini baadaye kwa sababu wenyewe walikiri. Kwa hiyo, hospitali ile inatusaidia sana na Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona nilipokwenda kutembea Pemba pia maendeleo ya ujenzi unaofanyika katika kambi iliyoko sehemu ya Chakechake. Nimeona kweli hatua kubwa imepigwa, ambapo tulipiga kelele sana kwamba, kambi ile imeachwa na kwa kweli si kwa nia ya kuachwa ilikuwa bado hali ya kifedha haijapatikana lakini zilipopatikana fedha, naona Waziri amelishughulikia suala hili. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima nirejee katika kuipongeza Kamati yako ya Ulinzi na Usalama uliyoiteua, imefanya kazi nzuri na nimpongeze zaidi Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dr. Samwel Malecela, amechukua juhudi kubwa kuiongoza Kamati ile. Wakati mwingine tunafika mahali tunakwama, anatuongoza mpaka kwa Amiri Jeshi Mkuu, kwenda kupeleka matatizo yaliyoko katika vikosi vyetu, kwa bahati tunafanikiwa. Kwa hiyo, nampongeza sana, nasema ile ni hazina ya Chama cha Mapinduzi. Waswahili wanazungumza kwamba, pale panapo wingi udhia penyeza yako rupia. Lakini sisi CCM tunasema, pale panapo matatizo basi umpeleke Mzee John Samwel Malecela, utaona mambo yanavyokaa sawa. Kwa hiyo, nampongeza sana, nasema hazina ile tuitumie katika chama na tuitumie katika Serikali, ni hazina nzuri itatusaidia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi mwenyewe nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa hiyo, niliijadili sana Bajeti hii na sikuwa na pingamizi nayo sana, kwa sababu nimeiona imepangika, wenzetu hawa Wizarani walifanya kazi nzuri kabisa kuipekua kabisa na kutuletea ikiwa safi. Kwa hiyo, natamka rasmi kwamba, mimi binafsi na Wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini, tunaipongeza na tunaiunga mkono hoja hii ya Waziri kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa mara nyingine tena na nikutakie kheri na mafanikio mema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa asubuhi hii ya leo. Kabla sijaendelea mbele, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwanza kwa hotuba yake nzuri, ambayo ina ufafanuzi mzuri tu wa maeneo yote kuhusu ulinzi nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kumshukuru Waziri na Maafisa wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa, nataka kuliongelea ni mwanzo kuhusu Kambi ya Potoa au Jeshi kwa ujumla katika upande wa Zanzibar. Kambi ya Potoa imeanzishwa mwaka 1972 na ikafunguliwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, katika mwaka huo wa 1972 na ni kambi nzuri tu. Lakini kulingana na mategemeo inakwenda vizuri lakini ina matatizo madogo madogo. Namshukuru sana Waziri, mwaka 2003 alipofanya ziara Zanzibar na kwenye Kambi ya Potoa, alifika na kuiona hali halisi ilivyo. Tukafanya mazungumzo mazuri tu na yeye mwenyewe Waziri na Maafisa walioko katika Kambi ile na mwisho wake tukamalizia kwa Rais wa Zanzibar kuhitimisha ziara yake. Kwa kweli nashukuru kwa hili, ni mafanikio makubwa. Ni usemi wa Kiswahili unaosema kuwa “mgeni njoo mwenyeji apone”. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa hatua ya mwanzo, namshukuru sana Waziri kuja kwake tumefaidika katika hatua moja ya kupata umeme katika Kambi ya Potoa, ambayo ndiyo ilikuwa kilio cha miaka mingi tokea mwaka huo mpaka kufikia mwaka huu ndiyo imepata umeme. Namshukuru sana kwa msukumo wake huo, ambao kaacha kumbukumbu kule ya kuhakikisha kuwa, umeme Potoa umefika. Mimi najivunia kuwa katika wakati wa Ubunge, nimesukuma hilo jambo ambalo limefanyika kwa ufanisi. Kwa hiyo, namshukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Kuna baadhi ya matatizo ambayo hayajaisha kama matatizo ya maji katika Kambi ile. Suala hili tumelizungumza vya kutosha na tukafikia mahali ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kupitia Rais, aliyeahidi kuwa anaweza akaisadia Kambi ile. Lakini tatizo kubwa lililopo Kambi ile haina Bajeti katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, angalau tuone kuwa, kama kuna Bajeti ambayo inakuja kwa Sekta za Muungano kupitia Zanzibar, basi iwekewe fungu maalum na mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wanaweza wakafanikisha hili suala na wakaweza kufanikiwa katika suala la maji katika Kambi ile.

Kwa kweli ni tatizo kubwa na utaratibu uliopo hivi sasa, lazima tupate machine ambayo inaweza ikasukama maji kwenye mlima, kwa sababu Kambi yenyewe iko kwenye mlima na huwezi kuyapandisha maji kwa njia ya kuweka mabomba tu, lazima upate na mashine ambayo inaweza ikasaidia katika kuhakikisha kuwa, yanaweza yakafika kwa urahisi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kwa hili naomba sana, tuangalie wale Wanajeshi wasitumie magari kubebea maji, wanatumia mafuta mengi kubeba maji na kupeleka katika Kambi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu miundombinu ya Majeshi kama majengo, mahodhi ya maji na mambo mengine na barabara na kadhalika. Kwa kweli, katika baadhi ya Kambi mambo haya kwa kweli yana hali mbaya ukilinganisha jinsi yalivyoanza. Kwa mfano, Kambi hiyo hiyo ambayo naizungumzia kuwa ukarabati wa majengo lazima ufanyike kila baada ya muda, kwa sababu nafikiri mwaka huo 1972 mpaka leo hakuna ukarabati ambao umeweza kufanywa na ukaleta ufanisi wa kutosha katika Kambi ile. Kwa sababu hiyo, naomba hiki kifungu ambacho kimetengewa Zanzibar, kwa ukarabati wa majengo na barabara ambazo zinaingia ndani ya Kambi za Majeshi, basi ihakikishe na Kambi ile inafikiwa katika kifungu hicho ili kuhakikisha kuwa barabara na nyumba ambazo wanaishi wajeshi wetu zina ukarabati mzuri.

Mheshimiwa Waziri, aliziona kwa sababu tulitembelea kwenye *manage quarters* zote za Wanajeshi, Mchangani pale Kivunge na tuliitembelea na hiyo Kambi ya Potoa, tukaona majengo ambayo bado yanahitaji ukarabati. Kwa kweli tunashukuru lakini ukarabati unafanyika pale wanapokuja wageni kutoka nje. Kwa mfano, wanapokuja *engineer* kutoka nje, kwa mfano, China, wanapokuja kutengeneza *radar* au mitambo mingine, basi hii nyumba inafanyiwa ukarabati. Lakini inafanyiwa moja tu ya kuweza kuishi wale wageni,ukarabati wa nyumba nyingine unakuwa bado hauwekwi katika Bajeti ambayo inaweza ikakarabati nyumba zote zile zikawa ni bora na wakaweza kuishi Wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, kwa kweli kituo kile kilipoanza kilianza na huduma nzuri tu ya afya na tulikuwa tunafaidika sana katika kijiji chetu, kuhakikisha kuwa wanapata hata madawa ya ziada ya kusaidia raia wa kawaida. Lakini kulingana na siku zinavyokwenda, madawa hawapati ya kutosha hata wao wenyewe kuhakikisha kuwa wanaweza wakakidhi haja hiyo. Kwa hiyo, ipo haja licha kuiangalia Hospitali ya Bububu, ambayo ni ya kanda, lakini tuziangalie na hizi hospitali ambazo ziko kwenye vituo, ambazo zina msaada mkubwa kwa sababu kutoka kwenye vituo vya Vijijini kuelekea Mjini kidogo ni mbali, kwa hiyo, huduma inachelewa kufika. Naomba hili tuliangalie, tuwaongezee madawa katika zile hospitali zilizomo ndani ya Majeshi, ambazo zamani zilikuwa zinasaidia vizuri tu hata raia wanaoishi katika maeneo yale, wanaweza wakafaidika na huduma ambazo wanazitoa Wanajeshi na Wananchi walikuwa wanalifurahia Jeshi kuhakikisha kuwa lipo katika kijiji chao na wao wanafaidika katika huduma hiyo nzuri iliyokuwa inatolewa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu suala la michezo majeshini. Suala la michezo majeshini hivi sasa limekuwa ni kama kimbilio la wanamichezo walio wengi Tanzania. Ndiyo sekta ambayo imebaki, ambayo inaweza ikadumisha michezo kulingana na sababu mbili zifuatazo: Sababu kubwa ambayo hivi sasa michezo jeshini inadumu ni kuwa nidhamu ya Jeshi kwa kweli ni nzuri na michezo inadumishwa vizuri. Kwa sababu jeshini bado nidhamu iko ya hali ya juu kulinganisha na uraiani. Kwa hiyo, bado wanamichezo wanatii amri zote za kijeshi na za kimichezo. La pili, ambalo ni kivutio ni kuwa, michezo jeshini inasababisha watu wanapata ajira ya kuhakikisha wanaweza wakaendeleza maisha yao. *(Makofi)*

Lakini la msingi ambalo nataka kuliomba, tuongeze Bajeti katika michezo, kwa sababu zipo timu zetu ambazo hivi sasa ziko katika mbio za mashindano, lakini wakati mwingine wanakwazwa na hali halisi ya fedha ambazo zinatengwa katika michezo, kwa sababu inawezekana kuwa wanatumia michango yao au wanabuni wao wenyewe, lakini hasa ni Bajeti gani ambayo inaweza ikawasaidia, inaonesha hakuna rasmi. Kwa hiyo, naomba Waziri, hili aliangalie kuhakikisha michezo katika Jeshi inatengewa fedha za kutosha kwa sababu inaleta sifa nzuri hivi sasa Tanzania. Kwanza, nidhamu, halafu ni ajira. Timu zetu za jeshi hivi sasa za ni timu ambazo zinafanya vizuri zaidi kulinganisha na timu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wangu, naona ni bora hivi sasa tuondokane na hii tafurani iliyopo ya kuchukua watoto wachache kutoka Zanzibar, kuchukua watoto 50 kuwaleta Tanzania Bara kwa ajili ya JKT. Naona kuwa hivi sasa Serikali ya Muungano, iombe eneo hasa Zanzibar iweke Kambi ya JKT, ambayo itaondoa bughudha nyingi, kwa sababu kuna suala zima la kupata Majeshi. Watu wanapata tu uraiani manung'uniko kibao, ambayo yanalikumba hili Jeshi letu katika kuajiri hawa. Lakini tukiweka kituo maalum, ambacho kitaweka watoto ambao wanapita pale kama ni JKT halafu wanachukuliwa pale kwenda katika Jeshi la Wananchi, wanachukuliwa pale kuingia kwenye polisi, basi ingesaidia sana kuliko kupita uraiani tu kutafuta watu. Kwa hiyo, naona hili suala tungetafuta eneo tukaweka kituo maalum cha JKT Zanzibar, ambacho kinaweza kikasaidia katika suala hili kwa sababu kule angalau wanawekwa kama ni

Wanajeshi ambao watarajiwa wanaweza wakaingia katika sekta hizi ambazo nimezitaja hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia ni kuhusu hawa Wanajeshi wetu, lazima tuwawekee mikakati ambayo watakuwa ni watu ambao baada ya kumaliza kazi wataweza kuyamudu maisha yao. Kwa hiyo, lazima tuwapatie mikopo ambayo ikawasaidia katika kuhakikisha kuwa, wananufaika au wameishi jeshini na badala yake walipostaafu wanaweza wakaendeleza maisha yao mpaka kifo kikawachukua. Kwa hiyo, tuhakikishie kuwa, tunawapatia mikopo ambayo ni nafuu kama vifaa vya ujenzi, kuliko kuwapatia vifaa vya usafiri kama magari, ambavyo wakati mwingine havisaidii katika maisha yao ya baadaye. Kwa hiyo, ninachoomba, tuwapatie Wanajeshi wetu angalau wakistaafu wasiishi uraiani pekupeku, wanaweza wakaishi mahali ambapo wamejiandaa wakati wa ajira yao. Kwa hiyo, hili naomba kuwa, tuwaangalie kuwapatie Wanajeshi wetu vifaa vya vijenzi, si vifaa vya usafiri kama hivi sasa ambavyo vinatolewa, tuwapatie vifaa vya ujenzi ambavyo vinaweza vikawasaidia katika kuhakikisha kuwa wanaweza wakaishi vizuri baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya Wanajeshi, kwa kweli ukilinganisha na sekta nyingine, Wanajeshi wanapata mishahara mizuri tu. Lakini kuna manung'uniko ya wale ambao wako chini ambao siyo maafisa, yaani kutoka *private* mpaka *corporal,* manung'uniko yapo kidogo kuhakikisha kuwa, maslahi yao ni duni kulinganisha na kazi ambayo wanaifanya na kulinganisha na kipato wanachokipata. Lakini tuangalie katika mtazamo huo na tuhakikishe kuwa mambo yote yaangalie Bajeti ya nchi ilivyo. Lakini hata hivyo, tuwaangalie na wao kwa zile kazi wanazozifanya. Kwa sababu wanadai kuwa maafisa wao ni waratibu wa shughuli, lakini watekelezaji wa shughuli bado kipato chao ni kidogo na wanahakikisha kuwa, wanasumbuka na maisha kulingana na kazi ambayo wanaifanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *ration allowance* walisema imepandishwa mpaka kufikia shilingi 90,000, lakini wanadai kuwa bado ipo pale pale kwenye shilingi 60,000 inaonesha kuwa kuna jambo hapo katikati linapata au urasimu. Wanachoshangaa, wanasema unapokwenda likizo au mafunzo ile inakatwa. Sasa kitu ambacho kimewekwa kwenye Bajeti lakini unakikata ambapo ukienda mafunzo au kozi hupati , sasa je, inakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie machache katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Phillemon Profesa Sarungi. Kwanza, nataka nichukue nafasi hii nikushukuru wewe binafsi, kwa muda wote tuliokaa wa miaka mitano, umetuongoza vizuri hapa Bungeni. Hata kama tulifanya makosa, basi tunaomba utusamehe kwa sababu binadamu si mkalifu wa mambo yote katika dunia hii. Kwa hiyo, nakutakia kila la kheri katika kazi zako za Uspika na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, atakusaidia kipindi kijacho tutakuwa nawe, *Inshallah. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga, kwa kazi nzuri wanazozifanya. Naamini Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, ana uwezo wa kuongoza Wizara yoyote ile katika nchi hii. Nilichojifunza kipindi kilichopita, alikuwa Waziri wa Afya, alifanya kazi nzuri katika Wizara ile. Amepewa Wizara hii, amefanya kazi nzuri sana kuliko alivyokuwa Waziri wa Afya. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, huyu mwenzetu ni Mbunge wa kuchaguliwa, kwa hiyo, muda ukifika, Wananchi wa jimbo lake, wasifanye makosa wakamwacha, hii ni hazina nzuri katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Vile vile nachukua nafasi hii, nampongeza Mkuu wa Majeshi, Wanajeshi wote na Wafanyakazi wote katika Taasisi hii, kwa kufanya kazi nzuri ya kulinda nchi yetu, pamoja na kutulinda sisi raia wa nchi hii. Lakini pia nachukua nafasi hii, kuwapongeza waandishi wa habari wote, *Television* za aina mbalimbali, waandishi wa habari, maana kama si wao, tusingesikika hapa tukiongea. Kwa hiyo na ninyi nawapongeza sana na Mwenyezi Mungu, atawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya pongezi hizo, mchango wangu nataka niuelekeze katika maeneo machache, hili moja nimetumwa lazima niseme mwanzo pengine inawezekana Wanajeshi wasije wakasema sikulisema. Nimetumwa na baadhi ya wastaafu, wale wanaochukua *pension* ya miezi sita, wanasema hivi huu muda waliopangiwa ni mrefu mno kwa hiyo, wanaomba wapunguziwe baada ya miezi sita, walipwe kila baada ya miezi mitatu. Nafikiri wastaafu mmenisikia huko taarifa yenu imefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nililotumwa, nataka niliseme hili kwa sababu juzi nilipokuwa nikichangia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nililisema hili hili na leo nitalisema hili hili. Wanajeshi wakishastaafu wanahitajika kufuata mafao yao Makao Makuu ya Jeshi Dar es Salaam. Kwa kweli jambo hili kero tena kero kubwa, kwa sababu wewe mstaafu ukitoka katika Mikoa mbalimbali kama Mtwara, Singida, Kusini Pemba, Mkanyageni na kadhalika, kufuatia mafao yako Dar es Salaam, pale Dar es Salaam huna nyumba, huna mjomba, huna shangazi, huna mahali pa kukaa. Tatizo ni hili lifuatalo sasa ukishafika pale siyo kwamba, mafao yale utayapata siku ile ile, utaambiwa basi ngoja wiki ijayo, ngoja mwezi ujao, baadaye unarudi tena kule kule.

Nauli aliyoitumia si chini ya shilingi 50,000 mpaka 60,000. Sasa natoa ushauri ufuatao: Ili kuwapunguzia matatizo hawa wastaafu ni vizuri Wakuu wa Majeshi au Wakuu wa Vikosi au Serikali yenyewe, isimamie kuwapatia hawa wastaafu fedha zao badala ya kuwaambia wafuate Dar es Salaam. Lakini hapo hapo ukishafika Dar es Salaam, kuna Mifuko chungu nzima, anaweza pengine akaacha kazi akaenda *PPF* akaambiwa Mfuko wa *PPF* wewe huhusiki, pengine uko *NSSF*. Kwa hiyo, hili nataka niseme kuwa, akisha ajiriwa askari, basi aambiwe mapema kuwa wewe ajira yako uko katika Mfuko wa *PPF* au mwingine ili akifika kule wakati wa kufuatilia mafao yake, ajue yuko katika Mfuko gani. Hili nilitaka niliseme kwa sababu lilishatokea, kuna mfanyakazi mmoja alifuata mafao *PPF* akaambiwa *PPF* ni Mfuko tu wa mambo ya Manispaa na

kadhalika, uko Mfuko mwingine. Nasema jambo hili nalo askari hawa waambiwe mko katika Mfuko gani ili mtu akifuatilia ajijue nafuatilia fedha yangu katika Mfuko fulani.

Mheshimiwa Spika, nimeshapata wivu kwa sababu kuna hospitali nyingi za Jeshi. Kwa mfano, pale Unguja kuna Hospitali moja ya Bububu nzuri tu, lakini kilio changu, Pemba hakuna hospitali kama hii. Sasa Mheshimiwa Waziri, naomba pale Pemba na sisi utuangalie kwa jicho la huruma, tupate hospitali ya kijeshi, kwa sababu Wanajeshi wanafanya kazi nzuri sana katika matibabu. Tunaomba hospitali kama hii ya Bububu basi moja mjenge Pemba ili tutakapopata matatizo, tujue pa kukimbilia, vinginevyo tutaendelea kusafirisha wagonjwa wetu pengine Bububu na maeneo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka nilizungumzie ni maisha ya Wanajeshi hasa wanyonge. Mwenzangu Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, alishazungumzia. Hivi sasa askari wengi wanaishi katika nyumba za kupanga, kwa sababu pamoja na kuwa kazi nzuri imefanywa ya kujenga nyumba za Majeshi ziko nyingi tu, lakini hazitoshi. Sasa askari wengine wanaishi katika nyumba za kupanga. Kwa hiyo, nyumba ya kupanga utalemaa nayo ile kijijini kwenu huna nyumba, sasa katika kazi, kuna kustaafu au kustaafishwa, tatizo sasa lipo hapa, ukishastafishwa kazi ukirudi kijijini kwenu huna nyumba, sasa niambie utaishi wapi? *(Makofi)*

Lakini hapo hapo kazini alipo yeye nyumba ya kupanga haina dhamana yoyote, anaweza akasema maadam nimeshaacha Jeshi, nyumbani kwetu sina nyumba, ngoja niishi katika nyumba ile ile niliyokuwa nikiishi wakati niko Kambini. Mimi nawahakikishia kuwa, ukishaacha kazi huna uwezo wa kupanga nyumba, siwaambii Wanajeshi, hata mimi Mbunge, nikimaliza kazi ya Ubunge, sina uwezo wa kupanga nyumba, itabidi nirudi kijijini kwetu. Kwa hiyo, naomba Wanajeshi wafanyiwe mpango wa kutafutiwa fedha na vifaa vya ujenzi, wajenge nyumba katika Vijiji walivyotoka ili wakitoka angalau basi waishi katika nyumba zilizoko katika vijiji vyao. *(Makofi)*

Lakini lingine nataka kusema kwamba, mishahara nayo pia iongezwe. Wenzangu wengi walikuwa wakilia na mishahara ya Wanajeshi, pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa, tangu hapo mshahara hautoshi, sijawahi kusikia hata siku moja mtu aliyelipwa mshahara akasema mshahara wangu mkubwa, huyo najua hayupo, lakini mishahara najua inazidiana. Kwa hiyo, naomba mshahara wa wanajeshi nao pia uongezwe ili waweze kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, unajua huko zamani ilikuwa ukishakuwa mwanajeshi tu, basi haraka unapewa mke, maana ndiyo tena mwanajeshi, mzuri, hodari. Nataka nikuambie kuwa, watu wengi hawapendi kuolewa na wanajeshi. Kwa sababu wanaonekana pengine ni watu wa kuruka ruka. Nasema kwamba, ni vizuri pia wanajeshi wafanyiwe maarifa ya kuongezwa mishahara ili waweze kuishi vizuri katika familia zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na sitapata nafasi tena ya kusema hapa Bungeni, napenda niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mkanyageni Pemba, kwa kunichagua kuja hapa Bungeni na naamini kuwa waliyonituma nimeyasema. Kwa

sababu tangu nimekuja Bungeni, nimeshauliza maswali mengi ya msingi na ya nyongeza. Nimeshachangia sana katika Wizara mbalimbali, kwa hiyo, naamini kipindi hiki kinachokuja watanichagua tu kwa kura nyingi ili tuonane tena hapa Bungeni katika ule Ukumbi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA S. ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Awali ya yote, naomba nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na yenye kuonekana, mwenye macho haambiwi tazama. Lakini pia napenda kuwapongeza Watendaji Wakuu wote wa Jeshi hili, pamoja na Maafisa. Nawapa hongera sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muda wangu wa miaka mitano niliyokaa katika Bunge, Bajeti yote ya miaka minne iliyopita, sijawahi kuchangia katika Wizara hii. Lakini leo nimehamasika na nimeshawishika kuchangia katika Wizara hii kwa sababu nyingi tu. Mojawapo ni jinsi utendaji kazi ambao umefanyika katika muda wa miaka minne. Kazi imetendeka kwa umahiri zaidi na ubunifu ambao unaonekana nchi nzima na hata nchi za jirani wanajua nini jeshi letu limefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wameweza kuwajibika kwa muda wa miaka yote, lakini hususan zaidi miaka minne ambayo mimi nimefuatilia, nimekuwa karibu zaidi kwa muda wote na ubunifu ambao wameweza kuuonesha na moyo wa kujitolea katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa. Lakini hili la kujitolea nitalifafanua kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la kujitolea, napenda nilipongeze sana Jeshi letu la Ulinzi, kwa sababu wameweza kujitolea katika mambo mengi, lakini hususan kujitolea katika maafa. Mwaka 2003 tulipata janga kubwa ambalo lilitokea kwa treni yetu kupata ajali. Mimi nilishiriki mpaka kwenda kuona kwenye tukio na Wabunge wenzangu wengi ambao ni mashahidi na vyombo vya habari vingi ambavyo vilitangaza ndani ya nchi na nje ya nchi. Jeshi letu lilifanya kazi usiku na mchana. Kwa kweli kazi ile ni ya kujitolea na ya moyo na upendo kwa sababu pamoja na kuwa ni jeshi, lakini wale Watendaji walikuwa na moyo wa upendo, moyo wa huruma, ndiyo wakayafanya yale ambayo yaliweza kufanikisha maafa yale yakafikia mpaka leo hapa tulipofika, hali ikawa nzuri, waliotakiwa kuzikwa wakawa wamezikwa.

Mheshimiwa Spika, zaidi napenda kuwapongeza Wananchi wa Jimbo wa Rorya katika Wilaya ya Tarime, Mkoani Mara. Maana ya kusema hayo, ni kumpongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Bila ya Wananchi wale, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, asingeweza kushiriki katika maafa yale ambayo aliacha kazi zake zote na kuweza kushirikiana na Watendaji wake wa Jeshi la Ulinzi, kuanza kuwashughulikia Wananchi ambao wamepata maafa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi na hasa zaidi Wananchi wa jimbo lake, ambao wamempigia kura yeye, ambaye sisi tumekuja

kunufaika katika nchi yetu, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa anaifanya katika maafa yale. Mungu atakujalia imani na utazidi kuendelea na nawaomba sana wakuchague tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika eneo la pili katika nafasi ya JKT. Namshukuru Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Wananchi wote. Nina imani kuwa, wanamshukuru kwa sababu ilipofika 2001, akaomba uwepo utaratibu au aliagiza uwepo utaratibu wa kuanzisha JKT. Muda wangu ambao nimekuwa nikichangia katika Bunge, nilikuwa nikipiga kelele sana kuhusu ajira za vijana. Lakini katika kitengo hiki kilichokuwa kimeanza mwaka 2001, kimeweza kutusaidia JKT kuchukua vijana wengi ambao wameweza kuingizwa katika Jeshi letu la Kujenga Taifa na vijana wale kuweza kujiandaa katika mbinu mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri, amezifafanua kwenye kitabu chake cha hotuba, jinsi wanavyoweza kupata mafunzo ambayo wanayapata kama wanavyopata katika utaratibu wa *VETA.* Hiyo ni sababu mojawapo ya kuwapongeza sana na kuwashukuru na kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa yale ambayo ameweza kuyandaa na kuyaonesha. Lazima Wananchi waelewe kuwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bado ana nafasi kubwa ya kuwajali vijana wake wa Tanzania. *(Makofi)*

Lakini pili, napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mwamunyange, kwa jinsi anavyoweza kuwaenzi vijana wale na kuwa nao karibu. Haya yote yanatokana na utendaji ambao anaufanya na kuweza kuamini kuwa JKT, itaendelea, itadumu na itazidi kuimarika kwa maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ningependa kuzungumzia kuhusu bajeti iliyopita, Mheshimiwa Waziri alituletea magari hapa tumekuja kuyaona katika Viwanja vya Bunge. Kwa kweli magari yale wamejitahidi sana kutengeneza na sasa hivi Serikali iangalie siyo yale tu ambayo wametuletea tumeyaona. Lakini bado Serikali lazima iangalie iwasaidie kuwapelekea pesa nyingi, waweze kutengeneza magari ambayo yatawasaidia wao wenyewe. Si lazima tuwe tunachukua pesa kuagiza magari nchi za nje, wakati Watendaji wetu wanao uwezo wa kufanya kazi hiyo na kupunguza pesa nyingi ambazo zinakwenda nje. Lakini bado pia katika maendeleo ya Wananchi na hasa suala la kilimo, kama tutachukua pesa zetu nyingi kupitisha katika maeneo haya, itaweza kutusaidia wakatengeneza pia matrekta ambayo yanaweza yakapelekwa katika kila Mkoa, Wilaya, kwa kuwakodisha Wananchi wetu waweze kuanzisha kilimo cha matrekta ili kuepukana na kilimo cha jembe la mkono. Haya yote yanawekezana katika nchi yetu, lazima tuwe na dhamira na nia, tunaweza tukayafanya na Serikali yetu iweze kuangalia maeneo haya ili utaratibu huu uweze kufanyika badala ya kuwa tunaagiza matrekta na magari katika nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali iangalie kwa sababu pesa hizi hazitapotea. Pesa hizi zitakuwa ndani ya nchi yetu, kilimo kitasaidia katika nchi hii. Kwa hiyo, lazima Serikali iangalie mambo haya kama vile Wizara ya Ujenzi ilivyoangalia badala ya kwenda kutafuta wakandarasi maeneo mengine, ikatumia jeshi letu na jeshi limefanya kazi nzuri ya kujenga nyumba ambazo zinaonekana, zenye sifa na zilizokuwa imara zaidi. Kwa hiyo, kama haya yanawezekana na mengine pia

yanawezekana na tunahitaji kuyafanya na itabidi tushangae sana kama Serikali haitatumia jeshi hili iagize vitu vingine nje na uwezo wanao, ili jeshi letu liweze kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali yetu iweze kusaidia haya.

Pili, kuhusu suala la mafunzo. Nchi yetu ya Tanzania ya amani na wako wengi ambao wanaipenda na wako wengi ambao hawaipendi. Kutokana na amani ya nchi yetu wako wanaoshawishika pia hata kuona kwa nini nchi inakuwa na amani. Lakini namshukuru pia Mheshimiwa Ali wa Kambi ya Upinzani, leo alipofuta katika *speech* yake yale maneno ambayo ameyafuta. Nampongeza sana, kwa sababu ya umahiri wake na kuelewa nini ambacho anakifanya ndani ya Bunge na ndiyo maana Wananchi wake wa *CUF* walimpigia kura za maoni na akapita kwa kura nyingi zaidi. Kutokana na ujasiri na wanaelewa kuwa aliyoyaandika angeendelea kusoma lakini kwa kuwa umesoma kwa niaba ndiyo maana ukafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mafunzo, nilikuwa naomba nitoe ushauri, kwa kuwa nchi yetu sasa hivi ina amani na kwa kuwa tunaenda katika sayansi na teknolojia, lazima tupate nafasi ya askari wetu waweze kwenda kujifunza katika nchi ambazo zimeendelea kwa masuala ya kivita. Wakipata nafasi hiyo, itaweza kuwasaidia wale Maafisa na wao kuja kutoa mafunzo yale kwa askari wetu ambao wako ndani ya nchi na maana ya kusema hivyo, kwa sababu lazima tuwe na maandalizi ya kujiandaa na maandalizi ya kujiandaa laiti tutaendelea na utaratibu ule wa zamani au yale mafunzo waliyokuwa wakipata zamani na nchi yetu au nchi zetu zinaenda zinabadilika, hasa kulingana na haya mambo mengi ambayo yanatokea ya kigaidi, watu wana mbinu za aina mbalimbali ambazo zinatokea. Kwa hiyo na sisi askari wetu lazima waende wakajifunze mambo mapya, ambayo yanalingana na sayansi na teknolojia. Wengine wanaita mambo ya *dot.com.*

Kwa hiyo, lazima tukubali Serikali iweke pesa za kwenda kuwapeleka kule askari wetu, wakajifunze ili jeshi letu lizidi kuimarika kisasa na hata wao wanaoifikiria nchi yetu kwa utaratibu ambao hautaweza kuwa wa maana, waweze kujua nchi yetu na sisi iko ndani ya *dot.com.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo, naomba pia nichukue nafasi hii, nimpongeze hasa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa John Samwel Malecela, kwa kazi yake nzuri ambayo ameifanya na Taarifa yao nzuri ambayo ameitoa kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina imani kuwa, utendaji wake, mawazo yake na ushauri wake, ndiyo uliosababisha jeshi letu la Tanzania kuweza kufanya kazi nzuri zaidi mpaka limefikia hapa ilipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nimefarijika kabisa kulingana na kina cha hotuba hiyo na

maudhui yote yanayohusiana na mambo ya Ulinzi. Kwa sababu hiyo, nampongeza yeye Waziri, Katibu Mkuu na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa Tanzania, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuandaa hii hotuba ambayo ameiwasilisha mbele ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yanategemea kwa kiasi kikubwa sana, utulivu na usalama katika nchi. Ni kwa sababu hiyo, nchi yetu ikapata bahati ya kupunguziwa madeni. Hii maana yake ni kutokana na Utawala Bora na Utawala Bora hauwezi kuonekana mahali ambapo kuna vurugu, hakuna usalama. Lingine ambalo linathibitisha hali ya utulivu ni kuvutika kwa wawekezaji kuingia katika nchi yetu katika sekta mbalimbali za uchumi. Pia ni kuendelea kuingia nchini kwetu kwa watalii na pia nchi yetu kukubalika kuwa msuluhishi katika nchi zile ambazo zina migogoro.

Mheshimiwa Spika, lingine pia ni nchi yetu kuvutia viongozi, hata wastaafu kama Clinton, alipokuja hapa kwetu na Mama Bush. Kama nchi hii ingekuwa haina amani, basi hawa wasingekuja na kwa hiyo, sifa ya nchi yetu inatokana na kazi nzuri ambayo Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaifanya katika nchi hii, kuweka amani na hivyo ndiyo siri ya maendeleo ya uchumi wetu tunaoupata. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi wa Jimbo la Kigoma Kusini, tuna sababu ya kutoa pongezi na shukrani za ziada kwa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na uongozi wa Jeshi la Wananchi. Kwanza, katika mwambao wa Ziwa Tanganyika, ambao jimbo langu la Kigoma Kusini lina eneo kubwa sana, kuna Kata saba za Simbo, Ilagala, Sunuka, Igunga, Igalula, Buhingu na Kalya, masafa yapatayo kilometa zipatazo 200. Ukanda huu ulikuwa umedumaa kutokana na mashambulizi yaliyokuwa yanafanywa na wavamizi kutoka nchi za jirani na kwa hiyo, uchumi usingeweza kuendelea. Lakini kwa sababu ya doria ambayo imefanywa kwa umakini wa hali ya juu na Jeshi la Wananchi, hali imeanza kutulia na shughuli za uvuvi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango mkubwa mwingine ambao umeletwa na Jeshi la Wananchi kwa jimbo letu ukanda huu wa ziwa, ni kushiriki kama wakandarasi katika kukarabati kivuko cha *MV Ilagala.* Wamekarabati katika muda mfupi na katika ufanisi wa hali ya juu na nataka nimpongeze Mkuu wa Majeshi, alipofika katika Kijiji cha Ilagala, ambapo ndipo uzinduzi ulifanywa na Mheshimiwa Rais, Wananchi hasa wavuvi walisema, sasa tutavua, maana yake jeshi limeingia katika ukamilifu wake katika kuwasambaratisha wote waliokuwa wanajaribu kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Kwa kushiriki katika ukarabati wa hicho kivuko, maana yake jeshi limetoa mchango mkubwa sana wa kuwezesha kujengwa kwa barabara ya mwambao wa Ziwa, ambayo sasa ina maana ulinzi utaimarika kwa sababu ni rahisi kwa vyombo vya ulinzi, kuweza kwenda kutoa msaada mahali ambapo vurugu zimetokea kama kuna barabara tofauti na ambavyo kipindi chote tulikuwa tukitegemea usafiri wa maji ambao ni wa mwendo wa pole pole sana. Kwa hiyo, kwa kufanya hiyo kazi aliyoifanya, maana yake wameimarisha ulinzi, lakini pia tayari wanachangia katika kuibua sekta zote za kiuchumi katika ukanda ule, ambazo zisingeweza kuibuka bila mawasiliano ya barabara. Kwa hiyo,

wamechangia sana katika kuhamasisha ari ya Wananchi katika uvuvi, kilimo, utalii, misitu, madini na katika biashara na huduma za jamii. Kwa hiyo, yote haya ni mambo ambayo sisi wa Jimbo la Kigoma Kusini, tuna sababu ya kuyapongeza na kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi maalum kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge letu Tukufu, inayoongozwa na Mheshimiwa John Samwel Malecela, Makamu Mwenyekiti wa Chama chetu. Kamati hii imefanya ziara katika Mkoa wetu na imewahamasisha Kamati ya Mkoa na ya Wilaya, ambazo kwa kweli baada ya hamasa hizo, zimefanya kazi nzuri na kwa namna ya pekee, napenda nimpongeze Mkuu wa Mkoa, Kanali Mstaafu Ermon Mahawa. Hivi karibuni ametoa agizo kwamba, wale wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria wazisalimishe. Hii ni hatua ambayo itazidi kusafisha mabaki yaliyokuwa yakichangia katika kuleta matatizo katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze pia Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Ndugu Henry Clemence, kwa ujasiri wake, pamoja na kwamba, siyo mwanajeshi, wamekuwa wakimwita ni Kamanda wa Mgambo, kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya utulivu na amani katika eneo letu.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nizungumzie ushirikiano mzuri sana ambao umekuwepo kati ya Wananchi na jeshi letu. Katika maeneo mbalimbali, kwa mfano, Sibweta, Mkomkwa-Buhingu, Serikali za Vijiji na Wananchi wamejenga majengo kwa ajili ya matumizi ya vikosi vyetu vilivyo katika doria. Ushirikiano huu, umedhihirisha jinsi ambavyo jeshi letu liko karibu na Wananchi na kwa hiyo Wananchi, pamoja na jeshi nawapongeza sana kwa ushirikiano huo. Katika maeneo mengine hata wavuvi wameunganisha nguvu zao, wakaunda mitumbwi na hata kununua injini ili wasaidiane na wanajeshi katika doria. Walishanituma katika hili kwamba, pale wanapokuwa wameandaa zana hizo za kufanyia kazi, wangependa wafikiriwe ruzuku kwa mfano ya kununua injini ambayo inatumika katika ulinzi. Kwa hiyo, Serikali ingeliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, huyu kama alivyosema mwenzangu, anaweza kuingia katika Wizara yoyote. Kauli yake katika Wizara hii ya Ulinzi, anapotoa msimamo ni tishio kwa wale ambao wanadhani wanaweza kuwa na ubavu wa kuja kuisumbua Tanzania. Kwa sababu hiyo, ni matumaini yangu kwamba, wapiga kura wa Rorya, hawatasita kumrejesha katika utumishi wa umma. Baada ya mwaka 2000, nilikuwa Dar es Salaam nikisafiri kwenye basi nikasikia watu wakizungumza, wakasema baada ya matokeo ya uchaguzi, mikoa ambayo imeonesha Wananchi wake wana msimamo waliutaja Mkoa wa Mara na Mkoa wa Kigoma, Rorya na Kigoma Kusini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naamini kwa sababu hiyo, hao watu wa Rorya na wa Kigoma, wataendelea na msimamo huo na kwa wale ambao nimesikia kwenye magazeti wanasema tunataka kwenda Kigoma Kusini, siyo kwa sababu Mbunge aliyepo hajafanya

kitu, ila kwa sababu nina kitu moyoni. Huko ni kukiri kwamba, wanaona maendeleo lakini wanataka kwenda kuridhisha kiu zao tu za kwenda kujitokeza kwa Wananchi. Lakini Wananchi wanafahamu, kwa msimamo wao, watawapa nafasi zao zinazostahili. *(Makofi)*

Nawapongeza Waandishi wa Habari, kwa sababu waliyaweka maneno yake kama alivyokuwa ameyasema huyo aliyekuwa anayazungumza, kuja kujaribu na kwa sababu hiyo, nawafahamisha Wananchi, nilikwisha wafahamisha kwamba, narudi na kwa haya yote yaliyofanyika, nina uhakika watachambua kati ya mchele na pumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kutoa shukrani. Kwanza, kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kuendesha vikao hivi, nimejifunza mambo mengi sana, kwa umahiri wa hali ya juu. Lakini pia nakushukuru kwa kunichagua katika Kamati ya Kilimo na Ardhi. Kwa sababu watu wangu wengi ni wakulima na nimejifunza mengi. Kwa hiyo, ninapokwenda nawazungumzia ya uhakika. Nakushuru sana. Kama nitarudi, naomba usiniweke Kamati nyingine. *(Kicheko/Makofi)*

Nawashukuru pia Wabunge wote, kwa kweli katika Bunge hili, nimejifunza mengi katika miaka hii miwili na nusu. Ni chuo cha hali ya juu. Hekima zilizopo na uelewa uliopo na siasa na upendo uliopo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. Nakishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi, kwa kunipa heshima ya kunifanya niwe mwakilishi katika jimbo lile, kwa kuniteua na Wananchi kunipa ridhaa waliyonipa kwa kunipa kura. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, kwa sababu tunamalizia, nisiisahau familia yangu, imeniunga mkono sana na kama wanavyosema palipo na mafanikio mwanaume nyuma, yuko mama. Napenda nimshukuru mke wangu, Bibi Rahel Ndeka na wanangu watatu, Stela Ndeka, Geofrey Ndeka na Kizito Ndeka, kwa jinsi ambavyo wamekuwa nami, wakiniombea, wakinisaidia kutimiza kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwanza, naunga mkono hotuba yake kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, amekuwa Mbunge tangu mwaka 1990. Kwa hiyo, kura yangu ile niliyoitoa kule Jimbo la Kigoma Kaskazini na yeye akaja pale Karimjee anaomba kura nikampigia na akashinda, ndiyo matokeo haya sasa ni kazi hii. Kwa hiyo, Jimbo la Kigoma Kaskazini, hawakupoteza na mimi kuweza kumpigia wakati ule bado ni jumuiya.

Lakini hakuishia hapo, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, akiwa Waziri wa Afya, bado alitambua umuhimu wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, Kituo cha Afya Mwamgongo, kwa kuweza kunisaidia baadhi ya vifaa na nilifikisha. Bado ni kazi

aliyoweza kuifanya si kwa kupendelea na maeneo mengine aliweza kuyajali. Kwa hiyo, bado nakupongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi. *(Makofi)*

Bado aliendelea akawa Waziri wa Elimu na Utamaduni, miaka hiyo hiyo. Kwa hiyo, aliiendesha vizuri sana Wizara ya Elimu na Utamaduni, ikiwemo Simba na Yanga kucheza mara kwa mara na wakati ule Simba na Yanga zilikuwa zikikutana uwanjani na nilikuwa namwona uwanjani wakati wote, akizitakia baraka. Lakini Yanga wakati mwingine ilimwendesha Simba vizuri, akiwa ndiyo bingwa mzuri tu na ikaleta vikombe vingi nchini. Kwa hiyo, bado ilikuwa ni juhudi alizoweza kuzionesha. Hakuishia hapo, baada ya utaratibu ule kubadilika, kisheria baada ya vyama vingi, suala la Viti Maalum likawa vimeondolewa. Lakini bado Serikali haikuachia pale, bali ilimpa dhamana akawa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, aliweza kushirikiana na matukio mengi ambayo yalikuwa yanatokea pale barabarani. Husiti kusikia ajali imetokea, lakini Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi yeye ndiyo ameshaingia kwenye ile Hospitali ya Tumbi, yaani mimi niko Kigoma lakini utamsikia yuko tayari. Yaani ameacha ule Ukuu wa Mkoa na kuunganisha mifupa ya watu ambao wamepata majeraha. Kwa hiyo, ni mtu mmoja ambaye huwezi kabisa ukampima kwa kuweka majukumu ya wajibu wake. Hajipendi huyu, ameweka maslahi ya Utaifa mbele kuliko lingine. *(Makofi)*

Nasema hivi, kama kule Rorya wanasema hawataki, njoo Jimbo la Kigoma Kaskazini, kwa sababu utafanya kazi zile zile mimi nitajiuzulu, tutafanya kampeni kwa ajili yako. Maana inawezekana watu wazuri unao lakini usiendelee kuona umuhimu wao, lakini naujua sana umuhimu wa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwangu binafsi. Hasa Wizara ya Ulinzi, hii aliyoingia, nafikiri kweli hapa amefanya kazi vizuri na sisi tunaokaa mpakani ndio tunaoelewa, watu wa Congo, amani yao sijui itapatikana mwaka gani, Burundi na Rwanda. Nimemsumbua mara nyingi sana kuweza kumwelezea hali halisi na anaijua tangu akiwa na Mkuu wa Majeshi aliyestaafu hivi karibu, Jenerali Mboma, naye pia nampongeza sana. Ile milima ya kule kwetu amepanda, siwezi kuamini kabisa Mkuu wa Majeshi anapanda milima, anatafuta maadui wanaokuja nchi mwetu ili waweze kurudi kwao. Haikuwa kazi nyepesi, mimi mwenyewe nimehudhuria JKT, sasa umri huu nikirudi kupanda ile milima kama nilivyomwona Jenerali Mboma, anapanda, anateremka, sio jambo jepesi. Nalipongeza sana Jeshi la Wananchi, kwa kazi nzuri ambayo wanajitolea ya kutulinda. *(Makofi)*

Sasa haya ni mambo ambayo nimeyaona na nimpongeze Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Unajua vyeo vingine vinaangukia mahali pake. Nchi hii ukishindwa kutambua mchango wa Mheshimiwa John Samwel Malecela, kwa kweli sijui utakuwa unafanana na mtu wa aina gani. *(Makofi)*

Mimi mwenyewe kwa Mheshimiwa John Samwel Malecela, huwa nakwenda tu kama nakwenda nyumbani na tena namwambia mzee leo nataka kula, karibu kijana wangu haya na nafika nakula. Lakini ana maneno mengi mazuri, yenye hekima, kwa hiyo, tunahitaji busara na hekima za Mheshimiwa John Samwel Malecela ziweze kudumu. Mkuu wa Majeshi, Jenerali George Waitara, namwona mwenye nguvu na nampongeza. Nilimpongeza tarehe 26 Aprili, 2005, hapa Dodoma, lile jeshi lilivyokuwa linapiga kwata, hebu kila mtu aliyeona aende aelezee ule ukweli, kulikuwa na vijana

wakakamavu wanatembea, nilitamani kurudi enzi zangu, maana kwata ile nilikuwa natamani nishuke kule niende nikajiunge, lakini muda huu wa miaka 54 niliyonayo, haiwezekani tena. *(Makofi)*

Lakini niliona kabisa, sasa nilikuwa najiuliza hivi Jenerali George Waitara, ana umri gani, lilikuwa ni swali moyoni mwangu. Lakini likuwa ni jeshi lenye nguvu, linaonesha ukakamavu kweli na yeye nampongeza kwamba, sasa mapambano ni mazuri. Nilikuwa nayaambia yale majeshi ya jirani kule nawaambia ninyi ni Jeshi la Tanzania, mkileta chochoko mlizozizoea, watatembea kwa miguu, watawateka nyara kwa kutembea kwa miguu, hatuhitaji kutumia vifaa vingine vya ajabu ninyi hamuwezi na nikawaambia mimi nilipitia JKT kidogo, pamoja na hiyo nikipata *recruitment* ya wiki moja tu kama ile aliyoifanya hapa, nikaiona nitaenda kupambana. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini hizi ni juhudi ambazo zinafanywa na Jeshi la Ulinzi, suala la ukakamavu linaridhisha kabisa, nawapongeza na nawaomba liweze kuendelea. Suala la mpakani, baada ya sisi kusema kule matatizo yapo, silaha ni nyingi zinazotoka Kongo, tunalala kwa hofu, kwa hiyo, tuunganishe majeshi yote, sasa sielewi kama kweli kuna mipaka kati ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Polisi au Jeshi la Magereza. Kwa sababu wote hawa wamejifunza pale ile tarehe 26 Aprili, siku ya Muungano hiyo niliyaona majeshi yote, huwezi kutambua ni nani alikuwa anatembea kiunyonge. Kwa hiyo, bado naomba kabisa, natoa wito kwamba, kuwepo utaratibu ambao hizi silaha zinazoingia kutoka Kongo, vita ambavyo ni vya muda mrefu, silaha zinazotoka Burundi, silaha zinazotoka Rwanda, zinatuudhi sana kwa sababu Wananchi wetu wa Kigoma wanaishi kwa usumbufu huo. Sasa tungeomba kuongeza angalau kama ni wanajeshi wengi wawepo pale waweze kutulinda. Wengi nafikiri huwa tunasikia ile mizinga tu ishirini na moja. Lakini kule bunduki za kutoka Burundi tunazisikia mara kwa mara, mashambulizi ya kujibu angalau hao wahuni waweze kusogea tunayapata, sasa ingekuwa ni jambo lililo la muhimu kuweza kuzingatia kwamba, mpakani tunahitaji ulinzi ulio imara.

Vyombo vya kusafiria, polisi tulionao sio wengi, ningeomba tuongeze jeshi la ku-*escort* mabasi yanayotoka Kigoma Mjini kwenda mpaka Kibondo, Mwanza, hali ni ngumu, wanaua watu wetu, yaani kila baada ya wiki mbili, tatu. Sasa sijui kama Jeshi la Polisi au jeshi lingine au vyombo vyote vinavyoweza kuhusiana na ulinzi huu, viweze kuwajibika. Tuongeze hiyo nguvu kwa sababu tumekuwa na mfundo tu labda ni nani aruhusiwe, sijui ufuate utaratibu, utaratibu uko huku Dodoma katikati, tumewalinda sisi huko, tukilindwa kwa nini hamuwezi kupata joto.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelezea lingine hili la Jeshi la Kujenga Taifa. Vijana wengi wanahitaji kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na mimi ningetoa mapendekezo kwamba, sasa hivi tufanye mabadiliko ya makusudi kwamba, wote watakaopata ajira polisi au sehemu nyingine, wawe wamepitia JKT. Kwa sababu sasa hivi JKT hawachukui mtu aliyemaliza darasa la saba, hizo nafasi zinagombaniwa. Kwa hiyo, ninyi mmekuwa na utaratibu ambao sasa hivi unaleta migogoro, mtu akienda kule JKT atajifunza mambo mengi na tusiwaachie watakapokuwa wanamaliza.

Tutoe mapendekezo kwamba, hawa ni vijana, ndio nguvu kazi, waweze kupata mitaji ya kuanzia. Sasa leo huwezi kuanza mitaji ya Serikali sijui zile hela za Serikali zinaenda kufanya nini, wewe unamkopesha mtu mwenye pesa nyingi, kwa hiyo, ni biashara tu hizo ambazo tunataka kusahau kizazi kipya, tuwape wale vijana wetu basi, tuzipeleke huko JKT. Ningetoa mapendekezo hayo kwamba, suala la vijana kujiunga na JKT, lisije likatazamwa kwa mazingira mepesi, litiliwe umuhimu wenye makusudi ya waziwazi ili vijana hawa watakapokuwa wanamaliza, waweze kuwa na kitu kinachoeleweka katika maisha yao, vinginevyo tutakuwa na kizazi cha vijana kisicho na mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, nichukue dakika moja kukupongeza, nimekuwa Mbunge kwa miaka kumi na tano mfululuzo, ningeomba niendelee miaka mingine kumi na tano kama Mheshimiwa Majogo, miaka thelathini. Wewe mwenyewe umeshapita, kwa sababu kazi ambazo umefanya zinaonekana, tulianza kule Karimjee kuna joto lakini hapa hakuna hata joto, sasa unataka kutupeleka tena. Kwa hiyo, kote tunafuatana angalau na wewe miaka kumi na tano ijayo, utakuwa ume-*recruit* Spika mwingine anayeweza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakupongeza na ninakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nataka nimpongeze Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda niungane na wenzangu wote ambao wamempongeza, sitaki niongeze kitu naogopa kuharibu na nataka nikuthibitishie kwamba, yaliyosemwa yote ni sahihi, mimi ni mjumbe katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge lako Tukufu, kwa muda wa miaka yote mitano, nakushukuru sana. Kwa kweli sio kwamba, nilikwenda tu pale, tuliokuwepo wanajua nini tumekifanya na wanajeshi wetu wanajua tulifanya nini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nataka nimpongeze sana na yaliyosemwa ni sahihi. *(Makofi)*

Lingine nataka nimpongeze sana Mkuu wetu wa Majeshi na nimefarijika sana kusikia leo yupo hapa, Mungu ambariki, amefanya kazi kubwa sana. Binafsi kama Omar, nataka nimshukuru sana, kwa mambo mengi ambayo tulikuwa tunawasiliana aliyonisaidia. Kwa niaba yangu binafsi na familia yangu na kwa niaba ya wanajeshi wote walioko Pemba, nataka nimpongeze sana Kamanda George Waitara na Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Spika, mwingine ambaye nataka nimpongeze sana ni Amiri Jeshi wetu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amefanya kazi kubwa sana na ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hilo limethibitishwa. Kwamba, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, imefanyika kazi kubwa sana, tungeomba Watanzania waione hiyo.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imesema katika kipindi cha mwaka 1995/2005, Serikali ya Awamu Tatu, imepata mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu ya ulinzi kwa Taifa ni kweli wala sio siri usalama uliopo Tanzania hatuamini kwamba, uko katika nchi yoyote katika dunia hii, ndani ya Uingereza

hauko sasa hivi, ndani ya Amerika hauko sasa hivi. Lakini ushahidi huu unathibitishwa na viongozi waandamizi wakuu wa Marekani, kufanya ziara ndani ya wiki moja wakati mmoja sio jambo jepesi, ni kazi kubwa ambayo imefanywa na wenzetu hawa, kwa kweli wanastahili kuungwa mkono kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilinukuu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, liko katika ukurasa wa 14 kuhusu ulinzi na usalama wa mipaka ya Tanzania. Katika mwaka 2004/2005, Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania liliendelea kutekeleza moja ya jukumu lake kulinda mipaka ya nchi yetu, watu wake na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kulithibitisha hili, nataka ninukuu vilevile tunaambiwa majukumu makuu ya jeshi letu la Wananchi, ni kulinda na kutetea uhuru na heshima ya Taifa letu la Tanzania. Sasa tuombe wale wenzetu ambao wako kwenye vyama vya siasa au wanasiasa na Wananchi wengine ambao hawapendelei wema wa jeshi hili waache kulipaka matope Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Limewafanyia kazi kubwa, limewaletea maendeleo makubwa katika wakati mgumu na kwa kulithibitisha hilo ni kwamba, tukubali Taifa lote bila ya amani, hakuna maendeleo, lakini vilevile kwa kulithibitisha hilo, nataka niseme kwamba, kuanzia miaka ya sitini mpaka themanini, nchi yetu haikuwa huru wala salama. Katika eneo lote katika Bara la Afrika na duniani kwa ujumla, tulilazimika katika vipindi vyote hivyo, kuingia katika vita katika nchi mbalimbali katika Afrika. Kuanzia miaka ya 60 mpaka 80 na vita vya mwisho tumepigana mwaka 1978 - 79 na 80 na ndugu zetu wa Uganda. Tunaijua kazi kubwa iliyofanywa na wanajeshi wetu hawa, sasa leo kama atatokea Mtanzania, ataweza kulidhalilisha jeshi hili au kulifanyia uadui wa aina yoyote, kwa kweli atakuwa hakuifanyia haki nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1978 - 79, majeshi yetu yalilazimika kupigana na ndugu zetu wa Uganda, kwa sababu tu ya jeuri ya Nduli Iddi Amini na majeshi yake ya uvamizi na yalitulazimisha kuingia vitani bila kutaka, lakini vile vile tunawashukuru sana Wananchi wa Uganda. Baadhi ya Wananchi wa Uganda, walipigana bega kwa bega na majeshi yetu, kuanzia Tanzania mpaka ndani kwao Uganda na tunaambiwa vipi kwa lengo gani kumuua Iddi Amini, lakini tunaambiwa Wananchi wa Uganda, waliwapokea kwa shangwe askari wetu wa Tanzania walipoingia Uganda. Wananchi wa Uganda waliyasaidia sana Majeshi wakati wa vita hivyo.

Mheshimiwa Spika, hii niliiangalia katika kumbukumbu za vita vya Uganda kupitia TVT siku ya tarehe 29 Agosti, 2004, kipindi kilichorushwa saa nne ya usiku. Sio kwamba, labda tunafanya tu, tuangalieni vipi wenzetu wamefanya, walikuwa wanaonesha kumbukumbu ya vita vile vya Uganda. Sasa kama wenzetu wa Uganda waliwapokea majeshi yetu, inakuwaje sisi Watanzania tunadhalilisha wanajeshi wetu, si vizuri, ni vizuri tukaiangalia Katiba yetu. Wanajeshi wanafanya majukumu haya kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndio tuliowapa sisi na nina uhakika imetungwa na imepitishwa hapa na Bunge letu la Jamhuri la Muungano wa Tanzania. Hakuna mwananchi hata mmoja anayeweza kusema hakuna kauli yake katika Katiba ile, kwa sababu Katiba inapitishwa na Bunge letu hili la Jamhuri la Muungano wa Tanzania.

Hakuna mwananchi hata mmoja kijijini au eneo lolote ambaye hana mwakilishi wake katika Bunge hili, tukiamua humu tunaamua kwa niaba ya Wananchi wa Tanzania.

Kwa hiyo, ni vizuri wanasiasa wasijaribu kujenga mazingira ambayo wataliingiza jeshi hilo katika matatizo, waliache lipumzike, tujenge uchumi wa Wananchi na wale wanasema maneno ya uzushi kwamba, nchi haina maendeleo, sio kweli. Kuanzia mwaka 1980 mpaka leo 2005, ni miaka 25 uchumi uko hivi. Kuanzia tulipopata uhuru 1961 mpaka mwaka 1980 tunapigana na Uganda na mpaka mwaka 1970 hatujatoa majeshi yetu Uganda, tumepigana na Shizenzi, Namibia, Zimbabwe na maeneo mengi ya Afrika, hawa wasomi wayaone haya, tunajisikia vibaya kwamba, hata historia hawaitaki, hata zile kumbukumbu hawazitaki. Ni vizuri tukawa wa kweli, tukaacha ubinafsi tukajenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie, nataka nikuthibitishie kwamba, Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, ilitembelea karibu mipaka yote ya nchi yetu na nchi jirani. Isipokuwa mpaka mmoja tu wa Mkoa wa Ruvuma na hii kutoka na muda ambao haukuwepo, na madhumuni ya ziara yetu ilikuwa ni kutembelea mipaka yetu ya nchi, kutaka kuona hali halisi ya ulinzi na usalama wa mipaka yetu iko katika hali gani na pia kuangalia ni matatizo gani yaliyoko huku katika mipaka yetu hasa askari wetu walioko mipakani wakiwa wanalinda amani na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nilithibitishie Bunge lako Tukufu na Watanzania wote ambao wanafuatilia Bunge hili, wanajeshi wetu walioko mipakani wanafanya kazi kubwa, ambayo nina uhakika hata Marekani na Iraq, hawawezi kuifanya. Nataka nikiri hilo, wanajeshi wetu wanafanya kazi kubwa katika mazingira magumu. Niiombe sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iiongezee fedha Wizara hii na vifaa ili vijana wetu watekeleze majukumu huku ndani, tuweze kujenga uchumi, hivyo hilo ni moja ambalo nataka nilizungumze hivyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni juu ya masuala ya kuwatupia lawama wanajeshi wetu na mimi nataka niiombe Serikali, iweke adhabu kali kwa wale madreva wanaomiliki vyombo vya usafiri kama Daladala na vyombo vingine, watakaothubutu kuwadhalilisha wanajeshi eti kwa sababu tu wameomba *lift,* sio kuomba *lift,* wanaendesha uchumi wa nchi hii kwa usalama walionao. Kwa hiyo, ni vizuri kuwasaidia askari wetu pale panapokuwa na matatizo sio kuwadhalilisha. Lingine ninalotaka nilizungumzie ni juu ya kuipongeza Serikali yetu na Wizara yote kwa ujumla, kwa kuyahamisha yale mabaki ya wanajeshi waliopigana vita waliofia Msumbiji na baadhi ya nchi nyingine. Kwa bahati nzuri kule Mtwara tulitembelea eneo hili na kwa kweli Serikali imefanya jambo moja kubwa sana, ambalo kwa kweli halina mfano kabisa. Ni vizuri tuipongeze Serikali na tuwapongeze wenzetu wa jeshi kwa kazi hii kubwa waliyoifanya ya tangu miaka ya 70 na kuweza kurudisha miili ile.

Naiomba Serikali ihakikishe kwamba, barabara zote za ulinzi inazitengeneza na iziondoe katika Halmashauri iziweke katika Serikali Kuu. Kwa sababu katika baadhi ya maeneo tuliyotembea kama Mtwara, tunaambiwa barabara za ulinzi fedha, zinazotengwa ni shilingi milioni 80, hazitoshelezi na bahati nzuri kama hii barabara ya Mtwara ni kama

kilometa 330. Ni vizuri Serikali ikatengeneza barabara hizi kwa mafanikio makubwa, lakini vilevile naiomba Serikali iwapongeze sana ndugu zetu wa Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, mpaka wetu wa Tanzania na Msumbiji uko shwari sana na kutokana na hali hii, lazima tuombe wenzetu wa *DRC,* Burundi na Rwanda, wawe makini na waweze kufuata misingi kama ambayo wamefuata wenzetu hawa wa Msumbiji. Wote hawa ni ndugu zetu, si vizuri kuturudisha tena nyuma, kutuingiza katika vita kama tulivyoingia na Uganda. Tunataka kujenga uchumi wa nchi yetu, hatuna muda sasa hivi wa kulumbana na ndugu zetu hawa.

Mheshimiwa Spika, nataka niliombe jeshi na Serikali kwa ujumla, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia juu ya mipaka ya maeneo ya majeshi. Sasa nataka nizungumzie hili eneo moja la *Umoja Camp,* iliyoko Mtwara. Tunaona kwamba, eneo hili Wizara iliwahi kutuma wataalamu kwenda kupima na tunaambiwa sehemu kubwa ya eneo hili, imeingia katika bahari, kwa hiyo, wanaomba ramani ile ipitiwe tena upya ili ifanyiwe marekebisho. Halafu nataka niipongeze Serikali kwa juhudi zake za kutatua matatizo ya makazi ya wanajeshi katika ujenzi wa nyumba. Lakini kule Mtwara tulielezwa kwamba, kuna matatizo ya nyumba 150, naomba Serikali itoe fedha mara moja ipeleke JKT ikafanye *operation* mara moja ili kuondoa matatizo yale. Tukiangalia wenzetu wa Kusini, kwa miaka mingi walikuwa katika vita, ni lazima sasa hivi wakae mahali pazuri na niwaombe Wizara iilazimishe Wizara ya Ardhi, kwa kutumia wataalam wake Wizarani, iweke mipaka ya uhakika. Ule mpaka wetu wa Msumbiji na Tanzania, ile miti tuna wasiwasi kwamba, labda kuna siku itakuja malizika, itaondoa ule mpaka. Hatujui baadaye atatawala nani na dunia inabadilika hivyo, hilo lingine ningeliomba.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nikupongeze wewe binafsi, tukiwa shuleni, jina lako tulikuwa tunalisikia muda mrefu sana katika maeneo tofauti, katika Bunge katika Serikali, katika Chama, lakini Mwenyezi Mungu, ametujalia kwenye miaka mitano hii, kufanya kazi na wewe ni mwadilifu mkubwa sana. Tunachokuomba, usiache kuchukua nafasi ya Ubunge katika uchaguzi unaokuja, Bunge jipya lazima ulianze wewe, uwape baraka tena Watanzania. Wewe na Mheshimiwa John Malecela, sijui niwazungumzie vipi, nimefarijika kwa dhati kabisa. Binafsi wewe umefika Pemba, umefika jimboni kwetu, mchango wako kituo cha afya upo, hatutokusahau maisha na umethibitisha Utanzania kwamba, Pemba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini vile vile ulitoa elimu ya uraia katika mashule mbalimbali, ambayo nataka nithibitishe kwamba, haiko hata hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Wizara hii ambayo kwa kweli ni mwakilishi wa wanajeshi, karibu *one third* ya jimbo langu kuna vikosi mbalimbali na nyeti. Nimefurahia sana kupata nafasi hii, ila kitu kimoja nimechemsha kweli, kwa sababu kumbe jeshi liko mbali kuliko mimi, nilivaa nguo hizi nilidhani basi nitakuwa sawasawa, nilivaa sare na yule kamanda wa kikosi cha jeshi la *Jet fighters,* nikakuta wana rangi nyingine kabisa, yaani

zinamelemeta kuliko hii. Kwa hiyo, nilipanga niliwaambia jioni waandae suti inayofanana na yake, lakini hata hivyo, maneno yangu yatafanana na ninyi ambao mlikuwa kama wanajeshi, sio askari, lakini ni askari wa akiba, Namba yangu ni F.2415, kikosi maalumu cha Mafinga JKT, naitwa *volunteer assistant guard,* sina nyota nina mwezi asante. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa historia tu ni kwamba, ukiambiwa *summary* ya hotuba ya Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, nikwambie kwamba, wakati mmoja nilimpa masharti magumu ili afanikiwe, nilimwambia lete nyoka mwenye matege akaniambia hana miguu, nikamwambia nyoka feki, akasema haiwezekani. Sasa matokeo ni rafiki yangu mzuri, tumetoka mbali na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, wakati akiwa Muhimbili, kwa wale wanaomkumbuka, wakati huo nilikuwa mkemia wa Serikali. Sasa mambo yetu yalikuwa hivyo, tukafuatana hapa, bahati nzuri tukakutana tena, mambo yake hivi hivi, yaani mara nyingi sana. Sikupigii debe, huo ni ukweli wenyewe, ingawa kuna watu watakasirika tu, wanawania jimbo lako. Lakini wale ni kwamba, ni demokrasia tu, lakini Wananchi wameona kwamba, wewe ni dhahabu katika jimbo lile, ulikuwa utangulizi mzuri tu. Uki-*summarize* hii, naiona kama hali ya Jeshi letu la Kujenga Taifa inasonga mbele, *summary* tu ya ile hotuba yake.

Huduma za jamii ndani ya jeshi lenyewe na familia zao zinaimarishwa. Familia za mwanajeshi sasa zinafanya maeneo ya kambi ni sehemu ya maisha yao, sio kambi wanangoja kusubiri kwenda kuishi baadaye, pale ni eneo lao la kufanyia kazi na maeneo ya kuishi, kwa hiyo, zile ni kambi lakini ni kambi makazi.

Uzalishaji mali, nimeona miradi imekwenda mbali sana, kwa mfano, Nyumbu, natoa mapendekezo nikiwa kama ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji, naomba Waziri awasiliane na Waziri wa Viwanda na Biashara, tulimwomba sehemu ile inatengeneza maskania na *valment* pale Kibaha ili Nyumbu sasa waanze kutoa vitu, wasitoe *models* ya maonesho. Walianza nanyi ili mpatiwe watu ili kituo cha *EPZ* mpate mbia kutoka nje mkatengeneze magari yetu pale na tulishaongea na Waziri wa Viwanda, huenda akawakubalieni, tutapiga debe.

Lingine kampuni za majeshi yetu kwa kweli ziimarike na nimeona dalili kwa mfano, nyumba za kwao zinajengwa, madaraja yamejengwa na barabara zinatengenezwa. Uimarishaji wa Kambi za JKT, michezo ndio hakuna tena, kuna timu zangu *super mkong'oto* ilifungwa vibaya sana juzi na timu ya Kizuka, ilifungwa kwa tabu sana magoli sita kwa bila. *(Kicheko)*

Tuna jeshi la kisasa lenye teknolojia ya kisasa, pili ni uvumilivu au vilevile na kujiamini na kuwa na moyo wa haiba ya kuja wenzako tofauti na wale waroho watatu. Waroho watatu siku moja walikuwa wameokota shilingi milioni tatu, wakaamua shilingi milioni tatu zile, baada ya kugawana shilingi milioni moja, ikaanza mizengwe ikazunguka wakasema hapa tumtume mwenzetu akanunue *chips* tule halafu ndio tugawane. Shetani akaanza kuwaingia. Wakamtuma mwenzao kununua *chips,* wa *chips* akamwingia shetani akasema nitakula huku huku halafu nitachanganya sumu wale wakifa nachukua zote. Wale nao wawili wakaanza mizengwe yao wakasema mimi akija yule

bwana tumuue tule *chips* halafu tugawane shilingi milioni moja na laki tano. Mizengwe ilizunguka shetani katembea akashinda, bwana kanunua *chips* akala kule kachanganya na dawa ya panya kuja kwa wenzake, kapigwa panga akafa. Wale wawili wakasema tule *chips* halafu tugawane, wakala wakafa, wakaziacha shilingi milioni tatu pale pale kwa sababu ya uroho na uroho huu ulijitokeza kwa sababu jeshi letu linajitegemea kwa sababu ni wavumilivu na vile vile wastahimilivu, wanagawa kilichopo kwa Wananchi na raia. *(Kicheko)*

Hata zahanati zao pale Kidugalo na maeneo yanayozunguka, Wananchi wote wa maeneo yale wanatumia Zahanati zao na wanatumia sekondari zao, kwa hiyo, moyo huu ni mzuri sana na ndio maana kwa wavumilivu Mungu atawapa tu. Kwa sababu uvumilivu umemsababishia mbuzi kupata mkia mfupi, walipangwa foleni wanyama wote, Mungu alitaka awagawie mikia, akawaambia mpate mikia, mbuzi hatulii katika nchi, ukienda katika kijiji mnyama wa kwanza kumkamata ni mbuzi tu, akapiga kelele mbele ya Mungu, akamwambia nani anapiga kelele akasema mbuzi huyo, akamwambia aje kapewa mkia wake mapema ili aondoke. Waliotulia simba na wengine, walipata mikia mirefu. Jeshi letu limetulia mtapata mikia mirefu, hongereni sana. *(Makofi)*

Hoja iliyoko mbele yetu ilikuwa kwamba, tukubali Bunge lipitishe Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 2005/2006, nimekubali kwa kweli imeshapita hii tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umenipa nafasi nyingi sana katika Bunge hili, umefanya nchi nzima inanifahamu. Wanasema kuna mbunge mmoja hivi, ana macho kama anachagua mchele hivi, ametulia anaitwa Semindu Pawa, ndio mimi hapa. Umenifanya kwa kweli natoa taarifa kwenye *internet* na kwenye kompyuta ambayo wanaendelea kufanya, umenipa nafasi 104 za kuchangia, hii hotuba ya 105 katika miaka kumi ya jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki. Umenipa nafasi ya kuuliza maswali karibu 160 na maswali ya nyongeza 339, Wizara hii nimechangia mara 12 na hii ni mara ya 13.

Kwa hiyo, mara nyingi napenda kuchangia ili nijiweke na mimi katika historia. Nawaambia kabisa makamanda kwamba, kuna vitu vinaliwa ambavyo havishibwi. Kitu ambacho kinaliwa hakishibwi ni kiapo, kitu ambacho kinapigwa hakiumi ni kura, kitu kinachovunjwa ambacho hakivunjiki ni moyo, unavunja moyo, kitu ambacho kinakata lakini hakikatiki ni tamaa. Kwa hiyo, vitu hivyo vyote ambavyo vipo duniani lakini haviumi sana, Makamanda nimefurahi sana, nimesikia wamekuweka wa kwanza Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, anajituma, yupo makini, anachinchanganya na watu wote wa kanda zote. Vilevile ameongeza bajeti yake kwa zaidi ya asilimia mia 300, huduma mbalimbali zimetolewa kwa uzalendo wake. Kwa hiyo, wanajeshi na hii inatokana na *Commander in Chief,* aliyepo hivi sasa, pamoja na waliotangulia na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Usalama ya Tanzania na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, amemuweka Mungu mbele, humu hataki kubaki nyuma na Mungu atapitishia kwake ili jamii ifaidike pamoja na majeshi ya nchi hii. *(Makofi)*

Wakati unajifunza mambo mengi, kuna mambo kama *limit of method of destruction,* mambo ya *distinguishing, converting* na *distinguishing* kati ya mwanajeshi na raia, *prisoners of war, self help* na *self confidence.* Vitu vingi mnajifunza, mimi pia nilijifunza lakini nimeamua tu sasa hivi nimeingia kwenye siasa.

Wananchi mbalimbali mnazipata huduma vikosini, hebu kwa wale wanaoishi karibu na vikosi hivi, tumieni vizuri vikosi hivyo kama ni mwenzenu, ili mshirikiane nao kama Wananchi wa kule Ngerengere, Ilugalo, Kinonko, Kwataujembe. Huduma ya wanajeshi sasa hivi, kwa mfano, wanapata mikopo, kuna maduka ambayo yamo ndani ya jeshi lile, kuna kila bidhaa ziko kule, halafu vilevile ukiona wanajeshi wanavyovaa sasa hivi, *they are smart.* Kwa hiyo, wanatoka *smart* kabisa, zamani wanajeshi walikuwa ovyo ovyo tu, lakini wako *smart* kweli. Ukiona dalili ya kwamba, wanajeshi hawa wamefanikiwa na angalau hali ya maisha yao inakuwa nzuri, angalia vijiji ambavyo viko karibu na Kambi hizo. Hapa Ihumwa angalia zile *blocks* za nyumba zilizoko pale, siyo nyingi, za raia asilimia 60, ni wanajeshi wastaafu. *(Makofi)*

Ukikuta kwa mfano, pale Kwataujembe - Ngerengere, ni vijana wa Kinonko wale, ukiona pale Ngerengere sehemu za Kipera, maeneo mengine ya kule Mgudeni na Ngerengere Sinyaulimi, majengo mengi sana ya wanajeshi wale, wanajeshi wa vikosi vya Sangasanga na Kizuka, wameamua tu kubaki na raia wao pale pale. Ukiangalia majengo ya kule Pangawe maeneo yale na hivyo hivyo Tanzania kote hebu angalieni, hayo ndio mafanikio ya kuliendeleza jeshi letu nchini. Pamoja na mapigano, lakini vilevile ni wale wale, sio kukaa kwa ajili ya kupigana tu, ndio maana linaathiri na miba, lakini halipigani kila wakati kwa ajili ya kujilinda, lakini linalindwa na binadamu vilevile ili lisiibiwe. Jeshi letu lina miba, linatulia wakati ambao litakuwa halitulii lakini likichokozwa wataipata, limetulia sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuna huduma mbalimbali amezitaja Mheshimiwa Waziri, kwa mfano, huduma ya maji maeneo ya Pangawe, Ngerengere na Kinonko, niliandika barua kwenda kwa Waziri wa Maji, lakini ninashukuru sana barua ile imepelekwa kwako na unaiangalia kwa makini sana. Tulikuwa na ujumbe wa *Colonel* Kitenga, *X - Colonel* Mfinanga na Bwana Mwangoka, wa kutoka *World Vision,* tulikuja kumwona Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa ajili ya kuunganisha Mradi wa Chalinze. Wanajeshi wako tayari kujitolea kutumia mitambo yao kuchimba mitaro, hakuna hata senti tano pale, ni nguvu kazi zinatumika na wako tayari. Kwa hiyo, wanaomba muwe na mawasiliano na Mbunge wa Chalinze, pamoja na mimi ili kuufikisha Mradi ule katika vikosi vya Ngerengere.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu barabara. Kuna barabara moja imerukwa kinyemela, inaitwa barabara ya Ubena inaenda Tununguo mpaka Kiganenda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Kwa bahati mbaya imerukwa Jimbo la Chalinze, wakaruka Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, ikaenda kuanzia Jimbo la Kusini. Tulichokifanya nikaamua kutumia Wananchi wale kama 300, wakajitolea kuchimba, wanajeshi sasa hivi mbioni wanachimba kwa mikono yao. Kwa hiyo, ningeomba lile daraja la pale silaha, ndio silaha, siyo daraja mpaka chini, naomba tafadhali na lile daraja la Ubena linaleta sura mbaya sana kisiasa. Lile daraja ni la jeshi

vilevile linasaidia hasa viongozi wanapokwenda Ngerengere watumie lile daraja kwa ajili ya kusaidia. *(Makofi)*

Waziri wa Ujenzi na Naibu Waziri, nimeongea nao mara nyingi sana lakini wamelikwepa ili kupata lawama, hakuna lawama, tarehe 4 naomba mniulize kwenye Mkutano Mkuu ule wa Jimbo, nitatoa jibu hili hili kwamba, lile daraja lisije likanifanya mimi nikakosa kura kule. Kura wananipa kwa sababu ya mambo niliyoyafanya katika Jimbo lile. Hivyo hivyo kwa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Jimbo lako ni kwamba, kama kulamba karata wamelamba dume, kwa kweli kule Rorya wala hakuna matatizo yoyote na kila Mbunge anaposimama anakusifu, najua kuna wachache sana wanachukia, inawauma.

Lakini kama inawauma kwa kweli wakereketwao shauri yao, wewe utapiga mambo yatakuwa mazuri na Spika wetu atarudi tutakuwa naye. Mheshimiwa John Malecela, tunakuomba uwepo na wewe, kwa sababu shamba haliwezi kukosa visiki, ukilima shamba ukikosa visiki maana yake ni kiwanja cha mpira. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana maombi niliyoyaomba yafikishiwe. Tatizo lingine ni kuwa *careful* katika mambo ya kuwa na haiba ya moyo. Kuna tukio moja lilitokea kule Iringa, ambapo watu walikuwa na sherehe kubwa, waliokota uyoga pori ule mzuri sana, wakaleta pale wakachanganya na ng'ombe watano, baba anaoa. Basi wakajaa watu karibuni 2,000 pale, honi, matarumbeta, viazi vikachanganywa, supu ikatengenezwa, kabla hawajala taarifa ya habari, Mkemia Mkuu wa Serikali ameonya kwamba, uyoga una sumu kwa hiyo, watu 12 wamekufa kule Rukwa na watu wanane wamekufa Iringa. Kwa hiyo, uyoga una sumu kali sana. Kumwaga ni hasara kwa sababu wamechanganya na wale ng'ombe wanane, sasa kulikuwa na mtaalamu mmoja pale, akawaambia hapana toeni mpeni mbwa ale kwanza, halafu tumwangalie kwa sababu sumu za uyoga zinachukua dakika 10 tu anakufa. Wakampa mbwa akala dakaki 1, 10, 20 mbwa hakufa, wakasema tuingie twende tukale, ila wakamuacha kijana mmoja aangalie kama mbwa atakufa aje kutoa taarifa. *(Kicheko)*

Baada ya kufanya hivi, matokeo ni kwamba, wakakaa, wakaendelea kula tu *iyena iyena* na nini, baada ya muda kijana akaja wameshakula tayari, mbwa kafa baba. Wale bila kumwuliza kijana kafa namna gani, wakaamua kwenda hospitali kutapishwa. Kumbe kilichotokea, pale alipokaa mbwa gari ilikuja kupaki ikamkanyaga, alikufa kwa kugongwa na gari. Kwa hiyo, viongozi tuwe makini, tuulize, walikwenda kutapishwa bure chakula chao, yule aligongwa na gari hakufa kwa sumu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na sababu nzuri sana ya kumpanga Mheshimiwa Semindu Pawa, awe msemaji wa mwisho kwa asubuhi hii.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapa pole wale wote waliofikwa na misiba humu Bungeni na nje pia. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi watarajiwa wote kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi kwa kupata uteuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Jimbo langu la Baraza la Wawakilishi nitangulie kwa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Niendelee kwa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa umahiri wake wa kuiongoza Wizara hii. Vile vile niwapongeze watendaji wa Wizara hii kwa ushirikiano wa karibu wanaompa Mheshimiwa Waziri na hatimaye tuna Jeshi lenye kulinda na kudumisha amani nchini na mipakani.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwenye hoja hii ni mmoja tu, nao unawagusa askari au wanajeshi wastaafu na hili linahusu mafao yao *(pension).* Mwanzo askari hawa walikuwa wakipata *cheque* za *TRA.* Hivi sasa wanalipwa kupitia *sheets* za Hazina na hili hufanyika kila baada ya miezi sita. Lakini la kusikitisha ni kwamba muda huo hivi sasa huwa unapindukia miezi sita. Kwa kweli kwa hili askari wastaafu wanahisi wametupwa. Wanaloomba askari kupitia sisi wawakilishi wao ni kwamba kutokana na ukali wa maisha wanaokabiliana nao, muda wa kupata mafao yao upunguzwe pamoja na hivyo basi Wizara ijitahidi pensheni zipatikane kwa wakati. Hili tumekuwa tunalipata kutoka takribani kwa kila askari mstaafu unayekutana nae.

Mheshimiwa Spika, kwa umahiri alionao Mheshimiwa Waziri pamoja na muda mdogo uliobaki ni imani yetu, hili liko katika uwezo wake na atalifanyia kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia pamoja na kuunga mkono hoja hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa utendaji wake kwenye Wizara hii katika kipindi cha miaka mitano tunayomalizia. Pamoja na hivyo namtakia kila la kheri na fanaka katika kinyang'anyiro kinachotukabili sote kwa pamoja huko Majimboni. Bila shaka sote tutapita na CCM itashinda. Shukrani.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi zake nzuri anazofanya kwa uhakika na kujiamini katika mwaka wa fedha 2002/2003. Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi kwa Kituo cha Jeshi la Ulinzi Potoa *(Navy)* kilichopo Zanzibar. Moja ya hadi alizotoa ni kupeleka umeme hapo Kituoni, maji na mawasiliano (simu).

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutimiza moja ya ahadi zake kwa kukipatia Kituo hicho cha Potoa umeme wa uhakika ambao haukuwepo kwa muda wa miaka 30 iliyopita. Hivyo ninamshukuru sana kwa kuwajali Askari hao ambao wamekuwa wavumilivu kwa muda wote huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika ahadi zake ni mambo mawili tu yaliyobakia yaani maji ambayo bado ni tatizo sugu hapo Kituoni na askari hao bado wanapata taabu ya kuyafuata umbali wa kilometa 5 ikiwa ni pamoja na kukosa mawasiliano (simu) hapo Kituoni.

Mheshimiwa Spika, ni tegemeo la askari hao kuwa Serikali yao italichukulia hatua suala hilo haraka iwezekanavyo, kwani Kituo hicho ni muhimu sana hasa ukizingatia kuwa ni Kituo pekee cha *Navy*, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, namtakia kazi njema na mafanikio Mheshimiwa Waziri ili arejee tena Bungeni kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kupata fursa ya kutoa mchango wangu kwa maandishi. Pili, naomba kuchangia yafuatayo:-

Moja, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja watendaji wake wote waliokaa pamoja na kutengeneza hotuba hii muhimu.

Pili, naipongeza Serikali kupitia Wizara hii kuiweka hali ya ulinzi na usalama katika mipaka yetu kuwa shwari na salama.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba kupendekeza yafuatayo:-

(a) Wanajeshi wetu wanapokaribia kustaafu watayarishiwe mafao yao mapema ili kuondoa usumbufu wakati wa kustaafu unapowadia;

(b) Mikopo ya vifaa vya ujenzi wapatiwe wapiganaji wetu na wasimamiwe kuhakikisha kuwa wanajenga nyumba za kuishi ili watakapostaafu wasiaibike kimakazi;

(c ) Vifaa vya kisasa vya kiulinzi viboreshwe ili kuendana na hali ya kimaendeleo ya sayansi na teknolojia; na

(d) Kwa wale ambao tayari wamestaafu au kufariki na mafao yao bado kupatiwa ama wao au familia zao, basi Wizara ijitahidi kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa asilimia mia moja. Ninaomba niishie hapo. Ahsante.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, juzi nimetangaza kuwa sitagombea Ubunge katika Jimbo langu la Nachingwea mwaka huu 2005. Jimbo hilo nimeliongoza kwa miaka 30 mfululizo. Hivyo nachukua nafasi hii kwanza kuwashukuru wanajeshi wote na viongozi wote katika vikosi *(TPDF* na JKT) vya Nachingwea kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha miaka 30.

Mheshimiwa Spika, pili, nilipokuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mwaka 1995 hadi 2000 nilipata ushirikiano mkubwa sana na *CDF, General* Robert Mboma, makamanda wote na wapiganaji wote nchi nzima. Nilijifunza mengi kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu lina uvumilivu na nidhamu ya hali ya juu. Aidha, nilitembelea nchi mbalimbali na kuona mifumo yao ya Jeshi. Nilijifunza kuwa Jeshi letu lina ujuzi wa masuala ya kivita wa hali ya juu sana. Nawaasa *CDF General* George Waitara, Makamanda, Maofisa na Askari wote waendeleze nidhamu, ubunifu na upendo kwa Amiri Jeshi Mkuu aliyepo na wajao na kwa wananchi wanaowalinda. Aidha, waendelee kuweka mbele maslahi ya Taifa letu na wawe tayari wakati wote ikibidi kujitolea maisha yao katika kulinda mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, barabara iendayo Ngerengere ni mbaya sana. Aidha, daraja la barabara hiyo karibu na barabara Kuu ya Dar es Salaam –Morogoro limekatika kutokana na ubovu huo wa daraja na barabara yenyewe inakuwa vigumu kusafirisha mizigo nyeti na magari makubwa ya mafuta. Nashauri daraja hilo litengenezwe, barabara ipigwe greda na ifanyike mipango ya kuweka lami kwenye barabara hiyo.

**MHE. AISHA P. MAGINA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Phillemon Sarungi, pamoja na wataalam wake kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri juu ya nyumba kumi za Jeshi la Kujenga Taifa zilizopo Kibaha ambazo zimeharibika vibaya, hazifanyiwi matengenezo wala ukarabati. Kwa bahati nzuri uamuzi uliokuwa umetolewa ni kwamba nyumba hizo ziuzwe kwa Wanajeshi wanaoishi katika nyumba hizo, lakini kwa bahati mbaya hadi leo hii hakuna kinachoendelea. Wanajeshi hao hawajauziwa nyumba hizo na hawafahamu hatma ya nyumba hizo kumi. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi juu ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze kwa dhati Waziri, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja yake vizuri sana na kwa muda muafaka. Lakini pia nimpongeze Katibu Mkuu, Ndugu B. S. Mchomvu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George Waitara na Mnadhimu Mkuu, Luteni Jenerali Iddi Gahhu, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali David Mwamunyange, pamoja na Makamanda na wapiganaji wote. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanywa na Jeshi letu kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni imekuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa majirani zetu. Lakini bado kuna haja ya kuchunguza vizuri vijana wanaojiunga na majeshi yetu, wawe *properly veted.* Wakati huu wa ulimwengu usiokuwa na mipaka, tuwe waangalifu zaidi. Tuanze kuwachunguza kwenye mchujo unaotokana na JKT. Tuzingatie elimu nzuri, afya nzuri, ari na uadilifu wao. Tukitaka Jeshi letu liwe la kisasa na lenye mwelekeo wa karne hii ya Sayansi na Teknolojia, elimu ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Kikosi cha Uhandisi cha Jeshi letu, lakini bado ahadi za siku nyingi za kujenga barabara za mpakani mwa nchi yetu hazijapewa msukumo unaostahili kwa kuwa zimeachiwa Halmashauri za Wilaya ambazo nyingine hazijawahi kuhudumiwa. Nashauri Waziri azikague zote na ajenge hoja ya kuzitafutia fedha na kwa kutumia vikosi vyake vya ujenzi vifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa mawasiliano ya pekee kwa ajili ya Majeshi na Serikali kwa ujumla upewe umuhimu wa kipekee ili kuanzia kipindi hiki cha Uchaguzi Mkuu, mawasiliano yenye uhakika na wa kiusalama yaanze kutumika maana Mikoa, Wilaya na Makao Makuu yawe rahisi na mepesi. Kama tatizo ni fedha ziombwe Hazina kupitia kibali rasmi toka kwa Mheshimiwa Rais ili hoja hii ipelekwa kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, hivi mapendekezo ya awali kwa kiwanda chetu cha Nyumbu na mshirika wao wa awali toka Ireland wa kutengeneza *jointly* magari ya zimamoto yaliishia wapi? Mbona Nyumbu inataka iache nafasi hii muhimu kwa biashara kubwa kama hiyo ambayo ingefaa kwa nchi nyingi za Afrika? Mfano gari moja lina gharama ya zaidi ya shilingi milioni 300 na kuendelea. Wilaya zetu 112 pekee, fedha zake zingeweza kurejesha hata mkopo wa kujenga kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, JKT nayo ikipewe msaada wa zana na vifaa vya kufanyia kazi, wangeweza kufanya maajabu katika nchi hii. Ipo haja kwa Serikali yetu kuendelea na mpango wake wa kuimarisha JKT kuingia ubia na makampuni mbalimbali yaliyopo hapa na hata nje ya nchi. Viwanda navyo vingesaidia kutoa ajira kwa vijana wa JKT.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine ni kuanza kuomba maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya matarajio ya baadaye, ardhi, viwanja, misitu na hata maeneo ya uwindaji, wawe *jointly* na wawekezaji wa nje. Tutumie nafasi hii ya mazingira mazuri ya kiuchumi kuandaa mpango wa miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote na kumtakia Mheshimiwa Waziri ushindi kwenye Jimbo lake.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba nzuri na kazi nzuri sana inayofanywa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati fulani nikiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1970/1971, wanafunzi tulikuwa tunapelekwa Kunduchi kufanya mazoezi ya kijeshi kama kupiga *range* na kutembea kijeshi kwa umbali mkubwa. Mazoezi kama haya yalikuwa yanafanyika kwa muda maalum kwa kipindi katika muhula maalum. Manufaa yake kwa wanafunzi na kwa umoja na uimara wa nchi yalikuwa mengi. Wanfuanzi waliji-*identify* na wajibu wao wa ulinzi wa nchi yao. Walijiona ni sehemu ya ulinzi huo. Walijivunia nchi yao na waliona *pride* kuilinda. Umoja kati ya wanafunzi uliimarika na kujiona kama Taifa moja.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa vizuri kuona ni vipi wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu zingeweza kurudia mazoezi ya kijeshi kama ilivyokuwa zamani za miaka ya 1970.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukupongeza wewe binafsi kwa jitihada zako za kuliendesha Bunge hili kwa umakini, umahiri na busara za hali ya juu katika chombo kikubwa kama hiki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na watendaji wao wote kwa kuwasilisha bajeti yao yenye matumaini na moyo wa ari kwa askari wetu ambao ndiyo tegemeo letu kwa ulinzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, tunayo kila sababu ya kuupongeza uongozi wote wa Jeshi hili kwa utaratibu mzuri walionao wa kuwaeleza Askari wao kujua thamani yao katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu ni Jeshi lenye uchungu wa nchi hii, ndiyo maana wako karibu sana na wananchi katika kufanikisha yale yote yanayowagusa wananchi kama kero kwani ni dhahiri kuwa Jeshi letu linashiriki kwa namna moja au nyingine ili kuhakikisha kero kuu zinaondoka tena kwa gharama nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda niiombe Wizara baada ya jitihada zote hizo sasa Jeshi letu limebakiza kazi moja ambayo naamini wakiivalia njuga basi litaondoka mara moja, nayo ni kupambana na majambazi. Ukweli ni jambo la aibu kuwa Tanzania yetu ina uafadhali mchana, usiku ndiyo hatari zaidi kuwa huna uhuru wa kufanya lolote kwa kuwaogopa majambazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulipongeza Jeshi letu hili kwa kutoa huduma za afya za hali ya juu kabisa bila ya ubaguzi wowote kwa wananchi wote na kuzifanya hospitali zao watu kuzipenda zaidi kutokana na huduma nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, napenda kuunga mkono hoja hii.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa mara nyingine hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama, ni ya kujivunia.

Nampongeza kwa dhati Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Phillemon Sarungi, Mkuu wa Majeshi, Jenerali George Waitara, Katibu Mkuu na Makamanda na wapiganaji wote.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, hasa vijana na kwa niaba yangu binafsi, tunaishukuru Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa uamuzi wa kuanzisha Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa Muleba eneo la Burigi. Tunasubiri kwa hamu kubwa uanzishwaji huo. Tutaendelea kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga hasa Mheshimiwa Waziri na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la Askari wa Kikosi cha Jeshi la Ulinzi Songea kuvamia stendi ya basi na kuharibu magari ya raia. Wananchi waliofikwa na mkasa huo wanaomba wapewe maelezo ni hatua zipi wahalifu hao wamechukuliwa? Ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao ambao magari yao yaliharibiwa katika tukio hilo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa utekelezaji wa ahadi yake ya mabati ya kuezekea Hospitali ya Kikosi cha 71 Welezo. Wapiganaji wa kikosi cha 71 wanakushukuru na kukupongeza ingawa ahadi hiyo imechelewa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi wa kiraia Jeshini, kuna matatizo ya upatikanaji wa wafanyakazi wa kiraia wanaofanya kazi Jeshini (Zanzibar) hasa

wanapofariki. Warithi wao wanasumbuliwa wakati wanapofuatilia mafao ya Marehemu kwani hulazimika kuja makao Makuu Dar es Salaam na hali wengine ni wageni na nauli wanajigharamia wenyewe. Aidha, malipo ya Marehemu hao yanachukua muda mrefu sana, jambo ambalo linawakatisha tamaa warithi wa Marehemu na kulazimika kuacha kufuatilia tena.

Hali hiyo inatisha na inasikitisha kwani Idara ya utumishi Jeshini MMJ haisaidii upatikanaji wa mafao na malipo ya Marehemu hao jambo ambalo linajenga dhana ya kuwa pesa za Marehemu hao zinaliwa. Mfano halisi wa Marehemu Asha Ame Makame, aliyekuwa akifanyakazi Jeshini *(Civilian)* ambaye alikuwa mke wangu amefariki mapema mwaka 2002 na mpaka leo pamoja na kufuatilia haki zake, Jeshi bado halijaonyesha nia ya kulipa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanajeshi wanaostaafu. Usumbufu wanaoupata askari wanapostaafu na muda mkubwa wanaokaa bila ya kulipwa unawalazimisha askari hao kugawana kipato chao na watu wengine ambao huwafanyia mipango ya kupata kiinua mgongo chao lakini kwa masharti ya watu hao kukatiwa kitu kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya watu Zanzibar ambao walikuwa wanajeshi (wastaafu) wenye vyeo vya juu na wengine askari wa kawaida lakini wana mahusiano mazuri na maafisa wa MMJ wanaoshughulikia mishahara na pensheni. Watu hao ambao ni *middlemen* ndio huwafanyia mipango wanajeshi wa Zanzibar kupata kiinua mgongo chao mapema baada ya kukubali kukatwa sehemu ya malipo yao ya kiinua mgongo chao na maafisa hao hugawana na hao watu wanaofanya mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo Mheshimiwa Waziri, naomba uijue na ni hali halisi inayotumika Zanzibar, askari hapati kiinua mgongo mpaka apitie kwa mtu huyo ili atoe chochote.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu si mzuri na wala hamuwatendei haki wanajeshi hao hasa baada ya utumishi wao wa muda mrefu. Haifai Jeshi kutumiwa na masuala ya rushwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Katibu Mkuu na watalaam kwa hotuba nzuri na kamilifu ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nyingi zinazofanywa na Wizara kuboresha utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali bado sijapata maelezo kwa nini wahitimu wa mafunzo ya mgambo hawajapata vyeti vya kuhitimu mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia kwenye hotuba za Bajeti ya Ulinzi karibu kila mwaka lini vyeti vya mafunzo ya mgambo vitatolewa kwa wahitimu, majibu yalikuwa baada ya Bajeti lakini hadi leo wananchi wa Wilaya ya Liwale Jimboni kwangu waliohitimu mafunzo ya mgambo hawapati vyeti hivyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri

wakati wa majumuisho yake aeleze lini wahitimu wa mgambo Wilaya ya Liwale watapewa vyeti hivyo. Kwa vile mimi ndiye niliyoanza kufuatilia kwa karibu sana vyeti hivyo kwa niaba ya wananchi wa Liwale ningetegemea wahitimu wa mgambo Liwale kupewa kipaumbele kupata vyeti hivyo. Hii imekuwa kero kubwa kwa wahitimu hao.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi endapo leo atatamka rasmi lini wahitimu wa mgambo Wilaya ya Liwale wapatao zaidi ya 500 watapata vyeti hivyo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono tena hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWANAIDI HASSAN MAKAME:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Makamanda wote wa JWTZ na JKT kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

(a) Wanajeshi wakopeshwe fedha ili wajenge nyumba zao wenyewe ili baada ya kuacha kazi waishi katika nyumba zao.

(b) Zijengwe nyumba za kutosha katika makambi yao ili wanajeshi waishi katika kambi kwa sababu kukaa uraiani kwa askari hawa huleta usumbufu kwa sababu wengine wanaishi mbali na vituo vyao vya kazi.

(c) Wapatiwe mikopo ya vyombo vya usafiri kama vile pikipiki na magari ili waweze kufuatilia shughuli zao hasa baada ya mapumziko, wafanyakazi hao wanahitaji kufanya kazi zao za binafsi.

(d) Vijana wanaoajiriwa katika Taasisi hii ni vizuri wachunguzwe vizuri imani zao, uzoefu, tabia na familia zao kujua msimamo wao, nasema hivi kwa sababu kazi hii ni muhimu sana hivyo si vizuri kuajiri vijana wasio na imani na nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Wizara hii, nasisitiza kuwa Serikali iipatie zana bora za kufanyia kazi ili imani yetu izidi kuendelea na imani ya nchi yetu ya Tanzania iwe na amani zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa juhudi za Wizara hii kuwezesha amani, usalama na heshima ya Taifa letu kuwa ni tabia ya kudumu.

Pili, nawapongeza sana katika kukiimarisha katika kuendeleza Taifa Kikosi cha ujenzi wa nyumba, barabara na madaraja. Naomba Serikali izidishe Bajeti kwa Wizara hii ili kuimarisha uhandisi wa kikosi chake cha ujenzi.

Aidha, wapewe kipaumbele katika ukandarasi wa utekelezaji wa miradi muhimu ya Serikali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Meremeta kipatiwe fedha za kutosha ili kiweze kununua vito mbalimbali na kuwapatia misaada na vifaa wachimbaji madini wadogo wadogo ili kuwaondoa katika kunyonywa na kudhulumiwa na wachimbaji wakubwa kutoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa uongozi wa Wizara kuwapatia sehemu ya shamba la Itaka liongeze kazi zake za uzalishaji ili shughuli za uzalishaji wa chakula uweze kusaidia makambi mengine hapa nchini. Eneo hili ni zuri sana kwa kilimo cha maharage, mahindi na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Aidha, mahali hapo pana chemchem yenye chanzo cha kuduma hata ujenzi wa bwawa na kuwezesha kufuga samaki.

Kwa kuwa teknolojia ya utafiti wa Shirika la Nyumba limeonyesha mafanikio makubwa, sasa Serikali ilipatie shirika hili mradi na kulitengea bajeti ili liweze kutengeneza magari ya majeshi mengine hapa nchini hakuna sababu ya kuagiza magari toka nje ya nchi wakati uwezo tunao. Nchi nyingi duniani zimejenga na kukuza viwanda vikubwa kupitia utaratibu huu wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya Jeshi la Mgambo bado nchi ina upungufu wa ulinzi vijijini iko haja na kuliunganisha Jeshi la Mgambo na Sungusungu ili kupata walinzi wa kutosha na kuwezesha ulinzi vijijini na kupambana na mauaji yanayodhalilisha Taifa vijijini.

Mheshimiwa Spika, iko haja ya kuenzi na kuzingatia kuwa dawa zinazotengenezwa na Jeshi letziyapewe umuhimu wa kwanza kutumika katika zahanati zetu na hospitali hapa nchini na wapatiwe nafasi kutangaza na mafunzo ili watu waweze kuyaelewa vizuri na kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mkuu wa Majeshi Jenerali, George Waitara, Makamanda wote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri na Katibu Mkuu, naipongeza JWTZ, Mkuu wao *CDF,* Mkuu wa JKT na Afande Gahhu na Makamanda wote mliopo ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya maisha ya wanajeshi, kujali wanajeshi na familia zao na kuwa wanapoishi siyo kambi ni makazi. Kama vile eneo la vita, wakati nchi tulivu makazi hayo ya kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa Askari, JWTZ iingie mkataba na vyombo vya fedha nchini ili kukopesha wanajeshi wa kawaida kukopa fedha za kujiendeleza kimaisha, nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya kambi JKT na JWTZ, pale ambapo wanajeshi au kambi ya JKT ipo wapewe ardhi wahakikishe mipaka ili kuishi bila ya migogoro na raia wao katika vijiji hivyo.

Maombi ni maji vikosini, barabara vikosini mfano daraja la Ubena na barabara ya Mdaula – Kidugala, Ubena hadi Ngerengere na Gwata hadi Kinonko.

Mheshimiwa Spika, nampa hongera sana Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, urudi.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi, Maafisa, Makamanda na Wanajeshi wote wa Jeshi letu la Wananchi Tanzania, kwa hotuba yake nzuri yenye mafanikio ya maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, natumia fursa hii kumpongeza sana sana Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama hapa nchini, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake uliojaa uadilifu mkubwa ambao pia umeviwezesha vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kuwa na maendeleo makubwa ya kifedha, kivifaa na kielimu kwa muda wote wa uongozi wake huo wa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri imeelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu imepata mafanikio makubwa katika kutekeleza majukumu ya ulinzi wa Taifa letu hili la Tanzania, ni ya kweli na kwa kweli yanastahili kupongezwa sana na kuungwa mkono na Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nikiri kuwa kwa kweli juhudi zimefanywa kuboresha huduma mbalimbali kwa wanajeshi wetu kwa hali ya juu sana. Huduma hizo ni pamoja na huduma za chakula, sare na huduma za tiba.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza sana sana juhudi hizi zilizofanywa na Serikali yetu hii ya Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na pia ninaiomba Serikali yetu hii kuiongezea fedha, vifaa na mambo mengine kwa Jeshi letu hili la Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile naiomba Serikali yetu kuongeza juhudi zake katika kujenga nyumba za kuishi wanajeshi wetu kama ambavyo hatua hizo za Serikali zilivyokwisha kuanza.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaeleza juu ya upimaji wa maeneo ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara hii ya Ulinzi kwa kulielezea suala hili la upimaji wa maeneo ya Jeshi, kwa kueleza kuwa, upimaji wa maeneo ya Jeshi ni zoezi lililopewa umuhimu wa juu katika mpango wa Serikali wa kuliimarisha Jeshi.

Mheshimiwa Spika, suala hili la maeneo ya Majeshi yetu ishughulikiwe ipasavyo na kwa haraka na ufanisi mzuri ili kuliwezesha Jeshi letu kuyamiliki maeneo yao kisheria na pia kuondoa migongano na baadhi ya wananchi wanaokaa na kuishi katika maeneo hayo yanayopakana na maeneo ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa kumi na nne, unaelezea juu ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka yetu ya Tanzania, utendaji Kijeshi na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa huu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inasema kuwa katika mwaka 2004/2005 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania liliendelea kutekeleza moja ya majukumu yake ni kulinda mipaka ya nchi yetu, watu wetu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sehemu hii ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ndiyo inayonipa kuiomba sana sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuliwezesha na kulijenga Jeshi letu hili katika kiwango cha kisasa kifedha na vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nchi yetu ni maskini lakini sura ya nchi yetu kiulinzi ni ya Kimataifa. Kwa hiyo, tujenge nguvu ya uchumi wa nchi yetu ili kuweka nchi yetu katika ramani ya dunia kuwa ni nchi yenye nguvu na uwezo kiuchumi na kiulinzi katika eneo lote la Bara letu la Afrika na duniani kwa ujumla. Kama tutajipanga vizuri tutafikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hoja hotuba hii asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mfenesini, tunatoa pole kwa wananchi waliofiwa na Wabunge wao katika kipindi hiki, Mungu awape subira na tuendelee kuwaombea wenzetu waliotangulia awape malazi mema. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Profesa Phillemon Sarungi kwa ushirikiano wake wa dhati na wa ukweli kwa Wabunge wote katika kipindi chote tangu apate uteuzi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri na uongozi wa Jeshi kwa msaada wao katika ukarabati wa hospitali ya Bububu ambayo ipo katika hatua nzuri, ila tu bado niombe atafutwe mfadhili ambaye atajenga upya hospitali hiyo ambayo ipo ufukweni katika Bahari ya Hindi ambayo naamini ikifika katika kiwango kizuri itasaidia pia kulaza hata viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuiombea Kambi ya Mwanyanya Mtoni, ifanyiwe utaratibu wa kufanya marekebisho ya njia yao katika kiwango cha kifusi hii itapelekea hata magari yao yatadumu ukilinganisha na hivi sasa ambayo barabara hiyo ina mashimo makubwa na mawe yasiyo na mpango.

Mheshimiwa Spika, lazima pia nichukue fursa hii kulipongeza Jeshi lote hasa Jenerali George Waitara, kwa uongozi wao mzuri katika utawala wa nidhamu ya hali ya juu kwa ni hivi sasa ni nadra sina kuwakuta wanajeshi wanazurura hovyo barabarani, hii inatuletea faraja sana kuona wanajeshi wetu muda wote wamekuwa na shughuli zao muhimu makambini.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza sana kikosi cha Ujenzi, kikosi ambacho kimeleta sifa sana kwa uaminifu katika mikataba ya ujenzi ambayo wamepewa na Wizara ya Ujenzi.

Lakini bado naomba Jeshi lizingatie kuboresha Kikosi cha *Field Engineering* ili nacho kiweze kupewa kazi za ujenzi wa barabara na madaraja hapa nchini kikosi ambacho ninaamini kina uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, bado napendekeza kikosi cha *Navy* Kigamboni wapatiwe Pantoni yao ndogo ambayo itakidhi mahitaji yao ambayo itaendana na harakati za kijeshi, badala ya hili Pantoni la kiraia ambalo ni la kusita sita.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza sana kwa hotuba yako nzuri yanye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia haya yafuatayo:-

Wakati umefika sasa wanajeshi wote wakae/wawekwe makambini. Serikali itenge fedha za kutosha kujenga nyumba za makambi ya wanajeshi wasikae uraiani. Hii itasaidia kujenga nidhamu ya wanajeshi wetu wanapokuwa pamoja makambini.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa wanajeshi uboreshwe vikosi vya Ihumwa na JKT Makutupora wapatiwe magari ya kutosha na vikosi vyote hapa nchini wapewe usafiri wa uhakika. Makambi ya JKT yaliyofungwa yafufuliwe ili kusaidia vijana wengi wanaomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari kujifunza ufundi na utaalamu mbalimbali wenyewe/ajira binafsi. Idadi ya vijana wanaojiunga na JKT iongezwe ili kuwapa mafunzo vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe wanajeshi wastaafu wanalipwa mapema bila usumbufu wowote kuliko hali ilivyo sasa kuna ucheleweshaji wa kulipa mafao ya wastaafu hao.Maslahi ya wanajeshi yaboreshwe. Wanafanya kazi katika mazingira magumu na pia kuboresha taaluma ya wanajeshi hasa kupata mafunzo ya kijeshi ya kisasa kulingana na karne ya 21 ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara hii. Ni hotuba nzuri inayowapa imani wananchi kwa nchi yao. Nawapongeza sana, nampongeza sana Mkuu wa Majeshi kwa kuongeza tena kwa kiwango cha juu nidhamu ya Jeshi letu. Vijana wengi wa Jeshi hili kuwa wanaridhishwa sana na uongozi wa Jenerali George Waitara kwa juhudi zake hizi. Hadhi ya Jeshi letu imepanda sana na ni matumaini yangu kuwa chini ya uongozi wake heshima hii itaendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kulipongeza Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri za kijamii zinazofanywa na wanajeshi hao. Kazi hizi zinawaweka wanajeshi kwa kweli wao ni wananchi wa Jeshi la Nchi hii na kwa maslahi ya wananchi wa nchi hii. Ni majeshi ya wanajeshi ambao sio tu wako tayari kufa kwa ajili ya nchi yao bali pia kuhakikisha ya kuwa wananchi wanapata muda wa amani kuendeleza nchi yao. Aidha ni wanajeshi watakaohakikisha kuwa adui wa nchi yetu atakufa kwa ajili ya nchi yake. Uimara wa Jeshi letu unatokana na uongozi mzuri wa kuwa karibu na majeshi yetu wa Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Benjamini William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba naupongeza sana uamuzi wa Serikali kupitia Wizara hii kuendeleza ukarabati wa Shirika la Mzinga

kwa manufaa ya nchi yetu. Uamuzi huu ni wa msingi sana kwa maendeleo ya amani dhidi ya adui wa nje na ndani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hospitali za Jeshi, binafsi nimepata huduma mbalimbali kwenye Hospitali ya Jeshi ya Lugalo, nimeridhishwa sana na huduma ya Jeshi letu. Ninaipongeza Wizara hii kwa huduma zake hizi za Afya kwa jamii, ninalipongeza Jeshi kwa kuipanua huduma hii na katika Mikoa mingine kama Mwanza na kwingineko nchini, napongeza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu JKT na Walimu, kwa vile walimu huwa wanasambazwa nchi nzima mijini na vijijini na kwa kuwa walimu wengi hukwepa kwenda vijijini kutokana na kukosa ukakamavu wa mwili na kiroho/kizalendo. Mimi ninashauri sana kuwa ili kijana apewe nafasi ya kujiunga na Chuo cha Ualimu awe amepitia mafunzo ya JKT angalau kwa kipindi cha miezi sita. Nasema hivyo kwa wale tu tuliopitia JKT kipindi cha nyuma hatukuwa tukilalamika tunapopangwa kwenda kufanya kazi mahali popote. Tulikuwa tukipikwa kishujaa, kimwili na kizalendo Jeshini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Shule za Sekondari za Makongo na Jitegemee zinasaidia sana sekta za elimu na michezo. Naomba Jeshi hili lifungue shule nyingi katika kanda na mikoa ili kuzipunguzia mzigo shule zilizo chini ya Jeshi la Ulinzi (Makongo na Jitegemee).

Mheshimiwa Spika, shughuli za kijeshi kufikishwa Wilayani, mafunzo ya kijeshi humpa mtu ukakamavu kujiamini na uvumilivu. Naunga mkono wazo hilo na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba naomba muda muafaka utakapofika, shughuli hizo kufikishwa Wilayani, Wilaya ya Kwimba nayo ifikiriwe ili vijana wa Kwimba nao wanufaike.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa wabunge, kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.51 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Niwashukuru waliochangia kwa kuzungumza na kulingana na utaratibu uliopo, wapo waliochangia kwa kuniandikia kwa vikaratasi kama ilivyo kawaida yetu hapa Bungeni. Wapo waliochangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na wapo waliochangia nje ya Bunge. Wote nawashukuru sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo uniruhusu kutoa ushuhuda wangu mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu sifa walizonipatia. Kama kuna kiongozi aliyenionyesha njia ya uongozi na aliyenitia moyo wakati nilipoanza kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiongozi huyo alikuwa Makamu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mheshimiwa Pius Msekwa, Spika wetu.

Baada ya kukata tamaa na mizengwe ya kitaaluma, ubaguzi wa kejeli kuhusu wahadhiri waliokuwa wamejenga hisia kuwa wao ndio wao bila wao hakuna Chuo Kikuu. Nilikasirika na nilikwenda Ofisini kwa *Vice Chancellor* na baada ya kujieleza alinipa ushauri ambao ndio umeniwezesha kufika hapa nilipo. Alisema bwana mdogo katika ulimwengu huu fanya uamuzi sahihi na utekeleze kwa uaminifu wako. Akaniambia kutofanya uamuzi ni dhambi, nenda utekeleze maamuzi yako na maamuzi ya Baraza la Chuo Kikuu bila kujali mtu yeyote awe Professa au *Chief Academic Officer* mimi nitakuwa upande wako. Kwangu hii ilikuwa ni kuhitimu Shahada ya Juu ya Uongozi. Kuanzia hapo nilizingatia ushauri wa *Vice Chancellor* wangu na sikurudi nyuma hadi leo hii. *Mr. Vice Chancellor, I salute you sir. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu sasa niwataje kwa majina waliochangia kwa kuzungumza. Kwanza kabisa kwa niaba ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Kudumu Ulinzi na Usalama ndugu yangu mpendwa, rafiki yangu Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, upande wa Upinzani rafiki yangu nataka nimpongeze sana kwa sababu ametuonyesha hakuna itikadi katika ulinzi na alifuta maandishi yote mengine yaliyoandikwa ya kutuvuruga. Tanzania sasa tumepevuka, tumekomaa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, Pemba, ndugu yangu Mheshimiwa Thomas Nyimbo - Mbunge wa Njombe Magharibi, Mheshimiwa Feteh Said Mgeni - Mbunge wa Bumbwini, Zanzibar, Mzee Ngwali Zubeir - Mbunge wa Nungwi, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud - Mbunge wa Mkanyageni, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka - Mbunge wa Kigoma Kusini, ambaye ni Mwanajeshi. Ni kweli mwanajeshi kweli kweli nampongeza. Mheshimiwa Halimenshi Mayonga - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Semindu Pawa - Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali - Mbunge wa Vitongoji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa George Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa, Mheshimiwa Bujiku Sakila - Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa Edson Halinga - Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Semindu Kisange Pawa - Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali - Mbunge wa Vitongoji, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa - Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame - Mbunge wa Kuteuliwa Zanzibar, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalillo - Mbunge wa Liwale, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu - Mbunge wa B.L.W., Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Mbunge wa B.L.W. Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi - Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Abdalla Khamis Feruzi - Mbunge wa Chake Chake.*(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Maokola-Majogo - Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Aisha P. Magina - Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Paul Kimiti - Mbunge wa Sumbawanga Mjini, Mheshimiwa Talala Bana Mbise - Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mheshimiwa Wilson Masilingi - Mbunge Muleba Kusini, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud - Mbunge wa Jang'ombe, Mheshimiwa Martha M. Wejja - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri - Mbunge wa Muleba Kaskazini na Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa, Mbunge wa Mwibara. *(Makofi)*

Pili, kwa dhati kabisa ningelipenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa pongezi nyingi ambazo zimetolewa kwa Mheshimiwa Rais na kwetu sisi hawa wote mliopo ambao mmetupatia pongezi, pongezi hizo ni za Rais, sisi ni Wasaidizi wake na ninaahidi pongezi hizi nitamfikishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na pongezi, Waheshimiwa Wabunge wametoa maoni maelekezo, maombi na mapendekezo mbalimbali ya msingi. Kwa yote haya, ningelipenda kuwahakikishia kuwa yatafanyiwa kazi katika kipindi ambacho nitakuwepo na pia nitaandikia maelezo kwa kina kwa ajili ya kufuatilia kwa watakaofuatia. Ukweli ni kuwa kwa usalama endelevu wa nchi yetu, yote yaliyoelezwa humu ni ya msingi na hayahitaji ushwishwi wa kipekee mbali na uendelezaji na hatua za utekelezaji.

Kama nilivyosema, nimejifunza mengi katika Wizara hii, inawezekana nidhamu katika Wizara hii ni sawa na fani yangu katika Udaktari. Hakuna ubishi! Unaambiwa, unafanya. Baada ya kufanya unajieleza. Kama umefanya vibaya cheti chako unanyang'anywa, hufai kuwa Daktari na Jeshini kadhalika. Sasa hapo mambo mengi siwezi kuyazungumza, yatatekelezwa ni amri. Yasipotekelezwa maelezo yatatolewa kwa nini. Kwa hiyo, nataka niwahakikishieni kwamba yatazingatiwa na yatatekelezwa. *(Makofi)*

Wakati huo huo, yako maeneo machache ambayo ningelipenda kuyatolea maelezo na ufafanuzi kama ifuatavyo:- Kwanza hoja imetolewa juu ya pongezi kwa *Commander in Chief,* Wizara na Uongozi wa Jeshi, Wajumbe wa Kamati Mheshimiwa Jackson Makwetta na Wabunge wote waliochangia pamoja na Msemaji wa Upinzani. Tumefarijika sana kwa pongezi, tutazifikisha kwa Kamanda na Wanajeshi na wafanyakazi wote. *(Makofi)*

Pili, nizungumzie juu ya ajira katika vyombo vya ulinzi kupitia JKT. Mheshimiwa Thomas Nyimbo amechangia, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga amechangia, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame. Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi. Hili ni agizo, hakuna maelezo. Kwa hiyo, nisiposema mengi huu ndio ujeshi wenyewe kwa sababu ukianza kutoa maelezo mengi utakosea. Kuna hoja imetolewa juu ya vifaa na mtaji kwa wanaofuzu JKT. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Thomas Nyimbo ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Barabara za mpakani ziimarishwe na uwekaji *beacons* mpakani utekelezwe, mpaka wa Msumbiji. Kamati ya Ulinzi na Usalama imetoa maelekezo. Mheshimiwa Omar Mjaka Ali amechangia na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Wizara itaangalia uwezekano wa kugharamia ukarabati wa barabara za mipaka na uwekaji wa *beacons* kadri ya mafungu yatakavyoruhusu na kama inawezekana tutaanza mwaka huu wa fedha 2005/2006. Ni pendekezo zuri tutalizingatia na Wizara ya Ujenzi. Nataka niwahakikishieni kwamba Wizara ya Ujenzi tuko nao karibu sana.

Hoja nyingine ni ununuzi wa madawa na sare za Majeshi toka viwanda vya JKT. Mheshimiwa Edson Halinga amechangia hoja hiyo na nataka nimhakikishie kwamba Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimeanza kununua madawa, utaratibu wa sare utaanza kwa JKT wenyewe na mgambo utaendelea kuimarishwa hatua kwa hatua.

Mishahara ya Wanajeshi vyeo vya chini viongezwe, aidha, utata wa gharama za *ration* kwa Sh.90,000/= kwa mwezi mmoja tu; hili limezungumzwa na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa George Lubeleje. Serikali inaendelea kuongeza viwango vya kukidhi gharama za maisha, hatua hizi zinatarajiwa kuendelea mwaka huu 2005. Maslahi yataboreshwa kama nilivyosema. *Ration* tarakimu sahihi ni Sh.60,000/= sio Sh.90,000/= kwa mwezi. Aidha, *ration* ni stahili ya chakula cha Mwanajeshi apewapo popote alipo ikiwa ni pamoja na mafunzoni, anapokuwa likizoni hupewa fedha taslimu na haiwezi kulipwa mara mbili. Sasa sheria hizi ziko katika kanuni za Jeshi hatuwezi kuzibadilisha. Tunapozibadilisha tunachukua tahadhari isije ikaingiliana na utaratibu wa Serikali.

Lakini suala la *ration* tumezungumzia na Wanajeshi wetu sasa wanakula vizuri sana na ningewaomba Waheshimiwa Wabunge mtakapokwenda katika Kambi watawakaribisheni tu. Mimi nimetembelea Kambi mbalimbali, nimekula na vijana, nimekwenda siku moja kwenye Kambi wameniandalia chakula changu *special*. Nilipokuwa nakwenda nikamwambia dereva geuza gari twende kula na vijana. Basi nilionja chakula hicho wala sikuamini. Ni chakula ambacho ni sawa na chakula ambacho kinapikwa katika hoteli mbalimbali.

Niliwauliza vijana wakasema Mzee tumeridhika. Nataka kuweka *standard* kwa sababu Wanajeshi wetu sasa wanashiriki katika mazoezi mbalimbali na wanakwenda kozi mbalimbali, Jumuiya ya Afrika Mashariki tuko pamoja, majeshi yetu yanashiriki pamoja hatutaki wakienda kule wajione wanyonge, wanasema wenzetu wanakula vizuri na wao wanakula kihunihuni tu. Kwa hiyo, hiyo *standard* imewekwa na haitarudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumbu kusaidiwa kuzalisha magari ya Nyumbu na Zimamoto. Hoja hii imezungumzwa na Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali. Serikali kwa kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara inaandaa mazingira mazuri ya uendelezaji wa viwanda vya magari nchini. Tunataka kuwa na viwanda vyetu vya Jeshi. Ndiyo sababu wale Wabelgiji walipokataa nikawaambia *go to hell,* basi tutafute sisi wenyewe. Nizungumze lugha ya kidiplomasia kama mtu amekasirika. *(Kicheko)*

Tutapata mitambo hiyo tutafunga na tumeanza kuandaa viwanda vya Jeshi hapa nchini. Ndiyo maana Nyumbu inafanya mambo mengi makubwa hatutaki kuyasema maana tukiyasema hawa wakubwa pia wataanza kusema eeh, basi haya mambo tuyaache hivyo hivyo, ikiwemo kuandaa sera ya kuendelea sekta hiyo. Tunaandaa sera ya viwanda ya Jeshi. Aidha, ushirikiano na Kampuni ya Ireland imefufuliwa, wamekubali watakuja. *(Makofi)*

Hoja ya mikopo mbalimbali kwa Maofisa na Askari, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame wamezungumzia sana. Wizara inatafakari uwezekano wa kuanzishwa kwa Mfuko wenye masharti nafuu kwa ajili hiyo. Lakini Wanajeshi sasa wanaweza kukopeshwa na wamejenga nyumba na kuna utaratibu ambao Mkuu wa Majeshi ameweka ili wasije wakakopeshwa fedha ambazo hawawezi kulipa. Kabla hawajakopeshwa lazima iangaliwe kama mshahara wake unalingana na mkopo huo. Lakini na sisi tunalifanyia kazi hilo, tumelijua.

Lakini nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Pawa. Mheshimiwa Pawa anatetea Jeshi sana na Mheshimiwa Ndeka, Mheshimiwa Nyimbo na hasa rafiki yangu Mheshimiwa Lubeleje pia ambaye ameomba kwa dhati JKT ya zamani ifufuliwe. Sasa mimi nina hakika mambo mengi ambayo tumefanikiwa ni kutokana na mchango wa Wabunge. Zamani Wabunge walikuwa wanaogopa kwenda Jeshini na Wanajeshi walikuwa hawataki kuonana na wanasiasa. Siku hizi imekuwa *symbiosis* na Mzee wangu Malecela alikuwa ananiambia kama kuna kitu ambacho kimetendeka katika awamu hii ni kwamba Wanajeshi sasa wana imani na Bunge, wana imani na wanasiasa jambo ambalo halikuwepo. Kwa hiyo, nakushukuru sana japokuwa unasema wewe si Askari ambaye una nyota, lakini Askari ambaye ana mwezi ni wa juu kuliko mwenye nyota. Kwa hiyo, nafikiri kuwekewa juu pale alama ya mwezi wewe ni mtu mkubwa sana. Kwa hiyo, nawashukuruni sana.

Mheshimiwa Ndeka ameweza kuchangia kwa kiwango kikubwa sana suala la ujenzi katika Jeshi. Amechangia miradi 20 na katika hiyo miradi 20 amechangia miradi 2 ya Jeshi. Kwa mfano Katumbi-Nkonkwa amechangia kujenga nyumba ya ulinzi JWTZ kwa Shilingi 215 kutoka mfukoni mwake kama Mbunge. Amechangia katika eneo la Kijiji cha Sibwesa ujenzi wa nyumba ya ulinzi JWTZ mabati *bundle* mbili Sh.300,000/=. Hii ndiyo inavyotakiwa.

Hili ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania, linatokana na ninyi wenyewe kwa manufaa yetu. Kwa hiyo, nakupongeza sana na wananchi wa Jimbo lako wananisikia. Kama ulivyosema juu ya Jimbo langu, msicheze na dhahabu wewe ni lulu. Kwa hiyo, tunakuhitaji katika ulinzi wa mipakani na katika uimarishaji wa Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upimaji wa eneo la Makambi, hili lilisemwa na Mheshimiwa Semindu Pawa. Wizara inaendelea na uhakiki na upimaji wa Makambi ili kuondoa migogoro iliyopo. Hili nimelifafanua kwenye hotuba. Uboreshaji wa zana za kijeshi. Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi limezingatiwa katika mwaka wa fedha

2005/2006. Aidha, uboreshaji utaendelea mwaka hadi mwaka kulingana na uwezo wa kifedha wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fujo zilizotokea Mjini Songea, hili lilisemwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Hapa mimi ningeomba tu niwaambie ndugu zangu, Jeshi wamefundishwa tofauti na raia wana miiko yao, wana maadili yao, wana taratibu zao na hasira zao ziko hapa hapa karibu. Msilazimishe Mwanajeshi awe raia. Haiwezekani! Ni Mwanajeshi! Sasa kwenda kupapasapapasa mke wa Mwanajeshi usingojee kwamba atacheka na wewe, atakupiga tu. *(Kicheko)*

Mimi nasema kwa moyo wa dhati na Mzee Malecela ametembea sehemu nyingi, ni shahidi. Majeshi mengine yanafanya vitu vya ajabu hata hawakemewi. Wanaweza kuingia Baa wanapiga watu wanatoka. Jeshi letu ni Jeshi linalojali watu, ni Jeshi la uadilifu, uaminifu tusiwachokoze jamani. Tuwaache hivyo hivyo. Ukiona anakuja, nenda pembeni. Sasa unamlazimisha aishi kama wewe sasa akiishi hatakuwa Mwanajeshi. Wana sheria moja, ukimchokoza mmoja wote umewachokoza, ndivyo walivyofundishwa. *(Makofi)*

Sasa mimi naomba kweli kweli acheni Wanajeshi wetu, ni vijana wenu wazuri, wanawafanyia kazi nzuri. Haya mambo kila siku Wanajeshi kwenye mabasi na kadhalika, Mahita anakuja mawe mchukue. Sasa wanawalindieni mipaka yenu ninyi mko pale kwenye disko, kwenye harusi mpaka asubuhi hakuna anayewabughudhi wao wanalala huko msituni. Hivi kuwachukua kwenye gari hata kuwaonyesha kwamba bwana tunawashukuru sana, matatizo yakitokea wao ndio wako msitari wa mbele. Sasa na ninyi toeni mchango msichokoze Wanajeshi, narudia. Hata mimi siendi Kambini kama Waziri wa Ulinzi bila *Order* ya Mkuu wa Majeshi, nitafukuzwa. Ndiyo utaratibu wa Jeshi. Waacheni jamani. Ama sivyo mnataka Wanajeshi wetu wawe kama Wanajeshi wa Marekani. Mnajua mambo waliyoyafanya.

Lakini Jeshi hili lina maadili yake, kuna falsafa yake na ndiyo tunaheshimika dunia nzima. Ninapozungumza hapa, nchi nyingi wameomba kuja kufanya mazoezi na sisi tumekataa. Wanasema Jeshi la Tanzania ni zuri sana. Ninyi ni mashahidi wakati wa vita vya Kagera. Wahaya walipigwa kama watoto wadogo wanakimbia ovyo tu na wengine walisharudi Uganda, Jeshi la Ulinzi likawafuata wakavuka Entebbe wakawarudisha Kampala. Sasa hili ndilo Jeshi la Ulinzi la wananchi msilichokoze. Kwa hiyo, suala zima la fujo zilizotokea Songea bado linaendelea kufanyiwa uchambuzi wa kubaini kiini cha suala zima ni nini. Maana juzi kuna watu wengine wanasema aah, wanaringa sana Wanajeshi wamevaa nguo zao zile wanajiona. Eeeh, ndio ujeshi. Sasa kwa nini asiringe? Sasa unataka aishi kama wewe tu! Kuna mbwembwe, lazima aringe! Hata huyu adui anapokuja akipita Mwanajeshi, atakimbia sasa wakiwa kama raia itakuwa Jeshi gani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kurejesha mafunzo ya JKT kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Suala hili limesemwa na Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Dokta nakuheshimu. Hili tutalifanyia kazi na imeshajibiwa. Ngoja kwanza tuanze Makambi ya JKT Kiwilaya tutekeleze agizo la Rais. Mimi naamini kabisa tutapunguza umaskini kwa asilimia

kubwa.  Kama hawa vijana watahudhuria mafunzo katika kila Wilaya na wafundishwe hapa kidogo wawe na nidhamu wapewe nyenzo za kufanyia kazi nchi itainuka na ndiyo hii nguvukazi ambayo tunataka kuijenga.

Mheshimiwa Wilson Masilingi, mjukuu wangu.  Shukrani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuanzisha Kambi ya JKT Burigi Muleba.  Kitu kilichotufanya Kaboya ilikuwa ni Kambi ya JKT na kutokana na vurugu za Amin, tuliwanyang'anya Wahaya tukaweka Kambi ya Jeshi.  Sasa tunawarudishia.  Nakushukuru sana jinsi ulivyohangaika na suala hili na ndiyo Wilaya peke yake ambayo imetupatia eneo kubwa maelefu ya eka.  Wanasema hata pori lote chukueni kutokana na huyu kijana.  Sasa wananchi wa Muleba Kusini nasema tena kama nilivyokutana na ninyi msicheze na Masilingi.  Mna kijana shupavu, mwaminifu, mwadilifu ana heshima kubwa na ananipa shikamoo kila wakati nikikutana naye.  Naomba mpeni kura, mpitisheni Masilingi. Mimi kama babu yenu nikiwaomba mkikataa, nitawalaani.  *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Hospitali za Jeshi kutoa tiba kwa wananchi wote.  Mheshimiwa Mohamed Rajad Soud pongezi zimepokelewa.  Walimu watarajiwa wapewe mafunzo ya kijeshi miezi sita ili wawe wakakamavu.  Hili liliulizwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila.  Nataka kuwahakikishieni kwamba kati ya vijana ambao wanapata mafunzo JKT hata vijana wenye shahada wapo na wengine wana *degree*. Wanapokuja wanamwuliza mbona wewe una *degree* na elimu ya juu nimekosa kitu kimoja, nidhamu na uzalendo na Utanzania.  Nataka nishirikiane na Watanzania wenzangu.  Kwa hiyo, sio kupata mafunzo tu, lakini hata kule kuwa na uzalendo, mshiriki pamoja kumleta Mhaya kutoka kule Kagera anapambana na Mngoni ni kitu muhimu sana.  Baadhi yenu hapa amani hii tuliyonayo na urafiki imetokana na JKT.  Bila hivyo, kila mtu angezungumza lugha yake.  *(Makofi)*

Uzalishaji wa mazao ya chakula Mbozi uongezwe.  Mheshimiwa Edson Halinga mimi nilikuwa kwako, ulinitembeza katika eneo lile, nakushuru sana.  Wananchi wa Mbozi wananisikia, mna mtu hodari mnasikia mchango wake hapa Bungeni, nataka nikuhakikishieni kwamba ushauri wako utazingatiwa.  Kambi ya JKT yaliyofungwa kama vile Mpwapwa JKT yafufuliwe.  Aidha, mafunzo ya JKT yaende hadi Vijijini. Mheshimiwa George Lubeleje nakushukuru sana, suala hili umekuwa unalihangaikia miaka mingi tangu nimeingia hapa Bungeni umekutana na mimi sasa suala hili limefika mahali pake dawa iko tayari.  Rais ameagiza tuanzishe Makambi ya Jeshi kwa kila Wilaya na tutaanza na hii Wilaya ya Mpwapwa.  Suala hili liko katika sehemu ya agizo la Rais kwa hiyo, tutaliingiza hatua kwa hatua maana tutaanza na majaribio.

Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi na Mheshimiwa Paul Kimiti wamezungumzia huduma ya mawasiliano. Kambi ya Potoa ni mojawapo kati ya vituo 17 vipya vitakavyojengewa mitambo ya mawasiliano chini ya awamu ya tatu ya mradi wa *ITN* unaoendelea kutekelezwa.  Kwa hili tutalitekeleza.  Sasa Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi waambie kwamba hili limetekelezwa na ndugu yangu Zubeir yuko pale nakushukuru sana ulinichukua mpaka nikaenda kule na mara ya kwanza akasema aliingia Ikulu tukapiga picha na Rais wa Zanzibar.  Kwa hiyo na Rais wa Zanzibar aliniahidi

kwamba atapeleka maji. Nakushukuru sana pamoja na Khadija kwa kazi mnayofanya kuhusu Jeshi letu. *(Makofi)*

Jeshi la Mgambo kuunganishwa na Sungusungu Mheshimiwa Edson Halinga alilisemea. Hili ndugu yangu haliwezekani kwa sababu Sungusungu wana taratibu zake. Lakini ni wazo zuri. Sasa Msukuma yule wa Sungusungu maana yeye ni Msukuma hawezi kufanya kazi ya Jeshi sababu hili ni suala la Kijiji, Mitaa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Lakini Jeshi lina masharti yake. Sasa utamweka pale umpe masharti Msukuma atakimbia tu kwa sababu amezoea mambo ya Sungusungu ya Vijijini. Lakini ni wazo zuri.

Vyeti vya Wahitimu Mgambo Wilaya ya Liwale, Mheshimiwa Kigwalillo namshukuru sana, sijui amekwenda wapi, nampongeza. Hili alifanyie ombi maalum na aliagiza kwamba waanzie kule kwake kwa sababu ni Wilaya ambayo imesahaulika sana na Mgambo wanafanya kazi nzuri na marekebisho yamekamilika na vyeti vitaanza kutolewa kwa wahitimu wa Mgambo katika kipindi cha miezi mitatu ijayo kuanzia mwaka huu 2005, tumezingatia.

Nyumba kumi *THB* Kibaha, Mheshimiwa Aisha Magina, Mbunge wa Viti Maalum, nyumba kumi zilizochukuliwa na Jeshi kutoka iliyokuwa Benki ya Nyumba *THB*. Wizara imeshafanya ukaguzi na tathmini kwa lengo la kuzifuta ziwe mali za *THB* na nyumba hizi zitauziwa Wanajeshi kama ulivyoomba. Ujenzi wa barabara za mpakani na alama za kudumu *beacons,* hili limesemwa na Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. Kuhusu ujenzi wa barabara za mipakani imekamilika. Zoezi la kuimarisha barabara zote za mipakani. Kazi inayoendelea ni kukamilisha kutathmini gharama zinazotakiwa kuzijenga ikiwa ni pamoja na kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili kuziombea fungu maalum la fedha ili kuzijenga kikamilifu.

Nataka nimshukuru sana Mzee wangu John Malecela suala hili amelizungumzia sana kwa uchungu kwamba je tukivamiwa barabara zetu hizo Wanajeshi watakwenda kwa miguu mtapelekaje vifaa vya kijeshi. Kuhusu alama za mipakani *beacons.* Wizara yangu inazingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Makazi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kutekeleza. Tutafuatilia na Mheshimiwa Waziri yuko hapa nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Cheyo kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Wizara yake. Kama kuna Wizara ambayo imefanya kazi nzuri ni Wizara hii. Tulikuwa tunashirikiana naye kwa karibu sana na kutokana na jitihada zake tumeweza kupima maeneo mengi ya Jeshi ambayo yangechukuliwa na wavamizi.

Mheshimiwa Spika, huduma za miundombinu katika Makambi; kwa mfano maji, umeme, barabara; hii imezungumziwa na Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, na Mheshimiwa Waziri Edgar D. Maokola-Majogo. Wizara imeanza kuboresha miundombinu kwa kutumia fedha kidogo inayopatikana katika fungu la maendeleo.

Imeanza kukarabati, uboreshaji wa miundombinu. Kwa sasa Wizara inaendelea na ukarabati wa mifumo ya maji taka katika Kambi za Lugalo, Keko *Navy*, na Mirambo - Tabora. Aidha, imeanza mradi wa maji safi katika Kiteule kilichoko Bumbwini Unguja, hilo pia tutalianza Magharibi. Kama ilivyofanyika Bumbwini, Wizara itatumia wataalam katika kutathmini kwenye Kambi ya Potoa ili mradi huu uweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Katika Mwaka wa Fedha uliopita, kazi za ukarabati wa nyumba mbalimbali Visiwani Unguja na Pemba unaendelea. Aidha, utaratibu huu umepangwa kuendelea katika mwaka huu wa Fedha, hivyo nyumba za waliooa na kuolewa katika Kambi ya Potoa zitafanyiwa ukarabati. Aidha, kwa kuzingatia ushauri wa Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Wizara yangu itaanzisha mazungumzo na Mamlaka iliyofikisha maji Chalinze ili kuona uwezekano wa kufikisha maji katika Kambi ya Kizuka na Sangasanga. *(Makofi)*

Kama ilivyo kwa madaraja mengine ambayo ni ya utendaji kivita yaliyojengwa wakati wa maafa katika maeneo mbalimbali kote nchini, Daraja la Ubena Zomozi ni mojawapo. Kiutaratibu madaraja haya yanatakiwa yarejeshwe Jeshini kwa mahitaji ya dharura yaliyokusudiwa. Hata hivyo, imeshindikana kufanya hivyo kutokana na kwamba Wizara ya Ujenzi haijakamilisha ujenzi wa madaraja ya kudumu katika maeneo hayo. Lakini ninataka nikuhakikishie kwamba Wizara yangu itafanya mawasiliano na Wizara ya Ujenzi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu ili madaraja hayo yajengwe na yale ya Jeshi yarejeshwe.

Kuhusu kuweka vifusi katika barabara mbovu, Wizara itajitahidi kukarabati barabara hizo kama alivyoomba Ndugu yangu Mheshimiwa Semindu K. Pawa na tutatuma wataalam kwenda kutazama daraja hilo na kuona kama tunaweza kufanya na kama hatutaweza kufanya, tutatafuta mbinu nyingine. Lakini nampongeza sana kwa ushirikiano wake na Wanajeshi wetu.

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Semindu K. Pawa na Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame walizungumzia Askari kurejeshwa Makambini. Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa viporo vya nyumba Makambini. Pia ujenzi wa nyumba mpya umeanza katika Makambi mbalimbali na utaendelea katika mpango wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa George M. Lubeleje alizungumzia kuhusu usafiri kwa Wanajeshi. Serikali imeanza kununua magari makubwa na madogo katika Mwaka wa Fedha 2004/2005 na itaendelea na zoezi hili katika Mwaka wa Fedha 2005/2006 ili kupunguza tatizo hili. Kwa kweli, kwanza tumpongeze Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama, amekuwa mfuatiliaji wa karibu sana. Mara nyingi hata usiku anakwenda kuona Mkubwa zaidi na amefanya kazi nzuri sana na Amirijeshi Mkuu akaniambia kwamba Jeshi hili lazima liwe Jeshi kweli kweli kama ilivyokuwa wakati wa Ukombozi wa Bara la Afrika. *(Makofi)*

Nilikwenda katika nchi fulani ya kirafiki, anasema Watanzania msifanye kosa, *when you have the power – military power*, ndiyo sauti yako inaweza kusikika katika dunia ya siku hizi. Kama huna uwezo utawekwa pembeni tu. Lakini hilo siyo hoja, la muhimu Jeshi letu hili lina historia. Lazima libaki Jeshi la kujivunia. Kwa hiyo, liimarishwe na wakasema tutawasaidia na wanaendelea kutusaidia. Sitaki kutaja ni nchi gani. Kwa hiyo, suala hili la kuimarisha Jeshi ni jukumu letu sote na Jeshi hili haliwezi kufadhiliwa na Wahisani kama Wizara nyingine. Akishakufadhili, basi atakuwa na sauti. Hili ni Jeshi letu wenyewe kwa maslahi yetu na lazima tulishughulikie, tujinyime na ndiyo nataka nimpongeze rafiki yangu wa Kambi ya Upinzani, amekataa mambo ya kipumbavu yanayoandikwa juu ya Jeshi. Futa hayo yote!

Mimi nakushukuru sana, umeihakikishia dunia, katika ulinzi tuko pamoja, hakuna itikadi na uendelee kuwa hivyo hivyo. Haya mambo mengine huko sijui nani kakunyang'anya mke wako, mligombana nini, achana nayo. Lakini inapokuja katika suala la ulinzi tuko pamoja na nakushukuru sana. Kwa hiyo, Jeshi tutaliimarisha kwa manufaa yetu na Waheshimiwa Wabunge, baadhi ya Wabunge wamesema kwamba Bajeti iongezwe, lakini Bajeti imeongezwa kwa kipindi cha miaka tissa tu kutoka asilimia ndogo 100 mpaka asilimia 386, sio haba. *(Makofi)*

Tumpongeze sana Amiri Jeshi Mkuu. Bila yeye kuingia hapa, Jeshi hili lingekuwa linadharauliwa tu. Alikuja Kiongozi mmoja Dodoma kuona Gwaride, aliandika kwenye gazeti: Hajaona Jeshi *smart* kama Jeshi letu hili. Hili ni Jeshi gani hili! Amesema amehudhuria hata nchi kubwa hakuna Jeshi *smart* kama hili na wanavyotembea wanavyopiga *mark time* utafikiri wameunganishwa pamoja." Alishangaa sana na akasema hii kweli ni nidhamu ya hali ya juu. Kwa hiyo, hata mataifa makubwa wanajua tuna Jeshi kweli kweli na kwa hiyo, Jeshi hili lazima tulihudumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali na Mheshimiwa Edson M. Halinga walizungumzia kuimarishwa kwa Mashirika ya uzalishaji mali ndani ya Wizara ya Ulinzi. Wizara itawasiliana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuona uwezekano wa kupatiwa eneo la *TAMCO*.

Tumeipongeza Serikali kwa kutoa Kandarasi za Ujenzi wa JKT. JKT inafanya kazi nzuri hasa katika ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Serikali. Hawa jamaa wa JKT, ninaomba Waheshimiwa Wabunge msihangaike na hawa wababaishaji. Tuna *Brigade* zetu Kanda tano. Kama uko Dodoma – Shinyanga, wapo, waite. Watakujengea kwa miezi miwili tu, una nyumba ya kisasa nzuri mno kwa gharama nafuu. Kwao hakuna kuongeza gharama, sana sana wanapunguza na kama imezidi wanarudisha. Hii ndiyo JKT. Kwa hiyo, mtumie JKT yenu na nashukuru sana Viongozi wa Serikali wanaotumia JKT katika Wilaya na Mkoa. JKT ndiyo nguvu kazi kubwa na Waheshimiwa Wabunge tumieni JKT na mimi nawatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Lubeleje alizungumzia uboreshaji wa huduma za usafiri kwa Wanajeshi hasa Vikosi vya Ihumwa na Makutopora. Mheshimiwa George Lubeleje anapenda Wanajeshi sana, sijui mtoto wake yuko Jeshini ama ndugu yake. Lakini kama sivyo, yeye ni mwanajeshi ambaye ni *reserve*, eeh! Unawaonea huruma! Mheshimiwa nataka kukuhakikishia kwamba Wizara ina mpango wa kununua mabasi katika mwaka wa Fedha 2005/2006 kwa ajili ya kuboresha usafiri Vikosini. Tumeshapeleka *Ambulance* katika Vikosi vyote nchi nzima, tumepeleka *Ambulance* mpya, mpaka Kaboya kwa Wahaya. *(Makofi/Kicheko)*

Tumekubali, Amiri Jeshi Mkuu amekubali na tumetenga pesa kwa malipo ya awali ya *Helicopter* nne. Lazima tuwe na *Helicopter,* nchi yetu hii ni kubwa. Tumenunua zaidi ya magari 600 lakini bado tutaendelea. *Boat* za doria zinakuja Mwezi wa Oktoba. Kwa kuanzia tunakuja na *Boat* 15 lakini tunaleta sita na kabla ya mwisho wa mwaka *Inshallah*, Mwenyezi Mungu akipenda tutakuwa na *Boat* nyingi tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Paul Kimiti, wamezungumzia kuongezwa kwa Shule za Sekondari zinazoongozwa na Jeshi. Wizara itazingatia ushauri wa kuongeza hizo Shule na nataka nimshukuru sana Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa kutupatia gharama ya uendeshaji asilimia 40 kwenye Shule zetu za Sekondari. Vile vile Wizara itafikiria uwezekano wa kuongeza idadi ya vijana wa kujiunga na JKT kutoka Zanzibar kama alivyoomba Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. Aidha, utekelezaji agizo la Mheshimiwa Rais kufikisha JKT Wilayani. Litafanyiwa kazi kurahisisha hatua ya kuwa vijana wengi kuweza kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Ushauri umezingatiwa, maeneo yamekwishapatikana na baadhi ya Wilaya zikiwemo Rufiji, Mkuranga, Muleba na Handeni.

Kwa hoja za Upinzani, Waziri Kivuli mimi nakushukuru sana. Nataka nimshukuru sana Makamu wangu Shekh Khalifa Suleiman Khalifa ambaye hapa tumepangana wenye vipara, tuna Chama chetu na mimi ndiye Mwenyekiti, yeye ni Makamu wangu na Katibu wangu ni Halimenshi K. R. Mayonga. Kwa hiyo, tunakwenda pamoja. Yeye ameniambia, kama hawakutaki kule kwenu njoo katika Jimbo langu uwe Mgombea wa *CUF*. Nakwambia Bwana nakushukuru sana, siwezi kusaliti Chama changu, hata wasiponipa kura nitabaki mwana-CCM. Lakini Jimbo lako likirudi CCM, nitakuja kugombea, nitapokea mwaliko wako. *(Makofi/Kicheko)*

Waziri Kivuli amezungumzia kuwaenzi Viongozi wa Jeshi Wastaafu kwa kuita Vikosi na Makambi majina yao. Suala hili limetekelezwa siku zote kulingana na utaratibu. Sasa kuna taratibu Jeshini, huwezi kubomoa Makambi na kuita, sasa itakuwa ni Makambi ya aina gani. Kuna taratibu na sheria za kuita Jina Kambi fulani.

Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir amezungumzia kuimarisha shughuli za Michezo katika Majeshi. Michezo ni sehemu ya shughuli za Kijeshi. Tunatambua

itaendelea kuimarishwa kadri hali ya fedha inavyoruhusu. Suala la shughuli za michezo limepokelewa na tutalifanyia kazi. Hata hivyo, tumeongeza Bajeti ya michezo. Wanamichezo wetu wa *Handball*, *Basketball* wanaongoza katika Kanda hii ya Afrika. Tulifanya michezo ya Majeshi ya Afrika Mashariki, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilichukua nafasi ya Kwanza Kampala. Kama nilivyosema, *Trans Camp* na Ruvu JKT, vilabu hivyo vinatisha na tishio kwa timu kubwa kama Yanga isipokuwa kwa Timu ya Simba hawana bao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud amezungumzia muda wa malipo ya Pensheni kupunguzwa toka miezi sita hadi miezi mitatu. Suala limepokelewa Kiserikali na ninasema Waziri wa Fedha alishatamka, sasa sheria inatungwa kwamba badala ya miezi sita itakuwa miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu amezungumzia mafao ya Wanajeshi wanaostaafu. Utaratibu wa malipo ya mafao katika Jeshi upo wazi na hauna mianya ya rushwa na wala haubagui kati ya wastaafu wa Bara na Zanzibar. Kama kuna mstaafu yeyote ambaye ameshawahi kudaiwa au kutoa rushwa, basi atoe taarifa kwa uongozi. Hapa nataka niwahakikishieni kwamba mimi mwenyewe suala hili nimesimamia na Mkuu wa Majeshi. Kuanzia mwaka 2001, tatizo la wastaafu halipo tena kwa sababu wameingizwa kwenye kompyuta. Tatizo tulilonalo ni kuanzia mwaka 2000 mpaka 1980 na kitu huko nyuma. Lakini tumeshaunda timu ya Wanajeshi na wataalam ambao wanakwenda huko Mikoani kuwafuata huko huko kutafuta maelezo na yakipatikana wanalipwa.

Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud na Mheshimiwa Semindu Pawa walizungumzia ujenzi na ukarabati wa miundombinu na maji katika Makambi ya Potoa, Pangawe, Daraja la Ubena, *Umoja Camp* Mtwara, ujenzi wa Hospitali Pemba.

Wizara itaendelea na juhudi za kukarabati na ujenzi wa miundombinu kadri fungu linavyoruhusu. Lakini hili suala la Pemba na mimi nimeliona ni muhimu sana. Hatuwezi kukubali Pemba ambayo iko mbali sana na Unguja, nafikiri Pemba iko karibu sana na Tanga. Hili suala tutalifanyia kazi, nitaagiza kule Wawi na sehemu nyingine tuanze kufanya utaratibu kujenga Hospitali. Maana hao ni ndugu zetu, hatuwezi kuwatupa, tu wamoja, damu moja, nchi moja tumeungana. Sasa Wapemba yakhe wana kosa gani? Kwa hiyo, hili tutalifanyia kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Aboud ameelezea kuhusu suala la kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo maeneo ya mipakani na kuongezeka kwa ujambazi ameshauri vyombo vya ulinzi na usalama viimarishe *co-ordination* ili kuongeza ulinzi. Aidha, doria katika ziwa Tanganyika ziongezwe. Vile vile, Mheshimiwa Mayonga amesemea sana kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tutapata maboti na maboti haya mengi tutayapeleka Ziwa Tanganyika. Lakini kwa wakati huu, yatafanya kazi kuona mambo ya bahari, maana bahari yetu pia ni kubwa. Wakati wa uchaguzi tutafanya doria, lakini baada ya hapo tutazipeleka Ziwa Tanganyika na nyingine zitakwenda Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa. Ni lazima tulinde mipaka yetu ya majini, nchi kavu na anga. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa tu tunalinda mipaka kati ya Tanzania na Malawi, lakini *Lake Nyasa* tunaacha wazi. Kwa hiyo, suala hili tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, tulionelea kwamba ni muhimu tuwe na Viongozi wa Serikali ambao wana ujuzi wa ulinzi, ndiyo sababu Serikali imepeleka Viongozi katika Wilaya zote za Kigoma na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla na sasa mmesikia mambo yaliyotokea, wameanza kurudisha silaha wenyewe. Wamepewa amri, lakini sasa wengine watakuwa wamepotea na nikisema lugha kwamba mtu amepotea mnanielewa. Kwa hiyo, asiporudisha kama ni mkimbizi amepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kuanzia leo bado wiki moja Bunge lako litatimiza uhai wake, niseme machache tu. Kwanza, kwa miaka mingi Bunge lako limefanya maamuzi mazito, Miswada mingi ilipitishwa na Rais kukubali ianze kutekelezwa. Maswali mengi yaliulizwa na kujibiwa bila matusi kama Mabunge mengine. Bunge lako limeonyesha mfano wa kuigwa, ndiyo maana ulichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri walizofanya. Wabunge hawa wamefanya kazi nzuri sana na ninaamini kwamba wananchi waliowachagua watawarudisha tena. Kila maendeleo tunayoyaona katika nchi yetu na mafanikio ni kutokana na Wabunge. Sasa wanapitapita watu wengine wanasema hakuna kilichofanyika. Kwanza wanawatukana wananchi na wanatukana Chama cha Mapinduzi ambacho wanaomba kura kupitia kwake. Kama kuna ukweli, hawa watu ambao wanapitapita waseme mambo yaliyofanyika ni makubwa na Mbunge amefanya kazi. Lakini mimi naomba kama fulani, sera yangu ni hii, ni hii, ni hii. Lakini hana sera! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako ni Bunge linaloongozwa kisayansi. Spika wa Bunge aliwahi kuwa *Vice Chancellor* na *Vice Chancellor* hawezi kuruhusu utovu wa nidhamu Bungeni. Asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ama walikuwa wanafunzi wako au wafanyakazi wako. Hivyo, mafanikio makubwa yaliyopatikana Bungeni ni kutokana na jina lako wewe Pius Msekwa. Ni jina zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila baharia anaweza kuongoza meli. Ukimpa ile ya kuongoza tu anakwenda, lakini anamchukua nahodha kuongoza njia ya meli. Siyo kuongoza tu, lakini kupanga safari ya meli. Siyo kupanga tu, lakini pia namna ya kupambana na dhoruba hadi kufikisha meli Bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati umekuwa nahodha wetu hodari. Umefikisha meli yako hii Bandarini, Bandari Salama. Lakini nakutakia maisha marefu

na ninakuomba urudi kuongoza meli yetu. Nasema urudi kuongoza meli yetu kwa kuwa safari bado ni ndefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Amirijeshi Mkuu - Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa heshima aliyonitunuku, kuniteua kuwa Waziri wake wa Ulinzi. Lakini nimshukuru zaidi kwa kunivumilia, maana kila mtu ana tabia yake. Rais ni mtu mvumilivu sana. Sijamwona amekasirika, kila wakati akikuita, Waziri njoo, kwanza unajiuliza leo kuna nini? Hakwambii! Ukienda kitu cha kwanza ni kucheka, anakurudisha moyo. Amenivumilia sana na mara nyingine kukubali ushauri wangu. Marais wengine huwezi kumshauri, atasema, wewe ni nani unanishauri? Lakini yeye anakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana kwa kunielekeza kuhusu mambo mazito kuhusu ulinzi wa Taifa letu. Haya mambo yote siwezi kuyasema hapa, lakini anasema nenda ufanye hivi, nenda ufanye hivi, nenda ufanye hivi. Baadaye narudi kumwambia Mheshimiwa Rais, tayari. Anasema, barabara, endelea. Ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kuwa Mheshimiwa Mkapa ni mrithi halali wa Baba wa Taifa, Marehemu Julius Kambarage Nyerere. Narudia tena, mimi naamini na Waheshimiwa Wabunge pia wanaamini na wananchi wa Tanzania wanaamini pia kuwa Mheshimiwa Mkapa ni mrithi halali wa Baba wa Taifa, Marehemu Julius Kambarage Nyerere. Alikuwa karibu naye sana, alimheshimu, alifuata nyayo zake za uadilifu, upendo, ushupavu, upole na ukali. Ukitaka kumkosea Rais, mkosee uone jinsi alivyo mkali, utakimbia! Kama uko kwenye chumba utasema, mbona hiki chumba kidogo? Hata milango hautaiona! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalendo na uchapakazi wake hauwezi kuulinganisha na wa mtu yeyote. Alipokuwa mgonjwa baada ya *operation* aliendelea na kazi, namwambia Mheshimiwa Rais, baki nyumbani, alikataa kufanya hivyo. Alifanya kazi kama Amiri Jeshi Mkuu na alituonyesha mfano na ana moyo wa Baba. Tunaomba Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na afya njema. Taifa letu bado linamuhitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mzee wangu Dr. Samwel John Malecela. Mzee huyu kwangu ni kijana wa miaka mingi, kwani kuna vijana wa miaka michache. Unamwona kijana wa miaka 40 unafikiri ni mzee wa miaka 60. Lakini kuna wazee wa miaka mingi, lakini ni vijana na mmojawapo ni mzee wangu Samwel John Malecela. Ni mzee mwenye hekima, busara, uongozi uliotukuka, anayependa sana watu wote. Amenisaidia sana katika nafasi yangu ya uongozi tangu alipokuwa Waziri wangu Mkuu hadi leo kama Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Kaka na mzee wangu nakushukuru sana, nenda ugombee Ubunge. Wapigakura wako watakurudisha Bungeni, bado Taifa linakuhitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa heshima kwa Waheshimiwa Wabunge. Nasema, mafanikio yote yaliyopatikana ni kutokana na uongozi wenu. Ninyi mlikuwa kioo, sauti na macho ya wananchi hapa Bungeni. Mmetekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa

asilimia kubwa sana, wananchi wa Tanzania wana macho, wana akili, wanapenda maendeleo, watawarudisheni wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wapigakura wangu wa Jimbo la Rorya, kwa imani waliyonayo kwangu. Ninawaambia tumefanya mengi kwa pamoja na ninyi ni mashahidi, nakuja. Sasa natangaza rasmi, nakuja. Nakuja ili tuweze kupanga tena maendeleo ya Jimbo letu. Mimi sina wasiwasi na ninyi, tutashinda tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 38 – Ulinzi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... ... Sh.156,127,395,200/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *The National Service Force* ... ... ...Sh.36,421,689,800/=

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1001, *sub-vote* 250100, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, kuna vikosi vitano vya JKT ambavyo vinafanya kazi za ujenzi na akataja kwamba Mkoa wa Shinyanga wanaweza kupata. Je, vikosi hivi vyote vitano viko Mkoa ya Shinyanga tu au viko katika Mikoa mingine? Kama vipo katika Mikoa mingine, ni ipi? Nashukuru.

**SPIKA:** Na hasa Lindi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Napenda kutoa ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa sana Maria Watondoha; Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Siyo vikosi, tuna Kanda za Brigedi za Ujenzi. Kwa mfano, nilisema tu Shinyanga kwa sababu ya rafiki yangu Dr. Ng'wandu, lakini Mikoa yote imezingatiwa. Kuna Kanda ya Mashariki na Kanda ya Kusini ambayo hata Mkoa wa Lindi umezingatiwa. Kwa hiyo, ime-*cover* Tanzania nzima. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Watondoha, usiwe na wasiwasi. Kama unataka ujengewe nyumba, Mkuu wa JKT yuko hapa unaweza kumwona na kama kuna kitu ambacho unataka, hata

Shule kujengwa yuko hapa na amefanya kazi nzuri. Lakini ni Mikoa yote ya Tanzania nzima.

*(Hapa Mheshimiwa Watondoha alisimama akitaka kuendelea kuzungumza)*

**SPIKA:** Umeshapata nafasi yako inatosha, tunaendelea. Hapa siyo mahali pa kubishana.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... .... Sh. 5,519,215,000/=
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*... ... ... ... ...Sh. 102,003,200/=
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*... ... ... ... ... ..Sh. 44,961,700/=
Kifungu 2001 – *Industries, Construction and* .....................................
*Agriculture* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 212,997,700/=

*(Vifungu Vilichotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 38 – Ulinzi**

Kifungu 1001 – *Administration and General* ... ... ... Sh.506,000,000/=
*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*... ... ... ...Sh.200,000,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 2001 – *Industries, Construction*
*and Agriculture* ... ... ... ... ... ... Sh.45,010,000,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kuketi kama Kamati ya Bunge ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2005/2006 kwa ajili ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa limeyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja kwamba makadirio hayo sasa yakubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(*Makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.04 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 25 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*